**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

*(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

DUA

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**Nam. 20**

**Kukemea uuzwaji wa Pombe za Kienyeji**

**Mhe. Salim Abdallah Hamad: (kny Mhe. Saleh Nassor Juma): -** Aliuliza**:**

Kwa kuwa mwishoni mwa mwaka 2014. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Wawi walifanya ziara ya kushtukiza katika eneo linalouzwa pombe za kienyeji (Mochwari) liliopo Fidel Castro Sec. School ili kujionea wenyewe eneo hilo hatarishi na lenye kuathiri afya za vijana wetu huku wakiwa pamoja na OCD Chake-Chake na Mkuu wa Wilaya na walijionea wenyewe hali ilivyo mbaya.

Je, tangu siku hiyo Serikali imechukua hatua gani katika kukemea maovu yanayofanyika Mochwari.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Saleh Nassor Juma kwa mashirikiano yake na Wizara yetu na Jeshi la Polisi katika kupambana na vita vya uhalifu katika Jimbo lake. Aidha, napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kwamba kufuatia ziara hiyo ya kushtukiza tuliyoifanya mwishoni mwa mwaka 2014 ambayo nilifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Spika, baada ya ziara hiyo tuliagiza Jeshi la Polisi kuchukuwa hatua mara moja na Polisi walifanya msako na doria katika eneo hilo la Wawi kwa nyakati tofuati na kufanikiwa kuwakamata baadhi ya watuhumiwa pamoja na kukamata madawa ya kulevya na malighafi ya kutengenezea pombe haramu.

Mhe. Spika, katika msako huu, jumla ya wanaotuhumiwa sita wamekamatwa na madawa ya kulevya, kete 178, bangi nyongo 74 pamoja na pombe haramu aina ya

Kangara na pipa tatu za malighafi (Mapapai bovu) la kutengeneza pombe haramu aina ya gongo. Tayari watuhumiwa hao wamefikishwa Mahakamani na kesi zao zinaendelea.

Mhe. Spika, Serikali inasisitiza kuwa kazi hiyo ya msako na doria ni endelevu na yeyote atakaehusika na kufanya maovu katika eneo hilo la Wawi pamoja na maeneo mengine nchini atakamatwa na kuchukuliwa hatua za Kisheria.

**Mhe. Salim Abdallah Hamad:** Mhe. Spika, kwanza nitoe pongezi za dhati kwa kupitia kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais kwa kutembelea pamoja na wenzake waliona tukio na kuchukuwa hatua kama iliyochukuliwa, nawapongeza sana kwa hilo. Lakini Mhe. Spika, kwa sababu ulevi ni kileo na si rahisi mwenye kuanza kulewa akaweza kuacha kwa urahisi na kwa sababu hawa ni binaadamu suala ni kuwa baada ya hatua nzuri iliyochukuliwa kama ilivyoelezwa je, serikali imeendelea na uchunguzi zaidi kuona kuwa hakuna sehemu nyengine ambayo watu hawa waliobakia na waliokuwa hawakukamatwa na makosa haya wamehamia na kuendelea na kazi yao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa sikumsikia vizuri Mhe. Mwakilishi naomba arudie tena swali lake, ili niweze kumuelewa vizuri.

**Mhe. Spika:**Mhe. Salim Abdallah Hamad rudia swali lako na huku ukielekea *mike*.

**Mhe. Salim Abdallah Hamad:** Mhe. Spika, swali ni kuwa kwa sababu ulevi ni kileo kibaya sana na pamoja na hatua nzuri iliyochukuliwa na naipongeza. Je, serikali imeendelea na kufanya uchunguzi endelevu kuona kuwa hawa wanaobakia na kutokana na ugumu wa kuwacha kileo cha ulevi si rahisi hawajahamia pahala pengine na kuendelea na kazi yao baada ya hapa Mochwari.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kama nilivyosema katika swali mama kwamba ni marufuku kufanya vitendo vyovyote vile kinyume na sheria na sio tu katika eneo au katika jimbo la Wawi bali mahala popote pengine nchini. Vitendo hivyo havitoweza kuvumiliwa na tayari kupitia Jeshi la Polisi imeagizwa kuhakikishwa kwamba linapambana na uhalifu pahali popote pale nchini, ili nchi yetu iendelee kuwa katika hali ya utulivu na amani na kupambana na wahalifu wote wale ambao wanaoharibu mali za watu na wanaharibu amani ya nchi yetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Salim Abdallah tunaupokea na hilo ndio lengo la serikali kwa Vikosi vyake vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha kwamba

uhalifu wa aina yoyote pahali popote pale na popote utakapokimbilia unatiwa mbaroni na kupelekwa katika mikondo ya sheria.

**Mhe. Mahmuod Mohammed Mussa:** Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri ambayo umeyatoa na kwa kuwa Chake Chake ni moja kati ya sehemu zilizomo ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar leo asubuhi tu nimesikia vyombo vya habari vikizungumzia suala zima linalohusiana na kadhia hii ya ulevi. Katika maeneo yale ya Ndagaa, kuna upatu sasa hivi unachezwa wa madumu ya ulevi watu wamekusanyika wanacheza upatu upande mmoja kila mtu anapokea kwa siku yake ambayo watakuwa wenyewe wamekubaliana na Jeshi la Polisi limeoneshwa na kushtushwa sana na suala hili. Je, serikali inalifahamu hili na kama serikali inalifahamu hili kuna mikakati iliyopangwa katika kukomesha vitendo vile ambavyo vinazalisha masuala ya uhalifu katika nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba pombe haramu ni marufuku nchini na wale wote watakaojishughulisha na vitendo hivyo vinavyohusiana na pombe haramu hatua za kisheria zitachukuliwa. Napenda nimshukuru sana Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kwa kututaarifu suala hilo la Ndagaa, nataka nimuhakikishie kwamba Jeshi letu la Polisi liko macho linafanya kazi zake na serikali itakuwa karibu zaidi na Jeshi la Polisi, kuhakikisha wale wote ambao wanashiriki au wanafanya vitendo vyovyote vya uhalifu ikiwemo pombe haramu na vitendo vyengine vyote vya uhalifu basi hatua zitachukuliwa na wale wote wahusika watapelekwa katika vyombo vya usalama.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nachukuwa nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kuwatetea wananchi wake wa Jimbo la Wawi kwa hali na mali ikiwa jua ikiwa mvua.

Mhe. Spika, lini serikali italeta msaada wenye nguvu na uhakika baada ya wananchi kuchoka na tabia hii ya pombe za kienyeji, madawa ya kulevya. Lini Serikali italeta msaada kupitia chombo chao hichi muhimu cha wananchi wa kupiga vita dawa za kulevya na pombe za kienyeji na Mhe. Saleh Nassor Juma eneo alilolitaja ni *specific* Mochwari, kwa nini pasiwekwe ulinzi wa muda wote huu na tokea kupeleka hao askari mara ngapi wameshakwenda kufanya kazi hii baada ya kishindo chako Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**

(a) Mhe. Spika, sheria iliyopo sasa imefanyiwa marekebisho makubwa na inakidhi kabisa haja ya kuwashughulikia wahalifu wote wakiwemo hawa wa madawa ya kulevya. La msingi hapa Mhe. Spika, ni mashirikiano kati ya serikali, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na wananchi. Kwa sababu tatizo kubwa ni pale wananchi wanapokataa kutoa ushahidi kwa watuhiwa wanaoshiriki katika madawa ya kulevya na sote tunajua kwamba madawa ya kulevya yanafanyika katika mitaa yetu, majirani zetu pengine wakati mwengine majumbani mwetu.

Kwa hivyo, jambo la msingi hapa ni wananchi kutoa taarifa na kuwa tayari kuwa mashahidi pale ambapo watuhumiwa wanatiwa mbaroni, Jeshi la Polisi na vyombo vyengine vya Ulinzi na Usalama vinafanya kazi kubwa katika kubambana na hali hii. Kwa hiyo, la msingi ni sote kwa pamoja kushirikiana kuyakataa maovu hayo ili kuhakikisha kwamba jambo hili halitokei milele.

Kuhusu eneo la Mochwari kama nilivyosema Jeshi la Polisi Mhe. Spika, limefanya msako na doria mara kwa mara na jambo hili ni endelevu tutaendelea kuwashughulikia pale na watakapokwenda pengine popote watashughulikiwa na wakatiwa mbaroni na wale wote wanaojishughulisha na vitendo hivyo vya uhalifu wakae wakijua kwamba iko siku watatiwa mbaroni na mkondo wa sheria utachukuwa nafasi yake.

Nawaomba sana wananchi wote wanapoona vitendo vyovyote vya kihalifu katika maeneo yao kutoa taarifa polisi au katika taasisi nyengine za serikali ili hatua ziweze kuchukuliwa.

## Nam. 80

## Kukosekana kwa Vitanda Vyuo vya Mafunzo

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: -** Aliuliza**:-**

Nampongeza Kamishana Mkuu wa Chuo cha Mafunzo kwa kuwa mbunifu katika shughuli zake za kikazi. Lakini bado wanafunzi wanaofika katika Vyuo vya Mafunzo wanalala kwenye magodoro chini.

(a) Je, Wizara inayohusika haioni kuwa kuna umuhimu wa kuwapatia vitanda kama Magereza mengine yalivyo.

(b) Je, ni lini Wizara itafanya maamuzi ya kuwapatia wanafunzi hao vitanda kama vile ilivyofanya katika kuwapatia sare wanazozivaa.

(c) Kwa vile wanafunzi hao wanasifa ya kulima, kujenga, kuchonga na hivyo wanao uwezo wa kuchonga vitanda. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia zana na vifaa kama vile mbao na kadhalika ili wachonge vitanda vyao wenyewe.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Muyuni swali lake Nam. 80 lenye kifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, naomba kupokea pongezi za dhati alizopewa Kamishna wa Chuo cha Mafunzo pamoja na wapiganaji wake wote na Mheshimiwa kwa kuthamini jitihada zinazochukuliwa na Chuo cha Mafunzo za kubuni mbinu mbali mbali katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara inaona upo umuhimu wa kuwapatia vitanda wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kama wanavyopatiwa vitanda wanafunzi wengine.

(b) Mhe. Spika, nia ya kuwapatia vitanda wanafunzi ipo. Nia hiyo itaelekezwa pale tu hali ya fedha itakaporuhusu kama walivyoweza kupatiwa sare wanazozivaa. Utekelezaji huu utaendana na hali ya vituo ilivyo. Baadhi ya vituo yaani vyumba vyake ni vidogo haviwezi kuingia vitanda ikilinganishwa na wingi wa wanafunzi na mahabusu. Hata hivyo, suala hilo litachukuliwa hatua zaidi kitakapojengwa Chuo kipya cha Hanyegwa mchana na majengo mengine ya Chuo Unguja na Pemba.

(c) Mhe. Spika, Serikali imeliona suala hilo la kuwapatia mbao na zana mbali mbali kwa ajili ya uchongaji na kazi nyengine za mafunzo ya amali kwani hilo ndio lengo mahsusi la kuitwa Chuo cha Mafunzo. Kadri hali ya fedha itakavyoruhusu utengenezaji wa vitanda utafanyika ili kuona haki za binaadamu zinatekelezwa ndani ya Chuo cha Mafunzo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, vile vile baada ya kumpongeza Kamishna na wewe nikupongeze sana Mhe. Waziri kwa kujibu swali hii la msingi kwa nguvu ya hoja, nikupongeze sana Mhe. Waziri.

Niendele tena kumshukuru Kamishna kwa mara ya tatu, ya nne na mara tano kwa kazi anayofanya kwa umakini wake wa hali ya juu. Swali langu kwa kuwa suala la kupatiwa vitanda ni sehemu ya utekelezaji wa haki za msingi za binaadamu na serikali imejitahidi sana katika Chuo cha Mafunzo tumeshuhudia sare kupatikana jambo la kupongeza, vyoo vizuri sasa hivi vipo pale baada ya kutumia vyoo vya mtondoo ni jambo la kupongeza sana kwa serikali imejitahidi vya kutosha.

(a) Ni lini hasa swali hili litakamilika na hivi sasa nilipopita vitanda vinaaza kuchongwa nimpongeze tena Kamishna mara nyengine na nyengine amekuwa akichukuwa jitihada kwa hali na mali, nikuombe tu Mhe. Waziri hii Bajeti yake muangalie kwa jicho la huruma msije kufika pahali mkaja mkamkatia tutamrudisha nyuma jitihada zake anazofanya, nikuombe hilo.

(b) Kwa kuwa mwanafunzi anapomaliza muda pale anatakiwa atoke na tabia njema. Je, wananufaika vipi baada ya kutoka kumaliza kifungu chao pale wanafunzi wanapokuwepo mitaani.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwanza na mimi naendelea kuzipokea pongezi za ziada kwa Kamishna na wapiganaji pamoja na Wizara kwa jumla. Ni lini serikali italishughulikia na italimaliza suala hili.

Kwanza hivi sasa serikali kupitia Chuo cha Mafunzo imeanza utaratibu wa kupasua mbao katika miti yao ambayo waliipanda katika mashamba yao kwa madhumuni ya kupata mbao na kuwapatia wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo ambao wanajishughulisha na useremala ili kuchonga vitanda kwa vile Vyuo ambavyo vinalingana na majengo ambayo yanaweza yakaingia vitanda. Kwa hivyo, ni lini hivi sasa hivi tumo katika mchakato huo wa kukata miti ambayo tumeipanda kwa madhumuni ya kupasua mbao na tutaendelea kupasua mbao ili kutengeneza vitanda.

Pili, wanafunzi ambao wanatoka Chuo cha Mafunzo tunawandaaje kama ulivyosema katika suala lako la msingi Mhe. Jaku Hashim kwamba miongoni mwa kazi za amali ambazo wanapewa katika Vyuo vya Mafunzo ni suala la Kilimo ni suala la Ufugaji, suala la Ujenzi na suala useremalla na fundi charahani. Kwa hiyo, tunawandaaje kwamba ni sisi kazi yetu kuwaandaa kuwapa elimu ya amali wanapokuwa katika Vyuo vya Mafunzo wanapotoka sasa ni jukumu lao kwenda kwenye Taasisi za Serikali ambazo zimewekwa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, ili wachukuwe mikopo na waweze kujiendeleza ili waweze kukimu maisha yao. Mhe. pia Mheshimiwa alisema suala la bajeti lakini kama Waheshimiwa Wawakilishi wanavyojua kwamba bajeti zetu zinatokana kana

kasma na vifungu ambavyo vimo ndani ya Chuo cha Mafunzo. Kwa hivyo kwa kile kifungu ambacho kipo kwa ajili ya kazi za amali kitafanyiwa kazi hizo. Kwa vile vifungu ambavyo havipo katika kazi za amali zitatumika kwa ajili ya kazi ambazo zimeoneshwa katika vifungu ambavyo Baraza hili la Wawakilishi huwa linavipisha na kuvifuatilia matumizi na utekelezaji wake.

Ahsante sana.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, ninakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nimejaribu kumsikiliza kwa makini sana.

Ni kweli Chuo cha Mafunzo kama anavyosema ni Chuo ambacho kinawafundisha hawa vijana wetu ili kuwapelekea kuondokana na yale matatizo ambayo yaliyowapeleka pale ili wanapotoka wawe wajasiriamali na mambo mbali mbali. Lakini mafunzo yapo ya aina nyingi; kuna mafunzo ya ujasiriamali na kuna mafunzo ya kitaaluma. Na kule kwa upande wa wenzetu wa Tanzania Bara tumekuwa tukishuhudia katika *graduation* mbali mbali kujitokeza baadhi ya wanafunzi au baadhi ya wafungwa ambao wana-*graduate* kutokana na taaluma wanazopata ndani ya Gereza.

Je, katika hili suala la kuwapatia elimu wanafunzi wa Zanzibar, wizara yake Mhe. Waziri imejipanga vipi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake kama ifuatavyo.

Ni kweli wafungwa ambao wamefungwa na wanaendelea kufungwa katika Magereza ya wenzetu huko Tanzania Bara mbali ya kazi za amali, wanajifunza pia taaluma nyengine ya Vyuo Vikuu. Na wanafanya hivyo kwa sababu haja hiyo ipo na wanafunzi wenyewe wapo tayari kufanya hivyo na sisi itakapotokea kwamba yupo mwanafunzi ambaye anataka kujiendeleza katika elimu ya juu, Chuo cha Mafunzo kitachukua taratibu za kumuwezesha mwanafunzi huyo aweze kujifunza kwa mujibu wa taratibu za Chuo cha Mafunzo.

Ahsante sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, ninakushukuru naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba wenzetu wa Magereza wamekuwa wakitoa mafunzo na kazi za ureselema na ninaamni kwamba kazi hii ya ureselema

wanaifanya kwa ufanisi mkubwa. Na kwa kuwa Serikali mfuko wa madawati ambao zaidi ya shilingi bilioni zinatumika kwa ajili ya madawati. Ni kwa nini sasa Serikali kupitia Wizara yake haijengi hoja ya kwamba badala ya kununua madawati nje ya Zanzibar, hatuwapelekei Magereza wakachonga madawati yale ili wakafanya kazi mbili sambamba; wakafanya kazi ya kutoa mafunzo na kazi ya kuongeza mtaji kwa Magereza.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kabla ya kujibu swali lake naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa kupita vyema kwenye mchakato ndani ya chama chake. (*Makofi*)

Serikali katika utengenezaji wa madawati ina utaratibu wa kufata sheria za manunuzi, nayo hufuata utaratibu wa kutangaza *tender* na wale wanaotaka kufanya kazi hizo huomba na mchakato hufanyika kwa ajili ya kufanya shughuli hizo.

Na sisi kama Chuo cha Mafunzo tutajipima tukiona kwamba tuna uwezo wa kuingia katika ushindani katika kuifanya kazi hiyo, basi pengine mwaka huu na sisi tutaanza kujaribu ili na sisi tuwe ni sehemu ya watu ambao wataingia katika utaratibu wa Kiserikali wa kuomba huo utaratibu wa kuchonga madawati.

**Na. 32**

**Tatizo la Kutozwa Kodi kwa Wafanyabiashara Wadogo**

**Mhe. Jaku Hashim** - Aliuliza:

Mhe. Spika, ahsante kabla ya kujibiwa swali langu ninataka kufanya marekebisho katika swali hili, ninafikiri makosa ya ofisi kidogo katika ku-*type* au vipi.

Pia niendelee tena kumpongeza Mhe. Waziri kuwa msikivu katika suala la utendaji wake jana baada ya kuchangia hapa, ametoa karatasi za wasafiri wanaondoka katika bandari yetu ya Zanzibar kutumia usafiri wa bahari kwenda nyengine ndani ya Zanzibar ninafikiri itakuwa shilingi elfu moja. Ni jambo la kupongeza, hapa ninafikiri inachokusudiwa ni shilingi mia tano lakini tutafika *inshaallah*.

Mhe. Spika, ahsante naomba sasa nipate majibu ya swali hili:

Serikali katika kipindi cha Awamu ya tano (5) ya Mhe. Kamandoo Dkt. Salmin Amour Juma, Seerikali iliondoa kodi ya *VAT* kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuwainua wawe wafanyabiashara wakubwa.

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nini isiondoe kodi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo hadi watakapofikia mitaji ya milioni 40.

b) Kwa kuwa sekta ya biashara ni nguzo kubwa ya uchumi wa Zanzibar kuwabana wafanyabiashara wadogo kodi kunasaidia kuwainua au kuwarudisha nyuma kimaendeleo yao.

c) Ni lini Serikali itakuwa na mfumo mmoja wa utoaji wa kodi badala ya kuwa na Taasisi nyingi zinazotoa kodi kama Baraza la Manispaa, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), Mamlaka ya Kodi ya Mapato (TZ) na Mabaraza ya Hal mashauri na Miji.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tufanye marekebisho hayo. Kwani ninadhani hayatakuwa yameingilia majibu ya msingi.

**Mhe. Waziri wa Fedha** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwanza na mimi ninataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa kuyaona hayo masahihisho lakini vile vile ninataka nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kuona usikivu wangu. Ninataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba nitakuwa msikivu kwa Baraza zima na kwa wakati wowote ule. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima kabla ya kujibu swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub lenye kifungu (a), (b) na (c) naomba kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo, ingawa mwenyewe ameshafanya masahihisho.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa ninapenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa kodi ya *VAT* imeanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa nia ya kukuza mapato kwa ajili ya mahitaji ya nchi na wananchi wetu. Kodi hii haikuwepo katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kikawaida kodi zinalipwa na mlaji yaani mwananchi na wafanyabiashara ni wakusanyaji tu wa kodi hizo na baadae hupaswa

kuziwasilisha Serikalini. Hata hivyo, ninapenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo hawatozwi kodi ya *VAT* yaani asilimia 18 ya mauzo bali hutozwa asilimia 3 ya ushuru wa *stamp*.

Kiwango hicho cha asilimia 3 kina lengo la kuwakuza na baadae kusajiliwa katika kodi ya *VAT*. Wazo la Mhe. Mwakilishi la kuitaka Serikali kuwasaidia na kuwakuza wafanyabiashara wadogo wadogo ni sahihi na ndiyo lengo la Serikali.

b) Mhe. Spika, Serikali haina nia ya kuwabana wala kuwarudisha nyuma wafanyabiashara wadogo wadogo. Nia ya Serikali ni kuwasaidia wakue kibiashara wafanyabiashara wadogo wadogo wamepewa fursa ya kulipa kodi hiyo ya asilimia 3 kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu, ili kuwapa nafasi kushughulikia zaidi biashara zao.

c) Mhe. Spika, wazo la Mhe. Mwakilishi la kuwa na mfumo mmoja wa ukusanyaji wa kodi ni jema sana na Serikali inalizingatia. Ninachoweza kumwambia Mhe. Mwakilishi kwa wakati huu ni kwamba kuwepo kwa taasisi nyingi zinazosimamia kodi hapa Zanzibar ni kwa sababu ya kupatikana kwa urahisi wa usimamizi wa kodi hizo, hasa tukizingatia kuwa kila taasisi zinakusanya kodi tofauti. Hata hivyo, ninapenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli suala hili linahitajia kuangaliwa kwa kina na ninalichukua kwa kulifanyia kazi kwa zile kodi ambazo zinaweza kukusanywa kwa pamoja na taaasisi moja.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, niendelee tena na tena kumshukuru Mhe. Waziri kwa umakini wake na jitihada zake anazozichukua kwa kuwajali wananchi.

1) Kwa kuwa Zanzibar biashara ni nguzo kubwa ya maendeleo ya nchi na wananchi wake kutokana na kuwa ni nchi ya visiwa. Kwa nini Serikali isiondoe kodi ya *VAT*, sababu imekuwa ni kilio kikubwa kwa wananchi kama alivyokiri Mhe. Waziri kuwa kodi hiyo inalipwa na wananchi ndiyo wanaoumia siyo wafanyabiashara wanaouza.

2) Serikali ya Awamu ya Tano ilichukua muda mrefu kutotumia sheria hiyo pamoja na Serikali ya Muungano kuwa imepitisha Bungeni. Je, Serikali ya Zanzibar iliangalia vipi athari zake katika kuimarisha sekta ya biashara kutokana na Zanzibar kuwa ni nchi ya visiwa na inahitaji unafuu. Bidhaa hizo kwa kivutio baada ya ndugu zetu Tanzania Bara kutaka sisi kwenda kununua kwao, tukaweka kivutio hicho wakatoka wao wakaja kununua hapa, unatoa kauli gani Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo.

1) Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kodi zote zinazotozwa mwananchi ndiye mlipaji wa kodi. Ninapenda kumuhakikishia Mhe. Jaku kwamba kuondoa *VAT* kwa sasa ni suala gumu lakini lengo letu ni kuishusha kwa awamu kwa awamu ili kutoa nafasi na kumsaidia mlaji.

2) Mhe. Spika, Mhe. Jaku ameniuliza kuhusu habari ya athari za kuwepo kwa *VAT*. Kodi zote zina athari kwa mwananchi wa kawaida lakini ninachopenda kumuhakikishia Mhe. Jaku na Waheshimiwa Wawakilishi wengine ni kwamba maendeleo yetu yanaletwa kutokana na kodi zetu, tukishindwa kulipa kodi maana yake tutakuwa ni tegemezi; tutegemea misaaada na misaada hii kila siku inapungua.

   Kwa hivyo mimi ninataka kumwambia tu kodi zote zina athari lakini athari yake ni ndogo kuliko maendeleo ambayo tunayoyapata; tunajenga mabarabara, skuli, tunapeleka maji kwa kutumia kodi zetu na hawa wanaotusaidia wanatusaidia kwa sababu wananchi wao wanalipa kodi.

   Hivyo ninataka nimwambie tu kwamba tuvumiliane tuendelee kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na wananchi wetu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza, kama alivyojibu Mhe. Waziri wangu msikivu maswali ya Mhe. Jaku.

1) Mhe. Spika, hivi sasa duniani watu wana misukumo ya kuangalia hasa katika hizi kodi ambazo zimekuwa zimepitwa na wakati. Je, Mhe. Waziri huoni ipo haja hivi sasa hii *VAT* na kutokana na muda ambao uliokuwa umeshapita. Huoni ipo haja hivi sasa ku-*change* sheria ikaweka vizuri zaidi.

2) Katika kitabu chako cha bajeti ukurasa wa 25, Mhe. Spika, kila siku kukikacha watu wanatengeneza majiko ambayo yaliyokuwa hayataleta athari. Sasa hivi imefanywa hesabu duniani ambayo majiko yanayotumia moshi ambayo huleta madhara ya *cancer* na mambo mengine. Lakini Mhe. Spika, hapa kuna jiko ambalo linatumia *spirit*. Je, Mhe. Waziri huoni ipo haja ya kuipunguzia na wao ili mwananchi wa chini akaweza kuitumia.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kujibu maswali mawili ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kama ifuatavyo.

1) Mhe. Spika, kodi ya *VAT* haijapitwa na wakati. Ni kodi thabiti ambayo nchi nyingi duniani wanayo na ni kodi ambayo mwananchi wa kawaida anaichangia na ni kodi ambayo mchango wake ni mkubwa sana katika maendeleo yetu.

   Hata ukiangalia makusanyo ya kodi zote zinazokusanywa na *ZRB*, *VAT* utaona mchango wake ni mkubwa sana na inatusaidia katika maendeleo yetu. Kwa hivyo kodi hii itakapokuwa imeshapitwa na wakati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakuwa na nafasi nzuri ya kusema sasa sheria tunabadilisha na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndiyo tuliopewa mamlaka ya kutunga sheria ya kubadilisha sheria. Wakati huo ikipitwa na wakati Baraza likisema sasa tubadilishe, Waziri wa Fedha atalipokea na kubadilisha lakini kwa wakati huu bado kodi hii haijapitwa na wakati kabisa.

2) Mhe. Spika, katika hotuba yangu nimeeleza na nimetoa nafasi ya kusamehe kodi kwa *spirit* ya aina *ethanol* ambayo itatumika kwa ajili ya majiko haya mapya ili lengo letu ni kuwafanya wananchi wetu wapunguze matumizi ya kuni na mkaa. Tunataka mazingira yetu yawe mazuri zaidi. Kwa hivyo katika upande huu tayari ukiisoma ile hotuba tumeshatoa msamaha wa kodi.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, ninashukuru sana kunipa fursa na mimi fursa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa *ZRB* inakusanya kodi mijini na mpaka vijijini. Na kwa kuwa Halmashauri pia nazo zinakusanya kodi kupitia maliasili zisizorejesheka kama mchanga, mawe na mambo mengineyo, viduka vidogo vidogo na Baraza la Mji huwa linakusanya kodi. Sasa je, Mhe. Waziri kwa kuwa Halmashauri hukusanya kodi zake kupitia viduka vidogo vidogo viliopo vijijini na kwa kuwa *ZRB* sasa hivi wanataka waende mpaka vijijini kukusanya kodi.

Je, huoni kama kwa kuwa *ZRB* ina mitaji mingi ya kukusanya kodi, kuwanyang'anya kodi za vijijini Halmshauri huoni kuwa itakuwa umepokonya mitaji yao ya kukusanya kodi. Kama hivyo ndiyo, je, haoni kama *ZRB* kwa kuwa ina mitaji mingi si bora kuwaachia Halmashauri vijijini wakakusanya kodi wao.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kabla ya kujibu swali la Mhe. Subeit Khamis Faki nimpongeze kwa ushindi wake mkubwa alioupata kule Micheweni kupitia Chama chake cha CUF. (*Makofi*)

Na ninawapongeza wale wengine wote walioshinda na walioshindwa na huo ndio mchakato wa uchaguzi. Kitu muhimu katika uchaguzi kama nilivyosema kwenye hotuba yangu Mhe. Spika, ukubali sauti za wananchi, ukishakukubali sauti za wananchi hugombani na mtu. Ninawapongezeni sana, saluti njema. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba nijibu swali la Mhe. Subeit kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ukiisoma sheria ambayo tumeipitisha hivi karibuni ya Tawala za Mikoa, sheria ile inatoa fursa kwa Tawala za Mikoa kupitia Halmashauri kukusanya kodi na imetoa fursa na imeelezea kodi za aina gani watakazokusanya wao.

Kama kuna kodi ambayo itakusanywa na *ZRB*, itakusanywa tu na *ZRB* kwa misingi ya kuwasaidia lakini baadae kuirudisha kule kule Halmashauri na hilo ndiyo lengo letu. Sisi tunataka Madaraka Mikoani kwa kila kitu mpaka katika suala zima la ukusanyaji wa kodi. *ZRB* haitoingilia kodi ndogo ndogo, kodi ndogo ndogo zote zitaachiwa kwa Halmashauri na kama kutakuwa kuna kodi ambayo unahisi wewe hii waachiwe Halmashauri basi njoo uniambie tutazungumza baina ya Halmashauri zetu na *ZRB* ili tuweze kuona kwamba ni kiasi gani tunaweza tukaiachia kodi hiyo Halmashauri. (*Makofi*)

**Nam. 2**

**Tatizo la Maji Chake-Chake**

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman** – Aliuliza:-

Tatizo la maji katika Mji wa Chake-Chake na Vitongoji vyake limekuwa la kudumu, ambapo wananchi wanahangaika kufuata maji mabondeni na masafa marefu. Naomba serikali ieleze ni lini tatizo hili litaondoka ili wananchi hao wapate huduma hiyo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 2 kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kupunguza tatizo kubwa la kukosekana kwa maji katika Mji wa Chake Chake na Vitongoji vyake.

Mhe. Spika, mpaka hivi sasa maji yanapatikana vizuri bila ya mgao. Linaonekana sasa hivi ni uvujaji wa maji katika mitaa mingi kutokana na *pressure* kubwa ya maji, inayotokana na majaribio ya mradi mpya wa maji uliotekelezwa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).*

Mhe. Spika, napenda kukuhakikishia kwamba msururu wa wananchi wa Chake Chake wanaoelekea mabondeni kutafuta huduma ya maji imepungua sana.

Napenda kukiri tu kuwa Chake Chake kuna malalamiko ya baadhi ya wananchi wanaotaka kuunga maji katika mabomba mapya ili wapate maji yenye *pressure* ya kutosha, suala hili halina pingamizi yoyote. Kinachotakiwa ni kufika Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba ili kupewa utaratibu wa kuunga maji.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Waziri Je, wizara yako ina mpango gani wa kuvitunza vyanzo vya maji ambavyo kwa sasa vingi vimeathirika kutokana na uchafuzi wa mazingira.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, azma yetu ni kuona kwamba vyanzo vinavyotoa maji kwa ajili ya wananchi vidumu na viendelee kuwepo. Kwanza sisi watu wa maji tunapenda kumuomba Mwenyezi Mungu atuletee mvua za salama ili ardhini kuwe na maji ya kutosha.

Pili, kwa sababu kuna uvamizi katika vyanzo vya maji, hatua ninayoichukua sasa hivi ni kuweka uzio katika kila penye chanzo cha maji ili watu wasiweze kufika katika lile eneo linalopatikana maji, kwa madhumuni ya kuwa maeneo yale yasiharibike na yaendelee kubakia.

Vile vile tunawaomba wananchi kwamba wasikilize sana Idara ya Mazingira inapozungumzia juu ya suala la uharibifu wa mazingira, kwa sababu athari zake zitakuwa kubwa kwa wananchi wote baadaye.

**Mhe. Raya Suleiman Hamadi:** Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa mjibu mazuri na pia kwa kufuatilia kazi zake za miundombinu. Mimi nataka nimuulize tu Mhe. Waziri. Mhe. Waziri mimi nakaa katika kijiji cha Ole Mchangamrima, natumia bomba au natumia kisima kilioko kwa Mwanamwari. Tuna miezi kama sita hatupati maji, kuanzia mbuzini hadi kijiji hicho, nataka nijuwe kuna tatizo gani.

Halafu nijuwe kuna mipango gani ya kwamba anayepata maji na aliyekuwa hapati pia anatoleshwa kodi. Kwa hivyo, tupate majibu ili tujuwe wananchi. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza nampa pole sana Mheshimiwa Mwakilishi, kwamba kwa miezi sita bado hawajaweza kupata maji katika maeneo yao. Suala hili inabidi nilifuatilie ili kujua hasa tatizo, kuna nini, kwa ghafla siwezi kumjibu hapa. Katika suala la kuchangia maji, suala hili Mhe. Spika, kwa kweli tumeliweka katika utaratibu wa kwamba anayepata maji ndie alipe kodi na asiyepata maji asilipe kodi. Lakini sasa kuna ugumu wa kuthibitisha kama kweli mtu hapati maji, hili tatizo lipo na tunaendelea kulifanyia kazi kuona kwamba wale wanaojaribu kudanganya kwamba maji hawapati kumbe wanapata kuwafuatilia kwa karibu zaidi.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa jitihada yake, lakini pia napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa tatizo la maji limo kila pembe katika nchi yetu, na kwa kuwa serikali inajitahidi kutatua lakini bado matatizo yapo. Kwa kuwa Jimbo langu la Micheweni mabomba yake ni mabomba makongwe sana, ni ya tangu mwaka 1972 wakati wa Mchina, mabomba yale tayari yameshaziba na kufanya kutu. Kwa kuwa yanasababisha maeneo ya Jimbo la Micheweni kukosa maji, na maji yakifika yanafika wakati wa usiku tu na tena siku nyengine yanakuwa na foleni.

Kwa mfano, Mjini Wingwi na Micheweni Chamboni maji huwa hayafiki. Sasa je, kwanza namuuliza Mhe. Waziri ni lini watafanya shauri la kuona kama mabomba yale sasa yameshapitwa na wakati na yanahitaji kupata msaada wa kuweka mabomba mengine. Je, kwa kuwa Jimbo la Mhe. Jaku Hashim la Muyuni kuna baadhi wana matatizo ya maji kama Muyuni, Muungoni, Kitogani na sehemu nyengine hawapati maji kama Michamvi. Je, ni lini tatizo hili Mhe. Waziri atasimamia ili limalizike.

**Mhe. Spika:** Swali la msingi lilikuwa ni tatizo la maji katika Mji wa Chake Chake, lakini Mhe. Waziri kama ana majibu ya karibu anaweza akasaidia. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, tangu nanyanyuka pale kuja hapa ningeshangaa sana kama Mhe. Subeit Khamis Faki asingeliuliza swali la Micheweni, kwa sababu ameshanikabili kwenye suala hili na kunieleza tatizo la mabomba machakavu ya maji yalioko Micheweni, tangu yalipopelekwa na Marehemu mzee wetu Mzee Abeid Aman Karume.
Mhe. Spika, tunachotakiwa kufanya ni kuanzisha mradi mpya kwa ajili ya Micheweni, kwa ajili ya kubadilisha mabomba yale. Kwa hivyo, siwezi kumuambia ni lini itakuwa tayari, lakini sasa hivi watu wangu wanafanya

mchakato wa kuona kwamba kupata mradi mpya wa kubadilisha mabomba yale ya zamani kwa Micheweni, ili tulete mabomba ya kisasa, tuondokane na yale mabomba ya *asbestos* ambayo nayo pia duniani yana matatizo yake kwa ajili ya kutumika.

Mhe. Spika, vile vile aliuliza kuhusu Jimbo la Mhe. Jaku Hashim, ambaye na yeye mwenyewe alikuwa anataka kuuliza na pia nilitegemea atauliza maswali ya eneo lake hili, kwa sababu nalijua kwamba lina matatizo ya maji. Kwa hivyo nasema kwamba lakini Michamvi haimo katika Jimbo la Mhe. Jaku Hashim, kwa Michamvi Mhe. Spika, ni kwamba kule ukichimba kisima basi unapata maji ya chumvi. Kwa hivyo, kule tumepeleka mradi wa *desalination*, ambapo usaidie kupata maji angalau ya kunywa kwa wale wananchi. Wakati huo tunatafuta mradi mpya kwa ajili ya kuweza kupeleka maji mpaka kule mwisho Michamvi. Hivi sasa mradi ule wa *desalination* unaendelea kufanyiwa kazi na tayari kule wataalamu wako wanatengeneza ili kuweza kupatikana maji, kama tulivyofanya katika kisiwa cha Uzi, hasa kule Ng'ambwa ambapo kuna tatizo kama hilo vile vile.

Kuhusu masuala ya Muyuni na kwengineko mule munamo mabomba ya Mhe. Jaku Hashim, nako kuna matatizo vile vile ya mabomba kupasuka. Tatizo hili lipo, ni machakavu sana na yanakuwa yanapasuka mara nyingi kwa sababu ni mabovu. Kwa hivyo, nako pia tuna kazi kubwa katika wizara yetu ya kuhakikisha kwamba tunafanya mabadiliko ya mabomba katika maeneo mengi, hivi sasa wananchi wengi wanategemea sana maji haya ya bomba na wameacha kabisa visima vya zamani.

**Nam. 77**

**Kilio cha Kuwepo Kwa Daktari wa Mifugo Jimbo la Muyuni**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Muyuni wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha Daktari wa Mifugo mpaka kufikia kulalamika kwenye vyombo vya habari siku ya Jumanne tarehe 14/4/2015 ili wapatiwe Daktari huyo wa Mifugo kutokana na usumbufu mkubwa kufuatilia Makunduchi.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Kituo katika Jimbo la Muyuni na kuepo Daktari katika Jimbo hilo.

(b) Serikali kutojenga Kituo katika Jimbo hilo. Je, haioni kuwa inarudisha nyuma maendeleo ya wananchi wa Jimbo hilo na kuwapa usumbufu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba dakika moja ili nimpongeze sana waziri wangu kwa ushindi mkubwa alioupata katika Jimbo la Magogoni.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga kituo kipya cha huduma za mifugo Muyuni kutoka na ukosefu wa fedha.

Mhe. Spika, hata hivyo uwezo wa kifedha utakaporuhusu wizara yangu bado inayo nia ya kuongeza vituo vipya vya mifugo Unguja na Pemba, ikiwa ni pamoja na nyumba za wafanyakazi katika maeneo ya vituo hivyo ili wafugaji waweze kupata huduma kwa karibu zaidi.

Mhe. Spika, aidha madaktari ambao wanatoa huduma katika Mkoa wa Kusini Unguja wakati wote huwa tayari kwenda kutoa huduma hiyo popote inapohitajika.

Mhe.Spika, wizara yangu inawapongeza wafugaji wote wa Unguja na Pemba kwa jitihada wanazozichukuwa katika kujiendeleza kiufugaji, kwani hii ni ajira na huchangia kuongeza kipato na lishe bora kwa kufuata ushauri wa wataalamu, ili wajitoe katika dimbwi la umasikini. Mhe. Spika, ufugaji bora unafaida kubwa na wa haraka iwapo mfugaji atafuata masharti ya ufugaji bora.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri siwezi kusema mazuri wala mabaya yako kati na kati. Je, kama mwakilishi atatafuta nyumba au atajitolea kwa Jimbo la Muyuni, mko tayari kupeleka daktari pale.

Pili, wananchi wamekuwa wakihangaika anayetoka Michamvi, Paje, anayetoka Kitogani kumfuata daktari Makunduchi kwa baskeli, na wakati mwengine wa mvua na anapokwenda wakati mwengine hata hamkuti daktari. Je, utakuwa uko tayari kuletewa ushahidi huu na utachukua hatua gani kwa watendaji wako, wanaporipotiwa pale na hawafiki kwa wakati na mifugo kuendelea kufa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, wizara yangu haina pingamizi yeyote kama watapatiwa nyumba au kituo cha pale ili kupeleka madaktari katika sehemu ile. Kwa sababu hiyo basi nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Mussa Ali Hassan kwa jitihada zake kubwa na yeye kutupa kiwanja na tayari tumeshajenga pale na karibu jengo lile litamalizika.

Hata hivyo, wale madaktari wa Kusini ambao tunao Muyuni C na Mungoni, wakiwa bado wanasua sua naomba taarifa tuletewe, ili tuweze kuwachukulia hatua za kinidhamu. Hata hivyo, niwashauri Waheshimiwa Wawakilishi kama wanao vijana ambao wanasomesheka katika maeneo yao basi watuletee ili tuwafundishe masomo mafupi ya kuwasaidia wafugaji katika sehemu hizo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza, kutokana na Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake mazuri sana aliyotujibu.

Kwanza Mhe. Naibu Waziri nikupongeze kwa jinsi ulivyotueleza kuwa tayari uko katika maandalizi ya kutujengea vituo vya madaktari ili kuweza kutibiwa wanyama wetu. Lakini Mhe. Spika, kutokana na hali kama tunavyojua bajeti yako bado ni finyu sana, kutokana na hali ya kuwa wepesi wa kuweza kujenga vibanda hivyo. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni iko haja hivi sasa ukatoa ofa kuwa wawe *any time* unatembea katika zone kwa wale wenye mifugo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, suala la kupeleka madaktari, madaktari wapo sasa wanatembea, na tutatoa namba za simu ziwe wazi ili wasaidiwe wafugaji wetu na wapate huduma bora zaidi. Lakini hili suala la bajeti finyu, bajeti finyu haiendani na udaktari, bajeti finyu katika maendeleo yetu. Lakini vile vile madaktari wapo wakati wowote na ukitaka hata wewe tutakupa.

**Mhe. Asha Abdu Haji:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Kwa kuwa Wilaya ya Kusini Unguja kulikuwa na kituo cha matibabu ya wanyama, namuuliza Mhe. Naibu Waziri. Je, kituo kile bado kipo na kinafanyakazi? Ikiwa hakipo ni sababu gani ya kuondolewa kwa kituo kile? Na ikiwa kipo ni wafanyakazi wangapi wanafanyakazi katika kituo kile?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, swali sikulipata vizuri, kwa sababu sikujua ni kituo kipo pahala gani anachosema yeye.

**Mhe. Asha Abdu Haji:** Kituo kilikuwa Makunduchi Uwandani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, kituo cha Makunduchi kipo na kina wafanyakazi wanne. Wawili wa uzalishaji wa mifugo na wawili ni watibabu wa mifugo pale, na kinaendelea kufanyakazi na tunaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wote wa Kusini Unguja.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya

**Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016**
na
**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na majadiliano na kwa nafasi ya kwanza leo naomba nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma na baada ya hapo Mhe. Hija Hassan Hija.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa hekima, ambaye katujaalia kuwepo hapa leo tukiwa wazima wa afya. Vile vile kuweza kutupa uwezo wa kutimiza majukumu yetu.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia katika hotuba hizi mbili, moja ikiwa ya Mhe. Waziri wa Fedha na nyengine ni ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Niseme tu kwamba nampongeza Rais wa Zanzibar hasa kwa umakini wake mkubwa wa kuweza kuliongoza taifa letu. Vile vile ni kwa kuweza kupanga na kusimamia vyema mipango mbali mbali na utekelezaji wa sekta zote za kiuchumi, kijamii pamoja na kisiasa.

Pia, nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Spika, hasa kwa kutuongoza katika mfumo wa serikali hii tuliyonayo ya Umoja wa Kitaifa katika hali ya utulivu na amani. Mhe. Spika, mimi niipongeze pia serikali kwa mpango mpya wa kibajeti ambao wametuletea na mpango huu Mhe. Spika, unaleta matumaini mapya hasa kwa kuwa sisi kama wawakilishi pamoja na wananchi tutaweza kuona uwazi pamoja na uwajibikaji wa serikali katika mambo mbali mbali.

Sasa Mhe. Spika, niungane na wenzangu vile vile kuipongeza serikali katika utekelezaji wa mambo kadhaa ya mwaka 2014/15.

Mhe. Spika, maendeleo ya nchi yoyote yanatakiwa yalenge makundi yote yakiwemo makundi ya wanawake yakiwemo makundi ya watoto, vijana pamoja na walemavu na wengine. Mhe. Spika, niseme tu kwamba nimefarajika sana kuona kwamba serikali imeweza kulifikiria kundi la wanawake hasa kwa kutengeneza barabara mbali mbali zinazoingia vijijini ili kuhakikisha kwamba akina mama ambao tunajua kwamba ni karibu asilimia 70 ya wakulima ni akina mama. Kwa hivyo, serikali imeona umuhimu wa kufanya matengenezo makubwa katika

barabara mbali mbali zinazoingia vijijini na hili kwa kweli limeleta unafuu mkubwa kwa upande wa kina mama.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba kina mama ni watumiaji wakubwa wa ardhi na basi kwa upande wao hatua mbali mbali zilizochukuliwa kwa upande wa ardhi hususan suala la kusajili ardhi, litawapa nafuu kubwa akina mama hasa katika kumiliki maeneo ya ardhi ambayo wanaishi lakini vile vile wanayatumia.

Mhe. Spika, napenda kuipongeza serikali hasa kwa kuweza kusaidia katika masuala ya kilimo na kuweza basi kuhakikisha uwepo wa chakula pamoja na lishe bora. Hii Mhe. Spika, itasaidia sana hasa katika afya za kina mama wajawazito pamoja na watoto.

Changamoto kubwa inayojitokeza katika kupunguza vifo vya akina mama watawazito pamoja na watoto chini ya miaka mitano Mhe. Spika, ni kuwa lishe bora. Hivyo, basi ningependa kuipongeza sana serikali kwa kweli kwa hatua iliyofikia kuhakikisha sasa kwa upande wa lishe bora kwa akina mama pamoja na watoto kwa kweli hilo tumeweza kufanikiwa. Hatua za kuelimisha jamii lakini pamoja vile vile na kuhakikisha wataalamu ambao wanatoa elimu basi wanapatika kwa wingi, niipongeze sana serikali.

Mhe. Spika, katika suala la biashara hasa biashara ndogo ndogo Mhe. Spika, serikali imechukuwa hatua ya kuhakikisha kwamba itasajili biashara zote ndogo ndogo, ili sasa biashara zile zijulikane rasmi. Mhe. Spika, naweza kusema kwamba hili nalo ni moja katika jambo ambalo litawapa kina mama faida kubwa, kwa sababu tunajua wengi wanaofanya biashara ndogo ndogo hususan akina mama pamoja na vijana wengi wao kwa kweli walikuwa hawatambulikani. Hatua ya kuhakikisha kwamba kuna mradi maalum wa kuwatambua hawa itakuwa ni hatua nzuri na hatua hii itawasaidia katika mambo mbali mbali hususan ya kupata mkopo.

Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa kuanzisha mradi wa kutengeneza taa kwa kutumia jua. Mhe. Spika, mradi huu ulilengwa kwa ajili ya kina mama na mradi huu kwa kweli sasa hivi umeanza kuleta matumaini mengi hasa kwa akina mama walio vijijini. Sasa mimi niseme tu kwamba kwa kweli mradi huu utaweza kusaidia kina mama hasa walioko ndani ya maeneo ambayo umeme haupatikani, lakini vile vile kutapunguza matumizi ya umeme kwa wale watu ambao hawana uwezo wa kulipia umeme huu tunaotumia.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la wajasiri amali ambao hasa kwa wafanyabiashara wanyonge. Kwa hiyo, Mhe. Spika, na mimi nizidi kuiomba

serikali kwamba watu hawa bado wanahitaji elimu ya ujasiri amali wapewe ili waweze sasa kuendesha shughuli zao za uzalishaji.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi nyengine vile vile kuipongeza serikali hasa nimpongeze Rais wa Zanzibar kwa kutoa ada zote za Elimu ya Msingi, lakini vile vile kwa kutoa ada za mitihani kwa Elimu za Sekondari. Mhe. Spika, hii ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwa wananchi na kama nilivyosema mwanzo serikali yoyote inapojipanga inaangalia upande wa kiuchumi upande wa kijamii na upande wa kisiasa. Lakini Mhe. Spika, jana wakati Profesa Ali Mzee alipochangia hii ndio ilikuwa azma ya Mapinduzi ni moja katika azma ya Mapinduzi ya Zanzibar na hili kwa muda mrefu lilikuwa linasuwasuwa kidogo.

Lakini nimpongeze sana tena nampongeza Rais wa Zanzibar kwa niaba ya wazazi wote suala hili lilikuwa ni kero lakini lilikuwa zito, lakini Mhe. Rais ameweza kuwakonga moyo wananchi wake. Niseme tu na niombe sana wizara na niombe wale ambao wanashughulikia masuala haya basi suala hili liweze kutekelezeka kama alivyoangiza Mhe. Rais.

Mhe. Spika, vile vile nichukuwe fursa hii kuipongeza serikali kwa kuanzisha mradi wa chakula, moja katika tatizo ambalo hasa katika maeneo yaliokithiri kwa umasikini maeneo ya Kaskazini kulikuwa na tatizo kubwa sana la watoto kukimbia maskuli. Lakini niipongeze sana serikali pamoja na Wizara ya Elimu kwa kuchukuwa juhudi ya makusudi kuhakikisha kwamba katika maeneo hayo watoto wanapata angalau mlo mmoja wakipo skuli, ili wahakikishwe watoto wale wabakie skuli na wao wapate elimu kama watoto wenziwao, hii ni faraja kubwa sana kwetu.

Mhe. Spika kamati yangu ilikuwa kila siku inalia kilio hiKi kwa sababu ukienda katika maeneo hayo unaona namna watoto ambavyo kwanza afya zao sio bora, lakini wengi wanatoroka skuli kwa sababu ya kwenda kufanya biashara na hii vile vile itasaidia katika kuwatoa watoto kwenye biashara mbaya.

Mhe. Spika, jengine niseme niipongeze sana Wizara ya Afya naipongeza serikali lakini Wizara ya Afya vile vile niipongeze kwa juhudi zao mbali mbali ambazo wamezifanya katika kuhakikisha kwamba tunapata jamii yenye afya bora. Tunajua kuna changamoto nyingi na nyengene zinatushinda kutokana na uwezo wetu wa kifedha lakini hata hivyo tumeona maanake mambo mengine sio ya kuambiwa, lakini tunaona namna serikali hii ilivyojipanga kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ya afya bora.

Mhe. Spika, suala la udhibiti wa Malaria limefanyiwa kazi kubwa sana na leo tunasema kwamba Zanzibar Malaria hayapo hata kama yapo ni machache sana sote

sisi tunajua tulikuwa hata mimi mwenyewe nilikuwa sikai hata muda wa kipindi cha mwezi miezi miwili Malaria napata, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu.

Jengine ni mipango ya kuhakikisha kwamba maambukizi ya Ukimwi yanapungua hatuwezi kuyaondoa kabisa lakini yanapungua. Lakini niseme kwamba pia suala la Elimu ya lishe kwa mama na mtoto kuongeza vituo vya afya mbali mbali katika vijiji, vituo vya afya vinapatikana kila baada ya kilomita tano (5) pamoja na kuwa na wahudumu ndani ya vituo vile pamoja na kusomesha vijana kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali za afya. Lakini tuna mradi wa damu salama ambao kwa kweli unasaidia sana katika kuhakikisha kwamba mgonjwa yoyote anaefika pale akiwa na matatizo ya upungufu wa damu anapata matibabu.

Kuna suala zima la Elimu ya Uzazi wa Mpango; Nasema haya Mhe. Spika, kwasababu haya yote ndiyo ambayo yanapunguza vifo vya akina mama na watoto, kwa kipindi kirefu kina mama walikuwa wakienda hospitali wanawasi wasi na sisi pia tuna imani kwamba kuzaa mguu moja kaburini mmoja uko duniani ambayo katika dunia  nyengine haipo hiyo. Kwa sababu katika dunia ya wenzetu watakwenda wazazi elfu moja pengine asifariki hata mmoja. Kwa hiyo, hatua serikali imechukuwa ni ngumu, mambo ni mengi sana lakini bado serikali imeweza kupunguza vifo vya watoto pamoja na wazazi naipongeza sana serikali.

Lakini jengine ni kwamba Rais ameelekeza kwa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba basi kina mama hawa wapate wanapokwenda hospitali kwa ajili ya kujifungua wapate huduma hiyo bure. Nimpongeze sana Rais wa serikali yetu na nampongeza kwa sababu yeye anafahamu uzito wa jambo hili yeye ni daktari kwa hiyo uzito wa jambo hili analifahamu. Lakini anaijua jamii yake uwezo wake kama kiongozi lakini anajua thamani ya mtoto na anajua thamani ya mwanamke anaona hasa sio vizuri mwanamke anapokwenda kujifungua mtoto analeta roho nyengine yeye anaondoka duniani. Kwa hiyo hilo ni suala ambalo kwa kweli tumpongeze sana Mhe. Rais kwa kuwa na busara ya kufanya maamuzi haya.

Mhe. Spika, ningeomba sana Wizara ya Afya kulisimamia hili bado lina changamoto, bado halitiliwi maanani na watendaji kwa makusudi. Lakini ningeiomba Wizara ya Fedha vile vile kwamba kwa kuwa hili tumefanya maamuzi ya kuhakikisha kwamba kina mama wazae salama basi uingizwaji wa fedha katika wizara hii uwe bora zaidi kuliko katika vitengo vyengine.

Mhe. Spika, niingie katika muelekeo wa Bajeti ya 2015/16 kwanza niipongeze sana Wizara ya Fedha pamoja na mipango kwa kweli Bajeti ya mwaka 2015/16 imetoa kipaumbele na kipaumbele chake kikubwa ni kihakikisha kwamba jamii ya Wazanzibari wananufaika  kiuchumi, kijamii katika maendeleo mbali mbali. Mimi niipongeze sana serikali kwa kuanza kufikiria kufanya tafiti mbali mbali ikiwemo

kufanya utafiti wa ukusanyaji wa mapato. Hili ni jambo muafaka ni zuri lakini niiombe serikali kwa sababu hichi ni kipindi cha miaka 5 sasa tunamaliza tunaingia katika miaka 5 mingine lakini niiombe serikali kwamba masuala ya ukusanyaji wa mapato ni masuala ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo, kwa sababu maendeleo hayamngoji mtu. Kwa hiyo, ningeomba sana hili Mhe. Spika, kama wizara ilifanyie kazi.

Suala la Elumu bora kama ilivyoainishwa katika Hotuba ya Mhe. Omar Yussuf ni suala muhimu sana, tunahitaji wataalamu wengi katika nyanja mbali mbali hasa kufikia katika kiwango cha kimataifa na sababu tunazijua tunataka wataalamu wa kufanya ndani ya nchi yetu, lakini hata nje kwenda nje kufanya kazi kwa ajili ya kuleta tija katika nchi yetu hilo ni muhimu sana, tunauelewa ubora wa elimu ambao kwa kweli hatujafikia kiwango cha kuwa na elumu bora ya kuweza kushinda na nchi nyengine.

Ningeomba sana serikali kuhakikisha kwamba Bajeti hii ambayo tutaipitisha basi tuhakikishe Wizara kama ya Elimu kwa kweli ipewe nafasi kubwa katika kihakikisha kwamba wanapata vile bajeti ambazo wamezipanga. Lakini vile vile niombe pia serikali suala la kubadilisha sheria ambazo zinakwaza katika ukusanyaji wa mapato.

Hapa Mhe. Waziri ameligusia hilo lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri kwamba muda wa kusema kwamba huyu tumuonee huruma na huyu tumuonee huruma, umekwisha Zanzibar inataka maendeleo, watu wanataka maendeleo kwa hiyo tutafute mbinu ya kuhakikisha kwamba tunachoingiza tutaweza kutusaidia katika shughuli zetu za kuleta maendeleo katika taifa letu. Suala la misamaha ya kodi ni suala ambalo linaweza kufanyiwa kazi na ifike pahala sasa tuseme kwamba hii misamaha iondoke kwa hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, nataka kumalizia katika ukurasa wa 25 wa Bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha amezungumzia suala la majiko ambayo yanatumia *ethanol* ambayo Mheshimiwa hapa amelizungumzia. Mhe. Spika, ninaliona hili umuhimu wake hasa katika kuhifadhi mazingira yetu kwa sababu wananchi wengi wanatumia kuni bado kutokana na ughali wa vitu vyengine ambavyo vitumika katika kupikia. Lakini sasa niseme tu kwamba nikiangalia kwa bei ya mafuta haya yaliopo na kwa kupunguzwa tu ushuru ambao utatolewa, kwa kweli bado naona bei yake haitopishana sana na bei ya mafuta ya taa ambayo tunatumia.

Ningeomba sana baada ya kusema inapunguziwa ushuru wa jambo moja basi ipunguziwe ushuru wa vitu vyote ili kuhakikisha kwamba tunahifadhi mazingira yetu, na wananchi watakuwa na uwezo na wananchi watakuwa na uwezo wa kutumia mafuta haya kwa ajili ya kupikia.

Ningeomba ifanye utafiti wa kina kabisa kuona tafauti yake, tafauti ya kutumia mafuta haya kwa bei hiyo ambayo Mheshimiwa anafikiria kwamba akipunguza ushuru wa kodi ya Bandari peke yake unaweza ukasaidia lakini tutizame na bei ya mafuta ya taa ilivyo. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri hili ulifikirie na uone vipi tutaweza kuwasaidia wananchi kama tunavyokusudia. Mwisho kabisa Mhe. Spika, nataka kurudisha tena pongezi zangu kwa Mhe. Rais.

Nimeona ni nafasi nzuri hii ya kumpongeza Mhe. Rais kwa sababu kwanza katika haya tunayoyazungumza yapo katika ofisi yake. Lakini vile vile kwa sababu sasa hivi ni lala salama, kwa hiyo naona ni nafasi nzuri ya kumpongeza Mhe. Rais. Nampongeza Mhe. Rais kwa kuwa na imani kubwa ya akina mama. Nampongeza Mhe. Rais kwa kuona kwamba akina mama wana uwezo. Nampongeza Mhe. Rais kwa sababu tulianza na idadi ndogo ya mawaziri wanawake, ametuongezea idadi ya mawaziri wanawake sasa hivi, nampongeza sana Mhe. Rais.

Nampongeza kwa sababu tulikuwa hatuna Mkuu wa Mkoa Mwanamke, Mheshimiwa sasa hivi tunajinasibu akina mama, tuna Mkuu wa Mkoa Mwanamke. Lakini tumeongezewa na mwanamke mwengine mmoja kuwa Mkuu wa Wilaya lakini tumepata na Makatibu Wakuu wawili sasa hivi, Wakuu wa Wilaya. Lakini tumepata Makatibu Wakuu, tumepata na Wakurugenzi mbali mbali akina mama. Nampongeza sana Mhe. Rais, kwa kuona kwamba kweli akina mama wana uwezo.

Tunaizungumzia asilimia 51 ya wanawake waliopo hapa Zanzibar. Lakini pia tunazungumzia wanawake ambao wanashika nyadhifa mbali mbali katika nchi yetu. Wanawake hao wameonesha ujasiri mkubwa wa kuwa na uwezo wa kufanya kazi mbali mbali. Tunauomba sana Mhe. Rais na naomba katika dua zangu zote Mhe. Dkt. Ali Muhammed Shein arudi tena 2015, aweze kutuongoza na aweze kuleta uwiyano wa kijinsia ndani ya jamii yetu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nitoe mchango wangu wa hotuba hizi mbili za Mheshimiwa Waziri na zaidi niende kwenye hotua ya mipango.

Mhe. Spika, bila ya mipango hakuna matumizi, kwa hivyo mimi mchango wangu huu kwa kiasi kikubwa kwa asilimia 80 nitajikita zaidi kwenye hotuba ya mipango ili kuonesha kwamba mipango yetu ndiyo ambayo ingetusaidia kujenga hoja, kupata mapato na hatimaye kuleta maendeleo ya Wazanzibari.
Mhe. Spika, mipango na maendeleo Mhe. Waziri kumeelezwa mambo mbali mbali zikiwemo changamoto ambazo zinasababisha kufikia miradi ya maendeleo kama

ilivyopangwa. Changamoto ya kwanza ambayo Mhe. Waziri ameeleza ni sakata la ESCROW ambalo lilisababisha kupungua kwa GBS misaada ya kibajeti ambayo Zanzibar haikufika.

Mhe. Spika, hoja ya pili ya Mhe. Waziri ni kushuka kwa thamani ya shilingi ya Dola ya Kimarekani. Sasa ningetegemea Mhe. Waziri juu ya mpango huu angetuelekezea kwa kina, nini hatua ya ufumbuzi wa sakata hizi mbili ambazo amekiri kwamba zimesababisha kutokufikia malengo ya miradi ya maendeleo. Sakata ya ESCROW tumeambiwa kwamba hatua zimechukuliwa na tayari wahisani wanaendelea kuleta misaada. Lakini mmong'onyoko wa shilingi yetu Mhe. Waziri hakutueleza kwa kina hasa zipi hatua za BOT na serikali kwa ujumla ili kulinda shilingi ya Tanzania ili isiendelee kuathiri miradi ya maendeleo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, wakati shilingi inashuka wasimamizi wa BOT wakati ESCROW imesababisha kupunguza GBS, jana nimesikia kwenye vyombo vya habari kwamba watendaji wanane wa BOT wamekamatwa wameghushi vyeti vya *form four* na hao wapo sehemu za mahesabu, (*account section*), kumbe inasababisha kwamba ikiwa mtu ameghushi elimu na ndiyo huyo huyo yupo kwenye kitengo cha mahesabu ya BOT, kwa nini GBS ije wakati mtendaji husika ambaye angepaswa kusimamia fedha kumbe elimu yake imeghushiwa. Lakini unapokwenda upande mwengine kwamba hoja ya BOT unapodai kwamba kwa nini Wazanzibari hawaajiriwi. Wanatwambia kwamba vigezo vya Wazanzibari ni vichache, uwezo wao wa kielimu ni mdogo, lakini kumbe wao wanaajiri watu wakiwa wameghushi vyeti hata vya *form four*.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri labda hili atwambie nini hatua ambazo zitachukuliwa. Mimi imenipa picha sasa kumbe ile hoja ya kwamba Wazanzibari hawaajiriwi BoT kwa sababu ya uchache wa elimu yao, ushahidi wa jana umenihakikishia kwamba sio sahihi. Bado kuna tatizo la mchango rasilimali watu kwa upande wa ajira za BoT na lazima serkali itupe majibu ni kwa nini Wazanzibari hatufaidiki ili tukawa na nchango mkubwa kwenye suala hili.

Mhe. Spika, suala la pili ambalo hotuba ya Mipango imeeleza ni suala la ukuaji wa uchumi. Mhe. Waziri ameeleza kwamba ukuaji wa uchumi kwa upande wa dunia kwamba umezidi kukua kwa asilimia 3.4. Nchi zinazoendelea ukuaji umetoka asilimia 1.4 hadi 1.8 umeongezeka. Nchi zinazoendelea ukuaji umetoka 5.0 hadi 4.6. Hapa ukuwaji wa uchumi wa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania umeshuka. Sababu kubwa zilizopatikana ni matatizo ya kushuka kwa uzalishaji na bei za mafuta.
Mhe. Waziri ikiwa ukuaji wa pato la taifa umeathiriwa na maeneo hayo, bila ya shaka na ukuaji wa pato la mwanaadamu la mtu wa kawaida, Mtanzania wa

kawaida, Mzanzibari wa kawaida limeshuka kwa athari hizo. Mimi ambalo nataka niseme kwamba mfumko wa bei mmetueleza humu kwamba imetoka 3.9 kwa dunia hadi 3.5, lakini nchi zinazoendelea wametoka 1.2 hadi 1.3 na nchi za leo zetu sisi zimetoka 3.9 hadi 5.1.

Mhe. Spika, kushuka kwa mambo haya tumeambiwa kwamba imetokana na kushuka kwa bei za mafuta na bei za vyakula. Lakini ukiangalia kwa upande wa Zanzibar Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba ukuaji wa uchumi ni 7.0 kwa mwaka 2014 lakini unatoka na 7.2 mwaka 2013 maana yake nini. Maana yake uchumi wa mwaka jana ulikuwa mkubwa zaidi kuliko uchumi wa mwaka huu kwa maana kwamba 0.2 umeshuka uchumi wetu kwa asilimia 0.2. Sasa Mhe. Waziri nadhani angetuwekea sawa, angetuwekea wazi, kwamba ni juhudi gani ambayo Wizara yake imefanya mpaka uchumi wetu umeshuka kwa 0.2 ya uchumi wa 2013.

Sababu ya kushuka kwa uchumi huo Mhe. Waziri ameelezwa kwamba ni kuimarika kwa sekta ya huduma, sekta ya viwanda, idadi ya watalii na amani na utulivu. Ukiangalia kwa mchanganuo hizi nimefanya mchanganuo hapa kwamba viwanda vimeendelea kushuka lakini idadi ya utalii imeendelea kupanda. Lakini la hatari zaidi kwamba Sekta ya Huduma imeendelea kuongoza kwamba Wazanzibari wanatoa huduma zaidi kuliko uzalishaji. Sasa hii ni hatari, kwamba sisi kazi yetu ni kuhudumia tu, lakini nchi inashindwa kuzalisha. Nchi inapofikia hatua hiyo Mhe. Spika, hii ni hatari kubwa kwamba sisi kazi yetu ni kuhudumia lakini hatuna ongezeko la uzalishaji katika sekta mbali mbali hasa viwanda, kilimo na masuala ya biashara.

Mhe. Spika, mimi ningemuomba Waziri wa Mipango atueleze basi ni hatua gani ambazo bajeti hii itaziba nakisi ile ya ushukaji wa uzalishaji wa viwanda, biashara na masuala ya kudhibiti ongezeko la watalii kwa thamani ya mapato.

Ukiangalia bajeti hii Mhe. Spika, watalii wameongezeka kwa zaidi ya silimia 50, lakini Mhe. Waziri hakutueleza kwamba ongezeko hilo la watalii limeongeza vipi mapato kithamani kati ya mwaka jana na mwaka huu. Mwaka jana ilikuwa laki moja kumi na nane elfu mara hii laki tatu na karibu kumi na moja elfu, ongezeko la zaidi ya laki moja thalathini.

Atwambie basi pamoja na ongezeko hili la watalii limeongeza kazi kiasi gani ya fedha za kigeni hapa Zanzibar. Mhe. Spika, wasi wasi wangu kwamba watalii wanakuja lakini wanaendelea kuja hapa kulala na kutia hasara bila ya kuongezea mtaji kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo ningetaka niseme ni mchango wa sekta mbali mbali. Mchango wa Sekta ya Kilimo ni asilimia 27.9 mwaka 2014. Mwaka 2013

ilikuwa ni asilimia 3.4 ni punguzo la mchango huo wa kilimo kwa asilimia 2.5. Wakati serikali inakiri kwamba mchango wa kilimo umeshuka na unakiri kwamba Wazanzibari asilimia 70 wanategemea kilimo, hii ni hatari, kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Wazanzibari wanategemea kilimo. Lakini mchango wa Sekta ya Kilimo umeshuka kwa asilimia 2.5 nadhani hii ni hatari. Ni hatari zaidi pale nilipoona kwamba sekta ambazo zimeshuka kwa upande wa kilimo ni mifugo na uvuvi.

Mhe. Spika, serikali imekiri kwamba masuala ya bei ya ndizi na samaki zimepanda sana, maana yake Mzanzibari wa kawaida sasa hatokula samaki wala hatokula ndizi, kwa sababu bei ya vitu hivyo zimepanda. Ni kwa nini? Kwa sababu uzalishaji wa vitu hivyo vimeshuka. Athari yake hii ni kwa mfano samaki, samaki ni muhimu sana kwa maisha na mlo wa mwanadamu. Samaki ana *vitamin* vyote, samaki ana protini ambayo inaitwa Albumin, hii kazi yake kubwa ni kuongeza ufahamu kwa watu. Sasa inaelekea na inawezekana wakati Waziri wa Elimu alipokuwa Mhe. Haroun Suleiman labda alifanya ushawishi kwamba wanafunzi wawe wanakula samaki sana.

Lakini wakati huu wa Mhe. Ramadhani Abdalla Shabani samaki hawaliwi kwa sababu bei zimepanda na pengine hakuna taaluma. Ndio maana Mhe. Spika, wanafunzi sasa wa Zanzibar wanafeli kwa kasi mno. Mfano wa hilo Mhe. Spika, kwa kila wanafunzi 100, ambao wanaingia *form five, six* , ni wanafunzi 12 tu ndio wanaoingia Chuo Kikuu. Sasa hii ni hatari kwamba kila 100 ambao serikali inawasomesha na kuwapasisha *form six*, hatimaye wanaoingia Chuo Kikuu ni wanafunzi 12 ni asilimia 12 ya wanafunzi hao.

Mhe. Spika, Kenya, kila penye wanafunzi 100 wanafunzi 60 wanaingia Chuo Kikuu na bado wanahoji kwa nini isiongezeke idadi hiyo ya ufaulu ya wanafunzi. Kwa Zanzibar takwimu zinaonesha kwamba kila wanafunzi 100 wanaoingia *form five* ni 12 tu ndio wanaoingia Chuo Kikuu, athari yake kumbe ni kwamba wamekosa mlo sahihi ambao unaongeza ufahamu na ni kwa sababu ya kupungua kiwango cha Sekta ya Kilimo kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, niseme kwamba biashara ya nje vile vile Mhe. Waziri amekiri kwamba zimeshuka, thamani ya nakisi 2013 ilikuwa ni bilioni 120.3 lakini 2014 ni bilioni 146.0. Maana yake ni kwamba usafirishaji wa biashara, kasi ya biashara ya Zanzibar na nchi za nje bado tunaendelea kushuka kwa kasi kubwa. Kwa maana kwamba Wazanzibari sasa wanaendelea kuwa na kasi ndogo zaidi ya kufanya biashara na nchi za nje kwa thamani hiyo ambayo nimeieleza, bilioni 146.0 nakisi ya thamani ya biashara ya nje 2014.
Mhe. Spika, lakini na wasafirishaji vile vile wa bidhaa kwenda nje Mhe. Waziri amekiri kwamba kasi hiyo pia imepungua. Maana yake ni kwamba mtazamo wa

mapato ya biashara kutoka nje yanaendelea kushuka. Ingawa makontena na biashara kutoka nje kuja Zanzibar yanaendelea kuongezeka. Lakini kwa kweli ni *transit* tu, biashara ile inapitia Zanzibar inaingia Tanzania Bara. Lakini nchi kama Zanzibar Visiwa ni lazima ifanye biashara wenyewe, biashara ya ndani ni lazima iwe kubwa kwa lengo la kuongeza mapato ya nchi yetu na wananchi wetu.

Mhe. Spika, hoja nyengine niende kwenye Uwekezaji wa Sekta Binafsi na naizungumzia Sekta ya ZIPA. Nipongeze binafsi ZIPA kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa umakini; wanafanya kazi kwa bidii kubwa, lakini bado zipo changamoto ambazo ni lazima serikali tuwasaidie ili kuweza kufikia ufanisi wa sekta hiyo. Mhe. Spika uwekezaji katika Sekta ya hoteli ZIPA wanatwambia kwamba umeshuka kwa sababu ya wawekezaji kwamba wameelekea zaidi kwenye sekta ya ukodishaji wa nyumba tena nyumba ambazo zimekodishwa ni miradi 9 badala ya 7 mwa mwaka 2013. Sasa hatuwezi kutegemea sekta ya ukodishwaji wa nyumba tena nyumba yenyewe ni tisa ndio ikichangia kwamba huo ni uwekezaji katika nchi.

Mhe. Spika, nadhani ZIPA tuwasaidie na tuwasaidie zaidi mtaji wa fedha ya utenaji ili waweze kuendelea na kubuni miradi mbali mbali kwa ajili ya kuvua wawekezaji kuja nchini. Hatuwezi kusifia kwamba ZIPA ndio wawe wanasimamia utendaji wakati wanasimamia ukodishaji wa nyumba, nyumba zenyewe ni nyumba tisa ambazo ndizo zinategemea kuleta mapato kwenye Sekta hii ya Uwekezaji kwa upande wa ZIPA.

Mhe. Spika, lakini kipimo cha uwekezaji Mhe. Spika, ni ajira, Mhe. Waziri amekiri kwamba ajira za uwekezaji huo ni za watu 972 kwa 2014, zimeshuka kwa asilimia 28.8 kutoka wafanyakazi 1365 ambao walikuwa ni 2013. Sasa Mhe. Spika, mwaka 2013 ilikuwa ni wafanyakazi 1300 ndio walioajiriwa na Sekta ya Uwekezaji, mwaka huu imeshuka kwa asilimia 28 ambao ni wananchi wetu ambao ni 972 sasa hili si jambo zuri Mhe. Spika lazima tulidhibiti, lazima ZIPA tuwaongezee nyenzo muhimu kwa ajili ya kufanya bidii kubwa.

Mhe. Spika, niwaombe Mhe. Waziri hasa Mhe. Waziri wa Fedha pale ZIPA ambapo wanajenga hoja kwa mujibu wa utaalamu wao, wakamshawishi muwekezaji akaja nchini basi vikwazo ambavyo havina msingi ni lazima viondoshwe ili ZIPA waende mbele kwa kasi mno kwa lengo la kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, hayo ni ya jumla ambayo ningetaka niseme kwamba hotuba hii ya mipango ni nzuri lakini ingetuonesha dhahiri kwamba vipi vifo vya wanawake na watoto vimepungua. Vipi kasi ya ufaulu wa wanafunzi imeongezeka na hii tusipime kwa darasa la saba, *form II* na *form IV* tupime ni wanafunzi wangapi

ambao wanaingia Vyuo Vikuu baada ya kupasishwa. Hii Mhe. Spika, nasema kwamba bado ni ndogo na ni lazima kasi hiyo tuongeze kwa *speed* kubwa kwa lengo la kupima maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa baada ya mchango huo wa hotuba ya mipango niende kwa ufupi sana hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha. Mimi nipongeze kwamba kwa kweli serikali imeweka mfumo mzuri wa PBB. Mfumo huu Mhe. Spika, utawezeshe Wawakilishi sasa kufuatilia utendaji wa taasisi mbali mbali, badala ya kwenda kwenye idara husika sasa Wawakilishi wataenda kwenye programu husika kwa ajili ya kuangalia ufanisi uliofikiwa.

Mimi Mhe. Waziri kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani niwapongeze sana na utendaji wako kwamba sasa mmetusaidia sana kuelekea kwenye kuwapima serikali kwa utendaji halisi badala ya kuangalia makaratasi ambayo hayatusaidii kitu. Lakini nikushauri Mhe. Waziri kwamba uendelee kuongeza vyanzo vya mapato na kusimamia mapato hayo. Bado pamoja na sababu zote ambazo mmezitoa serikali, bado mapato ya serikali hayajasimamiwa ipasavyo. Kama kweli mnahitaji kuongeza mapato ya nchi ni kusimamia vyanzo vya mapato lazima nyenzo za ndani ya nchi zisimamiwe kwa makini sana na hili Mhe. Waziri ni jukumu lako la kusema kwamba kama vile Pemba ulipowasimamisha watendaji ambao si waaminifu, nikuombe kwamba watendaji hao uendelee kuwatafuta, kuwasimamia na kuwaajibisha pale ambapo wanaonesha kwamba wanapoteza mapato ya Serikali lengo kwamba tupate ufanisi katika utendaji wa Serikali.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba bado kuna udanganyifu ya baadhi ya watendaji wa Serikali na Mhe. Waziri, hili usipolisimamia kwa kina basi utaendelea kupoteza mapato siku hadi siku. Kwa mfano Waheshimiwa wenzangu jana pale wamezungumza kwamba haiwezekani nchi hii iwe na sheria lakini watu wanaghushi mpaka usajili ya Kampuni wazi wazi na badala yake watendaji wanalindwa suala la *Transworld Zanzibar* hili Mhe. Waziri, hatulivumilii na leo hapa si pahala pake pa kusema.

Lakini Mhe. Waziri wa Miundombinu ajitayarishe, tutamletea ushahidi kwamba wameghushi usajili wa *Transworld Zanzibar*, walioghushi wanajulikana na tutazuia bajeti ile mpaka watolewe nje ya ofisi kwa uchunguzi, ni kwa nini wakaghushi jambo muhimu sana la nchi. Hii maana yake nini, maana yake ni kupoteza mapato ya nchi. Unaghushi kampuni kwa kunufaisha tajiri, sio malengo ya Serikali, kwa hivyo, hili leo hatulizungumzi hapa kwa upana, lakini ushahidi upo kwamba kuna watendaji wameghushi kampuni ile na kwa hivyo, lazima tuwashughulikie, tuwatambue na tuwachukulie hatua za kinidhamu. Huwezi ukapewa dhamana ya ofisi kubwa kama ile ukaghushi kampuni ya kimataifa kwa ajili ya kufanya *handling* pale uwanja wa ndege wakati huna uwezo.

Mhe. Spika, ushahidi tunao kampuni hizi ni mbili zimesajiliwa mbili; moja 2013, moja ame-*back date*, moja 2014, hatuwezi kukubali hata siku moja lazima Waziri wa Miundombinu ajitayarishe kwa ajili hiyo, lazima tupate maelezo. Umechukua watendaji wa Serikali mpaka Dubai kutia saini kampuni ile wakati kampuni feki, unapotosha Serikali wazi wazi hatuwezi kukubali hili Mhe. Spika, tunatoa angalizo hilo, Serikali ijitayarishe na hasa Waziri wa Miundombinu aje na majibu sahihi, kwa nini akaruhusu watendaji wake wakaghushi kampuni ndani ya macho ya Serikali, mbele ya uso wa dunia, hilo hatulivumilii lazima wawakilishi hili tupambane jambo hili likomeshwe hadharani.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii na niwaambie wawakilishi wenzangu tupitishe bajeti hii ili Waziri turumhusu akusanye na tuwabane Wizara ambazo zina maovu ziweze kuwashughulikia kwa ajili ya Wazanzibari wetu. Ninakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Hija, tunakushukuru naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, baadae afuate Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, wakati Mhe. Amina Idd Mabrouk, anajitayarisha.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, na mimi awali ya yote ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi kuwepo hapa katika Baraza lako kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya kuisimamia Serikali pamoja na kuwatumikia wananchi. Lakini pia Mheshimiwa ninachukua nafasi kukushukuru wewe binafsi kunipa nafasi ya angalau na mimi kutoa mchango wangu ijapo kwa muhtasari juu ya bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala kwa kuzisoma ripoti zao vizuri na kwa ufasaha na kwa ufanisi wa hali ya juu. Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika, nataka nianze mchango wangu kwenye kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, mchango wangu nianze ukurasa wa 14 unaozungumzia makadirio ya mapato kwa mwaka 2015/2016. Mhe. Spika, naomba ninukuu kifungu cha 34,kinasem;

> "Serikali imekadiria kukusanya jumla ya Tshs. bilioni 830.4 ambapo mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia Tshs. bilioni 450.5 na mapato ya nje kwa miradi ya maendeleo Tshs. 347 mpaka mwisho wa *paragraph* hii".

Mhe. Spika, hii ni azma njema ya Serikali kukusanya fedha kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Ninamuomba Mhe. Waziri asimamie vyema katika

ukusanyaji wa fedha hizi na zifikie lengo kama vile ambavyo ametarajia kwamba fedha hizi sikusanywe. Lakini Mhe. Spika, mimi nitazungumza kwa masikitiko kwamba kila mwaka wa bajeti tunakuwa na ukusanyaji wa fedha nyingi na zinaingia katika Serikali, lakini masikitiko makubwa kwamba kunakuwa na mianya ya kuvuja kwa mapato haya kwa watumishi wa Serikali wasiokuwa waaminifu.

Mhe. Spika, masikitiko yangu makubwa kwamba katika Baraza lako hili limegundua matumizi mbali mbali ambayo yanakwenda kinyume na taratibu za fedha, kuna fedha mbali mbali ambazo zimetumiwa ndani ya mawizara lakini hayafuati taratibu lakini hakuna hatua yoyote ya Serikali ambayo inawawajibisha au inawachukulia hatua wabadhirifu hawa wa mali za umma.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri hapa katika masuala mazima ya ukusanyaji ajue kwamba ukusanyaji ni neno moja lakini utunzaji na matumizi ni neno jengine. Je, Wizara yake ikiwa inasimamia shughuli nzima ya fedha na shughuli za maendeleo ya nchi anajipanga vipi kuzuia mianya ya uharibifu na mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa sababu wananchi malengo makubwa kwa wao ndani ya bajeti ya Serikali ni kufikia mafanikio ya maisha yao ya kila siku katika mambo yao mbali mbali ambayo yanawakabili. Sasa Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri, atuambie kwamba amejipanga vipi kuzuia mianya ya uharibifu wa fedha za Serikali zinapokusanywa na watendaji wake.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 27. Ukurasa huu nataka ninukuu maeneo muhimu yaliyozingatiwa katika bajeti ya mwaka wa 2015/2016 kifungu cha 63, Mhe. Spika, naomba ninukuu;

> "Serikali ni ya wananchi na siku zote huwa inafanya kazi kwa ajili yao kwa, kutambua ukweli huu bajeti ya Serikali itaendelea kuelekeza fedha katika maeneo makubwa yanayowagusa wananchi kwa mwaka ujao wa fedha, maeneo muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na haya. Kwanza ni miundombinu".

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo muhimu yaliyozingatiwa katika suala la miundombinu ni nishati, barabara, viwanja vya ndege, bandari na maji na kadhalika. Naomba Serikali iangalie vyema kuhusiana na miundombinu ya uwanja wa ndege uliopo Pemba. Ni juzi tarehe 13, Mhe. Spika, nilikuwepo pale uwanja wa ndege Pemba nataka kusafiri kuelekea Unguja ndege ya Shiri la *Asalaam Air*, kwa sababu ya hali ya hewa ilivyokuwa ngumu ilizunguka katika hewa zaidi ya saa moja na nusu na katika kujaribu kutua iliukosea uwanja ikatua mwisho wa uwanja na kuelekea katika manyasi, *yalla yalla* rehema za Mwenyezi Mungu zikashuka ndege ile ikasita kwa sababu labda ya tope tope zilizokuwemo kwenye manyasi

ikaganda kule. Abiria wote ililazimika wakapokewe kule, wateremshwe kule porini.

Mhe. Spika, sababu kubwa zinazosababisha kupotea kwa ndege ile kukosea njia ni kwa sababu ya miundombinu mibovu ya uwanja wa ndege wa Pemba.

Mhe. Spika, ninakuomba sana Mhe. Waziri katika miundombinu ya kuishughulikia basi miundombinu ya uwanja wa ndege wa Pemba alifanyie suala hili umuhimu wa hali ya juu kabisa. Ninamuomba mwalimu wangu Mhe. Omar Yussuf Mzee, atwambie tatizo hili lini litapatiwa ufumbuzi. Mhe. Spika, ni hatari kubwa kwa kweli waliokuwepo uwanjani siku ile kila mmoja alikuwa anasalia mtume kuiona ndege ile jinsi ilivyo ukosea uwanja.

Mhe. Spika, mara nyingi tunapiga kelele hapa kwamba uwanja wa ndege wa Pemba hauna taa za kuongozea ndege, mpaka leo taa zile bado hazijafanyiwa utaratibu, lini Mhe. Spika, Waziri wa Fedha ambaye ndie uliye na mkwiji wa Wazanzibari wote uwanja wa ndege wa Pemba utawekewa taa ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea na ajali ambazo zinaweza kuwatia watu kilema hata kuwapotezea maisha yao.

Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri aje atwambie kwamba suala hili ni lini litapatiwa ufumbuzi. Lakini mbali ya kuweka taa uwanja wa ndege wa Pemba ni mdogo, lini utatanuliwa ili ndege zenye kiwango cha hali ya juu ziweze kutua pale.

Mhe. Spika, nikiacha hapo niende katika miundombinu ya barabara, Mhe. Spika, tuna barabara nyingi ambazo hazina kiwango zinachimbika kila siku hata barabara ya kutoka Mkoani kuelekea Chake Chake, barabara ile imezidiwa na magari yanayopita. Barabara zinatiwa viraka kila baada ya wakati lakini viraka vile baada ya muda mfupi vinachimbika tena kwa sababu ya kukosekana umakini wa barabara ile ambayo ni ya muda mrefu na inapita magari makubwa makubwa. Ninaiomba Wizara ya Fedha kwa sababu ndie muhudumu wa Wizara zote iangalie kwa umakini mkubwa kuhusiana na masuala mazima ya barabara zetu.

Mhe. Spika, nikiendelea yale masuala ambayo Wizara inaangalia kuyapa vipaumbele ni pamoja na huduma za elimu. Niseme kwamba hotuba hii imezungumzia kwamba kutokana na bajeti ya mwaka 2015/2016 michango yote inayowahusu wazee wa wanafunzi wa skuli za msingi imemalizika. Mhe. Spika, ni jambo zuri na nia njema kabisa ya Serikali, lakini wasiwasi wangu ni mkubwa sana kwa sababu michango ya wazee Mhe. Spika, ilikuwa inawanyanyasa wazee kiasi fulani, kwa sababu wazee wetu wengi ni maskini. Lakini michango ile ilipokuwa ikipatikana pale skuli ilikuwa inasaidia mambo mengi ya uendelezaji wa masomo ya skuli.

Je, Serikali imejipanga kiasi gani kuzuia michango hii ya wazee katika skuli za msingi lakini kuiendeleza skuli kwa mujibu wa mipango ambayo ilikuwa inaongozwa skuli kabla ya kukatwa michango hiyo. Mhe. Spika, michango ya wazee ilikuwa haisaidii chaki na kalamu tu kwa wanafunzi, bali michango hii ilikuwa inasaidia mambo mengi ikiwemo majengo ya skuli, masuala ya michezo ya wanafunzi na masuala ya kulipia walinzi kwa sababu skuli zetu nyingi hazina walinzi. Lakini pia ikiwemo kuwatafuta vijana kusaidia kutokana na upungufu wa walimu wa skuli fulani, fedha hizi hizi za wazee zilikuwa zinasaidia kuwalipia baadhi ya vijana wanaosaidia nguvu ya kazi ya kuwasomesha wanafunzi.

Je, Serikali imejipanga vipi kiukamilifu wake kuziba hii mianya ambayo ilikuwa ikifanywa na michango hii ya wazee. Mhe. Spika, nahofia kuja kutokea mvutano baina ya skuli na wazee kwamba Serikali imepiga *stop* kwamba michango isiendelee, lakini skuli zikashindwa kuendelea kutokana na michango midogo itakayopelekwa skuli kwa Serikali. Kwa sababu hofu yangu inaweza kuwa kwamba Serikali inaweza kuona tu kwamba baada ya kupeleka chaki na mabuku ndio basi. Lakini kuna viti vinakatika, kuna mabanda yanachakaa yanahitaji kufanyiwa matengenezo, kuna walinzi wanalipwa, je, mchango huu ambao Serikali imeusimamisha kwa wazee Serikali inabeba majukumu gani kwa skuli za msingi ambazo zimekatiwa mchango huu.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza katika kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Fedha, niende katika ukurasa wa 30 kipengele cha 68, kinasema, naomba ninukuu;

> "Kwa upande wa elimu ya sekondari, serikali inajipanga ili nako elimu yote iweze kutolewa bila ya malipo kwa kuanzia kwa mwaka wa fedha 2015/2016 serikali inafuta rasmi malipo yote wanayotozwa wazee kwa ajili ya mitihani ya kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita. Wazazi hawatatozwa tena malipo yoyote ya mitihani ya Sekondari kwa watoto wao, Serikali inabeba pia jukumu hili."

Swali kwa Waziri wa Fedha kwani mitihani hii ya kidato cha pili, kidato cha 4 na cha 6 ilikuwa wazee wanalipia? Na kama walikuwa wanalipia walikuwa wanalipia vipi. Kwa sababu wazazi ni sisi, lakini mitihani hii tunaona kwamba tokea zamani ilikuwa inalipiwa na Serikali. Kwa hivyo, hivi sasa tunakatishiwa mkato upi, yaani tunapunguziwa mkato upi wakati ambao tokea mapema tulikuwa hatutoi fedha hizi kwa ajili ya mitihani ya darasa la kumi, 12 na14.

Mhe. Spika, kwa uchache sana niende katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, hapa sitokuwa na mchango mkubwa sana lakini

niende katika ukusara wa 10 kuhusu pato la mwananchi, lakini niende katika mchango wa sekta mbali mbali katika pato la Taifa niende katika sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, sekta ya kilimo ni sekta muhimu sana Zanzibar ni sekta ambayo inawakomboa Wazanzibari wengi kwa kupata mahitaji mbali mbali kupitia kilimo. Lakini inasikitisha sana kwamba sekta hii serikali bado hawajaweza kuisimamia ipasavyo, kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nimuombe sana Mhe. Waziri, wanapozungumza suala la kilimo waliangalie kwa upana wake. Wananchi wengi katika kipindi hiki ambacho walikuwa wanaimarisha konde zao kwa ajili ya kilimo wamesumbuka sana kwa miundombinu ambayo inasababishia kilimo chao kiwe bora.

Mhe. Spika, nitakuja kuchangia zaidi katika Wizara ya Kilimo na Maliasili, lakini kwa sababu ni mpango wa maendeleo na ni mpango ambao umeelezwa hapa lazima napo tuzungumzie ili serikali ielewe kwamba kilimo ni jambo muhimu sana katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Lakini hakuna pembejeo za kutosha katika suala la kilimo.

Kwa hivyo, kipindi hiki kilichopita tumeona wakulima wanavyopanga foleni katika vituo vya kilimo vya wilaya kwa kutafuta mbolea, kwa kutafuta dawa ya kuulia magugu na dawa za kupalilia. Foleni hizi zilitokea na watu walikuwa wakisumbuka kuanzia toka saa mbili za asubuhi mpaka saa 12 jioni bila ya mafanikio yoyote. Linalosikitisha zaidi kwamba dawa za kupalilia watu wanapiga foleni hawapati lakini nyuma yake kuna watu wanauza dawa zile, wanazipata wapi?

Mhe. Spika, niiombe serikali iwe makini sana katika kushughulikia kilimo ili wananchi wetu wajikomboe katika masuala mazima ya kibiashara kupitia kilimo, chakula na mambo mengine, kinyume na hivyo tutakuwa tunasoma tu katika vitabu lakini watu wetu wanadidimia katika umasikini bila ya kupata tija endelevu.

Mhe. Spika, baada ya mchango huu niseme kwamba na mimi niunge mkono hoja. Ahsante sana.

**Mhe. Mlinde Mabrouk Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi asubuhi hii ya leo kupata fursa hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba zote mbili hizi, hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Ikulu na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Fedha, kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee.

Mhe. Spika, napenda kuanza katika kitabu hiki cha Dokta Mwinyihaji Makame. Mimi mchango wangu ni mfupi tu, lakini hasa nimepatwa na wasiwasi, wasiwasi umekuja kutokana na kupungua kwa sekta hizi za uzalishaji. Ukizingatia kwamba

sekta zote hizi muhimu ukiangalia kwenye ripoti ni kwamba zinashuka, sasa kama zinashuka na sisi wananchi tunaendelea kuzaa; mtu mmoja unaweza kumkuta ana watoto 20 na bado anaendelea kuzaa. Sasa kama mpango uko hivi serikali ina mikakati gani ya kuweza labda kupunguza hii idadi ya kuzaa kiholela holela, lakini pia kuinua pato la mwananchi.

Mhe. Spika, ukiangalia sekta muhimu kama hizi za mifugo, uvuvi, kilimo zote zimeshuka. Sasa nilitaka kufahamu kwamba hasa kwenye uvuvi Mhe.Waziri wa Fedha kule nyuma kulikuwa kuna pesa za *MBRI* kwa kila siku tunazungumzia boti za uvuvi, boti za uvuvi, lakini hadi hivi sasa karibu huu mwaka wa tano tunamaliza bajeti hii hakujanunuliwa hata boti moja wala hatujaona kwamba huu mpango lini inawezekana ukawa umetimia, vijana wetu hawa hasa wale ambao walipata mafunzo ya uvuvi wakaanza sasa kwenda kwenye bahari kuu. Kwa sababu bahari ya ndani tumeona imeshakuwa kama imekauka hivi. Sasa nilitaka kufahamu mikakati ya serikali kwenye sekta hii imefikia wapi? Kwa sababu hizi pesa ni za muda mrefu na tuone kwamba serikali imeziongeza tangu muda ule hadi hivi sasa ziko kiasi gani.

Mhe. Spika, sekta ya viwanda na yenyewe imeshuka. Mimi nataka nizungumzie kidogo kiwanda kile ambacho niko jirani nacho, Kiwanda cha Sukari. Kiwanda cha Sukari wamejitahidi kuimarisha bonde la miwa na sasa hivi ukitembelea pale miwa iko mingi, lakini bado wanalalamika kwamba eneo dogo na kwa utanuzi wa kiwanda walioufanya miwa ile haitaweza kuwatosha. Sasa mimi niiombe serikali kwa kuwa tuna shamba letu liko Bara kule la Makurunge nadhani wakae na wawekezaji hawa kwa vile lile shamba lipo tu na limekuwa pori waliobahatika kulitembelea wameona hili, wawape wawekezaji hawa waweze kulima miwa. Kwa sababu kiwanda chao wanasema wakianza miezi tisa wapate miwa ya kutosha ili waweze kusimama kidogo kufanya *services* nyengine.

Sasa shamba lipo hebu kaeni nao hawa, kwa sababu wao wanahamasisha sasa hivi wananchi walime kwenye mabonde ya mipunga yaliyobakia, kweli maeneo Zanzibar hatuna. Mimi niwaombe serikali kama kweli tuna nia ya kumsaidia mwekezaji huyu na kama yeye yuko tayari apewe shamba lile aendeleze miwa yake pale ili kiwanda kile kiweze kuzalisha wananchi wetu waendelee kupata ajira na nchi iweze kukusanya mapato.

Mhe. Spika, nikiendelea tena nimeona hapa hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha, amezungumzia kuhusu ada ya uingizaji magari. Hapo awali ada hii ilikuwa ikitozwa na Shirika la Magari, lakini kwa sasa shirika hilo halipo na ada yenyewe ilikuwa inakusanywa shilingi laki moja, lakini sasa wamesema kwa magari yanayoingizwa inaongezwa asilimia tatu ya thamani ya ile gari na pesa hizi

zitakusanywa na *TRA*. Mimi hapa kidogo nilikuwa niombe tu kama kuna uwezekano wangezifanya *ZRB*. Kwa sababu gani nikasema hivyo.

Mhe. Spika, magari yanayoingia nchini ikitokea mtu kaingiza gari mpya ya thamani basi hapa pana uchakachuaji mkubwa, hapa vijana wanasema unapiga hela ndefu, pesa zinaliwa na zinaliwa vipi. Nitatoa mfano, labda umeingiza gari yako *Land Cruise, V8*, umelipia thamani pengine kwa mfano tu shilingi milioni kumi, gari ile ile anakuja mwengine anaingiza ya aina ile ile panafanyika mambo hapa inabadilishwa tu, labda jina la mwenye gari Omar Yussuf Mzee keshalipia ushuru wake kamili, anakuja mwengine anapewa gari ile ile, jina lile lile lakini anabadilishiwa *chassis number* inaonekana gari ile imelipiwa. Tutakwenda hivi mpaka lini, huku tunategemea tukusanye kodi, kama kodi ndio zinapigwa hivi.

Sasa mimi pesa hizi kukusanywa na *TRA* hapa nimepata mashaka, niombe pesa hizi kama kuna uwezekano tuzihamishie kwengine wao waendelee kukusanya hizo kodi nyengine za magari, lakini hizi kama kuna uwezekano basi zingekusanywa na *ZRB* ili tukaweza kuendelea na mikakati yetu. Lakini pia pesa hizi zikishakukusanywa zinasemwa zinakwenda kutumika kwenye Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Barabara tunavyofahamu kuna pesa zake ambazo pia zinakusanywa.

Mhe. Spika, niiombe serikali kwa kuanzia basi sasa hivi zitapokuwa tayari zimekusanywa kwa miaka hii angalau mmoja au miwili basi zitumike kwenye sehemu nyengine na nitoe mfano. Sasa hivi kuna majumba yetu yamaendeleo ambayo kweli wamepewa wananchi wake lakini hizi nyumba ziko katika hali mbaya.

Kwa mfano, mimi niliwahi kutembelea sehemu moja kule Pemba wanaita Mtemani kuna jumba lile la Mtemani, Wete; jumba lile linazuiliwa kwa myunda, badala ya kuwa unajenga ndio uweke myunda ili uweze kwenda juu, sasa hivi watu wanaishi linazuiliwa kwa myunda ili lisije likawaangukia. Sasa pesa hizi kwa vile pesa za Mfuko wa Barabara zipo, niiombe serikali kwanza ielekeze huko kuyahami haya majumba yetu na hata haya yaliopo hapa Unguja. Mfano makaro yanabomoka mara kwa mara maeneo ya Kilimani na maeneo mengine, angalau kwanza tuhami huku watu wetu wasije wakapata ajali na maafa makubwa, halafu baadae zirudi kama lengo lililokusudiwa zitumike kwenye barabara. Lakini kuendelea kukaa na majumba yale kwa hali ile ambayo iko safi kuna hatari kubwa ya wananchi hawa kuja kupata maafa.

Wenzetu tumeona juzi huko mtetemeko wa ardhi Mwenyezi Mungu atuepushie, yale yetu sisi yanawezekana hata kwa upepo yakaanguka.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mchango wangu ni mdogo, kwa hivyo, naunga mkono hoja hizi zote mbili za Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora.

**Mhe. Amina Idd Mabrouk:** Mhe. Spika, ahsante sana, awali ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kukutana hapa asubuhi hii ya leo tukiwa wazima na afya njema. Lakini pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora kwa hotuba zao nzuri ambazo zenye lengo la kuwatumikia wananchi na kuwapunguzia umasikini. Pia, nichukue nafasi hii adhimu kabisa kuwapongeza watendaji wao kwa kuwasaidia katika kazi zao za kila siku.

Mhe. Spika, vile vile, nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inaongozwa na Dokta Ali Mohammed Shein kutimiza kwa kiasi kikubwa malengo ambayo amejipangia katika mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, hata mtoto anapozaliwa basi anaanza na kukaa, kusimama na hatimaye anaanza kutembea. Kwa maana hiyo basi, niwaombe wananchi wa Zanzibar waipe ridhaa yao Serkali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na Dokta Ali Mohammed Shein ili waendelee kuyamalizia na kuyatekeleza yale ambayo wameyabakisha katika kipindi kilichopita na ninaamini kwamba wananchi wa Zanzibar na *Inshaallah* wataitoa ridhaa hiyo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais na serikali yake kwa ujumla kwa kubeba jukumu la kutusomeshea watoto wetu, lakini hasa kwa kuwaondoshea mzigo wazazi kwa kuwalipia ada ya mitihani wanafunzi wa Kidato cha Pili, cha Nne na cha Sita. Kwa kweli wazee walikuwa wanalalamika sana katika suala hili la kuwalipia watoto wao ada za mitihani. Kwa maana hiyo basi, ninaamini kwamba serikali kuwaondoshea mzigo wazazi hawa kutawapa fursa pesa ile ambayo ingetumika kwa kuwalipia wanafunzi watafanyia masuala mengine ya kijamii.

Mhe. Spika, pia, naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na Dokta Ali Mohammed Shein kwa kuwatunza wazee wetu kwa kuwaongezea pencheni kutoka shilingi 20,000 hadi kutimia shilingi 60,000. Haya ni yale yale kuendeleza Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo yameanzishwa na Rais Mstaafu Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo basi sasa mimi naomba niingie katika kitabu hiki, mchango wangu hautokuwa mkubwa sana kwa sababu wengi wao wameshachangia na wamezungumza yale ambayo nilikuwa nataka kuyazungumza. Kwa hiyo, natekeleza kama Kanuni zetu zinavyotutaka tusiwe tunarejea rejea.

Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 19 katika kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha. Mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa nia yake ambayo ametueleza hapa katika kitabu, kwamba ana mpango wa kuanzisha utaratibu wa kutumia mashine za kutolea risiti (*EFDs*). Mimi nakubaliana sana na wazo lake hili sio baya, lakini labda niseme kwamba ushauri wangu suala hili kwa kule Bara wenzetu walikuwa na wazo hili karibu miaka mitatu nyuma, lakini limeanza kutumika kama mwaka mmoja tu uliopita. Tumeona sote tunashuhudia matatizo ambayo yamejitokeza kwa wenzetu wa Bara. Kulikuwa na malumbano makubwa na mpaka sasa hivi kuna vikao kadhaa wa kadhaa vinaendelea na suala hili bado halijapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, labda mimi nimshauri tu Mhe. Waziri wa Fedha kuwa suala hili waliangalie kwa umakini mkubwa sana, lakini pia waangalie na mazingira tulionayo hapa kwetu Zanzibar. Mimi naamini kwamba malumbano yaliyokuwepo kule kwa wenzetu Bara kati ya serikali na wafanyabiashara hayawezi yakawa ya bure bure lazima mfumo huu una matatizo yake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kabla ya kulianzisha wakae waliangalie kwa umakini mkubwa ili na sisi hapa kwetu lisituletee matatizo kati ya serikali na wafanyabiashara.

Mhe Spka, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 30. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuendeleza mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wetu. Mimi naamini kwamba vijana wetu wanafaidika sana na mikopo hii. Lakini mikopo hii imeanzishwa toka mwaka 2011 na kwa wale ambao *courses* zao za miaka mitatu basi ni dhahiri kwamba mwaka jana wamemaliza mikopo hii na hawa wengine wamekuwa tayari wameshaajiriwa na wanafanya kazi.

Mhe. Spika, sasa nilitegemea hapa Mhe. Waziri tutaona mapato ambayo yamerejeshwa kwa hawa wanafunzi ambao wamemaliza masomo yao na wameanza kazi. Lakini kwa bahati mbaya sana katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri tunaona tu hii hali halisi ya mikopo lakini hatuoni marejesho yao.

Lengo kubwa ni kwamba wanafunzi tuwapatie mikopo ndio lengo kuu la serikali, lakini kama tulivyokuwa tunaambiwa kwamba mikopo hii itatolewa baada ya hapo wanafunzi watakaoajiriwa tu, wataanza kurejesha mikopo hiyo. Sasa Mhe. Waziri kama mikopo hii imetolewa kama ruzuku tu basi ni sawa, lakini kama lengo la

mikopo hii kuwa irejeshwe hatimaye marejesho yale wafaidike wanafunzi wengine na vijana wetu kwa ujumla.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri atapokuja hapa anieleze kwamba hii mikopo ni kama ruzuku au lengo kuu ni kupewa wanafunzi lakini hatimaye warejeshe ili waweze kufaidika na mikopo hii vijana wetu wengine.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana kwa sababu wengi wao wameshachangia na ili kuepusha yale marejeo basi Mhe. Spika, niseme kwamba niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikiongozwa na Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuwasaidia wananchi, lakini pia kwa kuwasaidia kina mama kwa kuwafutia ile ada ambayo wanailipa hospitalini ya uzazi. Naomba wananchi tuendelee kuichagua Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ili iendelee kutusaidia wananchi wa Zanzibar. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, tumalizie basi tena kwa kifupi kwa Mhe. Mohammed Haji Khalid.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa ya kuchangia machache katika hotuba hizi mbili ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa katika ukumbi huu kwa ajili ya kazi zetu za kawaida na tukiwa katika hitimisho la miaka mitano iliyopita tukiwemo katika ukumbi huu. Hii ikiwa ni Bajeti ya mwisho tunangojea baada ya uchaguzi kuendelea na mengine.

Mhe. Spika, hotuba hizi nizipongeze Mawaziri kwa uwasilishaji wao mzuri na mipango mizuri waliyoiandaa katika kuhakikisha kuwa pindipo ikitekelezwa itaweza kulikwamua Taifa letu hapa lilipo, kama walivyotajwa wenyewe kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi masikini sana, wametaja hivyo wenyewe. Sasa umasikini huu kama haya yaliyoandaliwa humu yakitekelezwa kwa kima fulani umasikini unaweza ukapungua.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kidogo na Hotuba ya Mhe. Fedha na nianze katika Sekta hii ya Miundombinu. Mhe. Spika, kwenye Miundombinu kataja mambo kadhaa yakiwemo wa barabara, viwanja vya ndege , nishati, maji na nakadhalika.

Mhe. Spika, barabara zetu tunazojenga nyingi zao hazina kiwango au wanaopewa kujenga barabara hawana utaalamu na hili linajitokeza katika wakati huu wa mvua nyingi hapa nchini, barabara zetu takribani zote zinaponyesha mvua zinageuka mito na maziwa, maji hayana pa kukimbilia huu ni ukosefu wa ufundi wa ujenzi.

Ni aibu iliyoje barabara ambayo inaelekea kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume wa Zanzibar kuwa barabara hii inakuwa kama *River Nile*, ni ajabu na ni aibu iliyoje kwa maji hayana pa kwenda. Maji yanapotuwama hatimae yanatafuta pa kukimbilia yanazama chini na yakizama lami inatanuka na hatimae inapasuka barabara inakuwa na mashimo ya hapa na pale.

Kwa hivyo, bado hatujapata wahandisi na mafundi wa ujenzi katika suala hili. Ningeomba serikali kwa hilo tunapokuwa na ujenzi wa barabara watafute mafundi, wakandarasi ambao wana udhoefu wa kujua ujenzi wa barabara kwa nchi yetu ilivyo.

Mhe. Spika, hata ule Uwanja wa Ndege unavyokwenda, hata baada ya mvua kupita bado maji baadhi ya mwahala yanakuwa yametuwama. Hizi ni kasoro kubwa tena sana.

Mhe. Spika, Mheshimiwa, mmoja kasema hapa juzi alikuwa anasafiri tulikuwa pamoja kutokana na ubovu wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, kutokana na kuwa hauna taa za kuongozea ndege pale chini, kuna kidege kilitembea na hatimae kikatoweka msituni.

Mhe. Spika, tena mimi na huyo mwenzangu tulikuwa majasiri kwa sababu ndege ile ile iliyopotea na hatimae ilivutwa kwa trekta ndio tuliyopanda kurudi Unguja, kuna watu wametushangaa kweli kweli kuwa chombo kimepotea kimekwenda msituni bila ya kufanyiwa *service* yoyote tukaingia hivyo hivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, Zanzibar tunaunda ajali sisi wenyewe kwa kushindwa kushughulikia miundombinu yetu tuliyoiweka.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naona wengine wanatoka toka na nimesema kuwa huyu ni mchangiaji wa mwisho, mkitoka maana yake hatutaweza kuendelea na shughuli hii. Niwaombe walioko nje na aliyetoka sasa hivi arudi. Tuendelee Mheshimiwa.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, ningeiomba Serikali isiunde ajali, kazi ya Serikali ni kujaribu kuondoa na kupunguza ajali. Lakini miundombinu yetu tulionayo inaunda ajali, huu ni msiba.

Mhe. Spika, hapa tumezungumzia huduma za elimu na kuna sentensi iliyoandikwa kwa wimo mzito kabisa na Mhe. Waziri wa Fedha, iliyosema hivi;

"Natamka rasmi kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 michango yote inayotozwa wazazi kwa kwa elimu ya watoto wa Skuli za Msingi imefutwa,

hakuna mzazi atakaetozwa malipo yoyote kwa mtoto anaesoma Skuli ya Msingi ya Serikali, hii imefutwa."

Mhe. Spika, hii kwani nani aliyeirejesha baada ya Mzee Abeid Aman Karume kutangaza elimu bure, nani alierejesha malipo? Hata leo serikali inatwambiwa kuwa inafuta malipo, nani alirejesha? Nataka Mhe. Spika, nielezwe nani alierejesha na alirejesha kwa sababu gani au alikuwa anampinga Mzee Abeid Aman Karume huyu aliyeirejesha?

Kwa sababu elimu ilipotangazwa bila ya malipo mimi nilikuwa tayari niko duniani na wakati wote huo sijamsikia Rais yeyote alitengaza kurejesha malipo. Leo Serikali inatwambia inafuta, nani aliyerejesha? Mhe. Spika, kama ilikuwa tunalipishwa na ilikuwa tunalipishwa kweli, ilikuwa tunalipishwa kinyume na taratibu.

Lakini Mhe. Spika, mimi hili nalipongeza kuwa limerejeshwa kinyemela na leo linafutwa rasmi. Lakini sisi wazazi tayari tumesikia kuwa malipo haya yameondolewa. Katika hali hii Mhe. Spika, kuanza mwaka huu wa fedha wazazi wamesikia, kwa hivyo, hakuna mzazi atakaeambiwa na mtoto wake kuwa anataka buku akamnunulia, hakuna mzazi atakaeambiwa kuwa nimeambiwa nipeleke pesa za kununulia chaki akatoa, kwa sababu serikali imetamka rasmi kuwa mambo haya sasa basi.

Je, ni kweli serikali imejipanga kuweza kupata vitabu na mabuku ya kuandikia kwa skuli zetu zote za msingi? Isije kuwa maneno haya yamo kwenye karatasi tukawageuza walimu na wazazi ikawa wanavutana, kwa sababu mwalimu hatoweza tena kumwambia mtoto mwambie baba akununulie buku, mwalimu hatoweza tena kumwambia mwanafunzi lete pesa ya chaki.

Mhe. Spika, bado ufundishaji wetu wa kusema na kuandika haujabadilika. Kwa hivyo, walimu wanahitaji chaki ili waandike kwenye ubao, chaki inanunuliwa, serikali tayari imeweka bayana kuwa michango hii haiko tena, ghofu yangu pamoja na bilioni zilizotwaja lakini itafika siku mwanafunzi anataka buku akaambiwa kuwa buku haliko na tayari serikali imetoa tangazo hili.

Ningeiomba serikali kama haijajipanga ijipange ili mwaka huu wa fedha ukianza maskuli, mabuku na chaki ziwe ziko kama vile nilivyokuwa nikisoma mimi, vyenginevyo, itakuwa tumewaongezea walimu mzigo ambao hauna maana.

Kadhalika tumeondoa ada ya kulipia mitihani lakini Mhe. Spika, malipo haya yaliyofutwa kwa ajili ya mithani ya darasa ya 10, 12 na kidato cha 6 kwa ajili ya mitihani hii, wazee bado hatujalipishwa kwa sababu mimi nina watoto wanaosoma katika vidato vyote hivi, wanaodaiwa ni watoto wangu na ni wanangu. Sasa hapa

panafuta nini au panaondolewa nini, panaondolewa jambo ambalo toka zamani halipo.

Mhe. Spika, nije kwenye wazee, niwapongeze hapa kwa kima fulani wazee tumewajali tumewaongezea kidogo pencheni zao. Kwa hivyo, hii ni hatua moja ya serikali angalau kuona kwamba hawa wazee na wao huko nyuma walitoa mchango katika nchi hii na ndio ikafikia hapa tulipo hivi sasa.

Mhe. Spika, nije kidogo katika kitabu cha Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Hapa nizungumze kidogo katika Sekta ya Kilimo. Mhe. Spika, nchi hii kila siku tunafanya jambo moja kuwa ni uti wa mgongo, haijambo siku hizi kilimo si uti wa mgongo tena kwa hivi Mhe. Waziri, alivyoitaja kwa sababu mazao ya kilimo na mifugo kila mwaka yanapungua. Kupungua kwa mazao ya kilimo, kwa hivyo, itakuwa kila mwaka tunaongeza kuagiza bidhaa kutoka nje. Kwa sababu sisi tunazalisha kidogo matumizi yetu ni makubwa hii ina maana uagiziaji wa bidhaa kutoka nje utaongezeka, ukiongezeka pesa kidogo iliyopo tunaitoa nje na sisi mazao yetu tunayosafirisha ni kidogo, kwa hivyo, badala ya nchi hii kutononoka kiuchumi kwa kweli tutakuwa tunaagizia zaidi kutoka nje kuliko vile tunavyosafirisha, kwa hivyo, ule umasikini tunaoutabiri kuundoa au kuupunguza itakuwa siku hadi siku baada ya kupungua unaongezeka. Je, serikali ina mpango gani wa kuimarisha hizi huduma za kilimo na mifugo ili ziweze kuwa endelevu na zitoe tija zaidi baada ya kila mwaka zinarudi chini baada ya kuongezeka.

Mhe. Spika, mazao yetu yanaathirika kwa magonjwa mbali mbali kama mihogo inakumbwa na wadudu wanaoathiri mihogo, migomba kadhalika na bado serikali haijachukuwa hatua muafaka ya kutafuta tiba ya magonjwa haya ya mazo yetu ya kilimo. Kwa hivyo, ningeiomba serikali ifanye utafiti wa magonjwa yanayoathiri mazoa ya mashambani hasa mihogo na migomba, baadhi ya migomba kule kwetu Pemba ndizi unaigundua kuwa imewiva na bado ni changa imeathirika kutokana na maradhi ya migomba.

Mhe. Spika, kipindi kilichopita niliuliza swali juu ya mti mbaya sana mtunda kanga unaoathiri mazao yetu ikiwemo hata mikarafuu. Nashukuru kuwa Wizara ya Kilimo haikudanganya ilisema haijafanya utafiti wowote juu ya athari ya mti ule. Sasa mti ambao upo unaathiri na wizara ipo inaona lakini hakuna utafiti iliofanywa ili kujua athari zake, je, hii serikali kwa ujumla inaimarisha mazao ya kilimo au inadumaza, kwa sababu inaona kuwa upo mmea ambao unaathiri lakini hakuna utafiti wowote uliofanywa kuona yale madhara yake. Kwa hivyo, ningeiomba serikali mmea ule ni adui tena mkubwa wa mazao yetu, ufanywe utafiti na ikiwezekana upatiwe tiba ya kuuangamiza kabisa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache niseme kuwa hapa limezungumzwa pato la Taifa na pato la mwananchi...

**Mhe. Spika:** Unazo dakika tatu tu kumaliza hotuba yako.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Pato la Taifa na pato la mwananchi. Mhe. Spika, bado kwa pato hili la mwaka kwa mwananchi inaoneshea bado hali ya uchumi wetu haujatononoka kama vile wenyewe tunavyojiona kuwa uchumi umekuwa. Kwa sababu wastani uliotajwa hapa wa pato la kila mwananchi ni mdogo mno. Kwa hivyo, iko haja ya kuongeza bidii ya ukusanyaji wa mapato ili tapo letu la Taifa liweze kuongezeka na wananchi wakwamuke katika hili dimbwi la umasikini linalotukabili. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Mohammed Haji Khalid, kama nilivyotangulia kusema kwamba huyu alikuwa mchangiaji wa mwisho alieniletea ki-*note*, baada ya hapo basi itabidi umuandikie Mhe. Waziri haraka haraka kama kuna jambo muhimu kwa maandishi. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora.

Ninategemea na yeye atafanya majumuisho kwa uwazi lakini kwa ufupi ili nipate *quorum* hii kupitisha hoja hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa mara nyengine tena kunipa wasaa huu wa kufanya majumuisho ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu walipokuwa wakichangia hotuba mbili hizi zetu; kwanza ya mwenzangu ya Waziri wa Fedha na ya pili hii niliyoitoa mimi ya hali ya uchumi ya mwaka 2014 pamoja na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2015.

Mhe. Spika, kama utaratibu wetu ulivyotuwekea mimi nitajikita kwa upande wangu ulioguswa na Waheshimiwa Wajumbe wakati wakichangia kwa upande wa uchumi wa mwaka 2014 na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2015.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataallah* kwa kutuwezesha kwa mara nyengine tena kufika mbele ya kikao chako kutoa ufafanuzi wa michango hii ya Wajumbe kama nilivyosema. Kwa ujumla Mhe. Spika, tulikuwa na michango niliyoipata upande wangu ni 21; wakati waliochangia humu ukumbini ni 18 na 3 wameniletea kwa maandishi.

Kabla ya kuwatambua naomba muhtasari tu Mhe. Spika, niseme kwamba Waheshimiwa wote kwa kweli niwashukuru sana kwa michango yao ambao wote niseme wameikubali hotuba yangu au hotuba zetu mbili. Muhimu wametaka tufanye kuzifanya uwe bora zaidi mipango yetu, kwa dharura ninasema tuseme

tuiboreshe, aah! tuifanye iwe bora zaidi. Ninafikiri hilo ni suala la msingi sana na siku zote ukiwa na mipango mizuri ndiyo utekelezaji nao unakuwa mzuri na hata tena sekta zetu nyengine hasa ya fedha ambao wao ndiyo wenye nyenzo watatupatia vizuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema Waheshimiwa takriban wote wameiunga mkono hotuba yangu na kuna salamu maalum zimetolewa kwa Mhe. Rais kwa uongozi wake mzuri wa kusimamia uchumi wetu na maendeleo ya nchi kwa ujumla, akiwa yeye pia kwa nafasi yake kama Mwenyekiti wa Tume ya Mipango. Kwa hivyo, zile salamu ambazo umetupa kwa Mhe. Rais tumezipokea kwa niaba yake na tutamuwasilishia.

Aidha, lakini naomba pia nikupongezeni kwa salamu mbali mbali mulizotoa kwa Mawaziri mbali mbali pamoja na watendaji, nao pia wengi wao wapo na wamesikia na pale ambapo labda hatukufanya vizuri, basi tunachukua ahadi kwamba tutajirekebishe tuone yale mapungufu tunayaweka sawa. Na nafasi nzuri kama mulivyosema munazo kwenye sekta zenyewe zikija kutoa bajeti zao kwa ufasaha zaidi.

Ushauri muliotupa Mhe. Spika, tumeupokea na masuala yale mbali mbali tutajaribu kuyajibu kwa kifupi sana, lakini kwa ujumla itakuwa ni kama cha kufungua kazi kwa mwaka mpya ujao wa fedha kwamba tuone ushauri wenu huu kama ni dira au ni chachu ya kupanga vizuri mwakani.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, moja kwa moja naomba niwatambue Waheshimiwa waliochangia:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Makame Makame Mbarouk
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali
4. Mhe. Raya Suleiman Hamad
5. Mhe. Mwanaidi Hassan Mussa
6. Mhe. Fatma Said Mbarouk
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
10. Mhe. Omar Ali Shehe
11. Mhe. Ali Salum Haji
12. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
13. Mhe. Ali Mzee Ali
14. Mhe. Mussa Ali Hassan
15. Mhe. Asaa Othman Hamad

16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Hija Hassa Hija
18. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
19. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
20. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
21. Mhe. Mohammed Haji Khalid

Wote tunasema tunawashukuru sana kwa michango yenu, wakati ulikuwa mdogo lakini kwa ufupi tu mengi muliyotupa tumeyapokea, tumeyasikia na tutayazingatia.

Mhe. Spika, kimaandishi waliochangia ambao wameniletea ni:-

1. Mhe. Salma Mussa Bilal
2. Mhe. Nassor Salim Ali
3. Mhe. Marina Joel Thomas

Kwa ujumla wote tunawashukuru na tunasema tena kwamba michango yao tumeipokea.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza wakati naomba kwa haraka haraka nizungumze ile michango au nijibu hoja ya yale ambayo yametugusa.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, yeye alikuwa kwa ujumla mambo kama matano, mambo mengi yalikuwa kama mambo saba. Kwa hivyo, kwa haraka haraka nitajaribu kuyagusia.

Kwanza aliuliza swali au alitoa hoja kwa namna gani wananchi wamefaidika kwa kuungiwa umeme kwa asilimia 28. Mhe. Spika, umeme ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla. Umeme unamnufaisha mwananchi kutokana na shughuli anayoifanya kwa mfano uvuvi, ushoni, biashara ndogo ndogo, kilimo, upatikanaji wa maji safi na salama, shughuli za afya, elimu na kadhalika. Kuongezeka kwa wananchi kuungiwa umeme kwa asilimia 28 kumeleta mabadiliko katika kaya zilizofaidika katika huduma hiyo.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka zamani mitaa yetu ya ng'ambu tulikuwa tunazihesabu nyumba ambazo zina umeme, tunaita duu! nyumba hiyo ina simu, nyumba hiyo ina mfereji, tunazihesabu. Leo sijui kama zipo labda tunahesabu nyumba ambazo hazina umeme, imekuwa kinyume, Hayo maendeleo yapo wazi wazi, hayataki tochi hayo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninamuunga mkono Mhe. Mwenyekiti, alitaka nitoe ufafanuzi lakini ninaamini na yeye anafahamu. Hata Jimbo la Kwamtipura ninaamini aliko umeme umekwenda nyumba kwa nyumba. Hayo maendeleo makubwa sana Mhe. Spika.

Kwa upande wa uvuvi tunaona wavuvi wanaweza kuhifadhi samaki katika kipindi cha bamvua na kuendelea kuuza samaki kwa bei muda wote. Aidha, ushauri wa Mhe. Mwenyekiti, kuitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kufanya tathmini, rai yake hiyo tumeichukua. Hata hivyo, ninapenda kumjuulisha kwamba Ofisi ya Mtakimu Mkuu inaendelea kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya ambayo kwa kawaida unafanyika kila baada ya miaka mitano na unatoa viashiria vingi vikiwemo viwango vya umaskini kwa sasa. Ofisi hii pia imo katika hatua ya kukusanya taarifa za mapato na matumizi ya Kaya kwa mwaka 2014/2015.
Mhe. Spika, hoja ya pili ya Mhe. Mwenyekiti, aliulizia au alizungumza suala la kuongezeka kwa idadi ya skuli za msingi na sekondari kumefikia vipi dira ya maendeleo ya 2020 ya Zanzibar na MKUZA 11. Mhe. Spika, maendeleo ya elimu yameweza kuonekana hasa kwa kuongezeka kwa ufikaji wa elimu kutokana na kuongezeka kwa skuli kama tulivyoeleza kwenye hotuba. Kwa upande wa uandikishaji kutokana na umri (*Net and Enrollment Rate)* imefikia asilimia 83.6 kwa elimu ya msingi.

Aidha, uandikishaji kwa ujumla *(Growth and Enrollment Rate)* imefikia asilimia 124.5, tumevuka lengo kabisa la millenium. Uwiano wa wanawake na wanaume msingi ni 101, sekondari ni 118 na elimu ya juu 137. Taarifa hizi mpaka kufikia mwaka 2013. Muamko wa wazazi umepelekea kuongezeka kwa wanafunzi wanawake maskulini na kuimarika kwa mazingira ya skuli kama vile kupatikana huduma vya vyoo na kadhalika.

Mkazo kwa sasa ni kuimarisha ubora wa elimu ikiwa ni pamoja na kuweka maabara, madawati, walimu wenye sifa na msisitizo kwa masomo ya Sayansi, Kiingereza na Hesabu. Hapa naomba pia kumgusa Mhe. Hija Hassan Hija, alitaka kujua kwamba mafanikio isiwe kwa kujenga idadi ya skuli tu, lakini zaidi kwa watoto wanapasi viwango gani. Kwa hivyo, tuki-*improve* kwenye mambo haya; madawati, maabara, walimu wenye sifa, ninafikiri lile lengo letu la kupata *quality education* nalo tutafanikiwa.

Suala la tatu, aliloulizia Mhe. Mwenyekiti ni mpango wa maendeleo kwa mwaka 2015/2016 haujaeleza wazi au wazi wazi idadi ya wanafunzi waliomba na waliopata mikopo. Naomba kusema kwamba kitabu cha pili cha hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2014 na mwelekeo wa uchumi kwa 2015 kimeeleza wazi wazi katika ukurasa wa 74, mchanganuo wa wanafunzi waliomba na waliopata

mkopo kwenye Kifungu 11.4 "Elimu ya Juu" kinaeleza kwa ufasaha kabisa, sitaki kurejea tena *figures* zote zipo wazi kabisa.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wanafunzi wa Zanzibar wanapata mikopo kutoka Bodi ya Elimu ya Juu ya Tanzania. Aidha, kwa upande wa utoaji wa mikopo ya hapa Zanzibar kuna vipaumbele vya mafunzo ya elimu ya juu, kama vile udaktari, uhandisi na walimu wa sayansi na kadhalika.

Mkazo wa Serikali kwa sasa ni kusimamia urejeshwaji wa mikopo kwa waliobahatika kupata kazi ili kupata uendelevu wa mfuko huo. Huo mfuko ni *revolving*, tunataka hawa waliopata walipe ili wengine nao wapatiwe. Sasa naomba kama Waheshimiwa sote, kama tulivyosaidia vijana hawa kupata mikopo basi ninaomba sana tusaidiane kuirejesha mikopo ili ipate kuendeleza vijana wengine.

Mhe. Mwenyekiti kifungu cha nne alitaka kujua ni mipango yetu haielezi wanafunzi waliohitimu katika fani gani na mapungufu yaliyojitokeza. Ukweli ni kwamba utafiti wa hali ya utumishi nchini unaofanywa na Tume ya Mipango kila baada ya miaka mitano huainisha wazi wazi mapungufu na huwa ni kigezo cha kuibua maeneo ya mahitaji ya wataalamu nchini.

Kifungu cha tano Mhe. Mwenyekiti, alizungumza ni kiasi gani ukuaji wa uchumi unakwenda sambamba na ustawi wa jamii katika eneo la afya, ikiwemo kupunguza vifo vya akinamama wajawazito, vifo vya watoto wachanga na watoto chini ya miaka mitano.

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi unaongezeka kutokana na ongezeko la madaktari, watabibu, wakunga na wahudumu wengine ni kama ifuatavyo.

- Kwa kila akina mama laki moja kwa mwaka 1998 walikufa 377.

- Lakini mwaka 2012 idadi hiyo imepunguka mpaka 307, hii ni *figure* iliyotokana na sensa ya watu na makaazi.

Kwa hivyo, *trend* inaonesha tuna-*improve* kadiri ya siku tunavyokwenda. Aidha, takwimu za vifo vya watoto zinaonekana katika kitabu cha hali ya uchumi wa Zanzibar kwenye katika ukurasa wa 82. Kwa urahisi taarifa hizo zinaonesha kwamba vifo vya watoto wachanga navyo vimepungua kutoka 120 mwaka 1988 hadi 46 katika kila watoto elfu moja waliozaliwa.

Pia, kwa mwaka 2012 katika vifo vya watoto waliozaliwa, hai mwaka 2012. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano navyo imeshuka kutoka 202 mwaka 1988 hadi kufikia 66 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2012. Hii *trend* inaonesha

wazi wazi kwamba kwa kweli tunafanya vizuri katika mambo ya afya kwa ujumla ikijumlisha elimu ile tunayotoa na tiba za wazazi na ushughulikiaji wa wazazi kwa ujumla.

Mhe. Spika, suala jengine la sita ambalo Mhe. Mwenyekiti, amezungumza ni suala la mfumko wa bei Zanzibar kwamba hajadhibitiwa. Wafanyabiashara wanaendelea kufanya wanavyotaka katika biashara huria. Mhe. Spika, ukweli ni kwamba Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kudhibiti mfumko wa bei kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 23 mpaka 24 wa kitabu cha Hali ya Uchumi.

Taarifa zinaonesha kuwa mfumko wa bei umetoka asilimia 18.8 mwaka 2011 hadi kufikia asilimia 5.6 mwaka 2014. Miongoni mwa juhudi zilizochukuliwa na Serikali ni kusimamia mwenendo wa bei za bidhaa na huduma kwa wafanyabiashara. Vile vile, Serikali inaendelea kusimamia bei za mafuta na nishati kwa jumla.

Hata hivyo, kuwepo na kuanza kazi kwa *Zanzibar Utility Regulatory Authority (ZURA).* Hichi ni chombo maalum ambacho kitakuwa kinadhibiti mwenendo wa bei za mafuta. Kutatatua changamoto nyingi zinazojitokeza au zitajitokeza katika kusimamia masuala ya bei za mafuta.

Mhe. Spika, hoja ya mwisho ya Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu Tume ya Mipango kusimamia kikamilifu miradi yote inayoibuliwa na Halmashauri na Mabaraza ya Miji hasa katika matumizi bora ya ardhi. Naomba kulijuulisha Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, kwamba kwa mujibu wa sheria ya Tume ya Mipango Na.3 ya 2013, miongoni mwa majukumu iliyopewa Tume ya Mipango ni kusimamia na kutathmini miradi yote ya maendeleo nchini.

Kwa hivyo, ushauri wako huu tumeupokea. Hivi sasa Serikali imetoa tena muongozo kwamba mradi wowote wa maendeleo unaotaka kuanzishwa katika sekta yoyote basi lazima upitie na kuidhinishwa na Tume ya Mipango. Kwa hivyo, tunaratibu miradi yote mipya kwenye chombo kimoja, isiwe vyombo mbali mbali vinaanzisha mradi halafu tunagongana. Kwa hivyo, tume-*centralized* mambo yote ya miradi kwenye Tume ya Mipango ianzie hapo. Sekta zote kama unaibua miradi basi wailete Tume ya Mipango, hapo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ndipo tutakapoanzia. Kwa hivyo, ule mradi wako uliosema wa *SECRONA*, tafadhali ulete tutaupitisha na tutauzingatia kwa taratibu ziliopo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana alikuwa na mambo mengi lakini mengi yalikuwa yakitushauri na ilivyokuwa tulikaa naye kwa zaidi ya siku tatu, mengi kwa kweli tumeyapokea na tumechukua. Sasa naomba niingie sehemu nyengine nimguse Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Fatma Mbarouk Said

na Mhe. Omar Ali Shehe. Kwa nini tumewaweka pamoja, kwa sababu michango yao kwa ujumla imelingana sana na michango yao zaidi ni mitatu.

Naomba niitaje:

1. Walitaka kujua au walituagiza kwamba tutumie fursa ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*) katika miradi mbali mbali ikiwemo mradi wa kilimo ambao tayari mwekezaji yupo tayari;

2. Wametushauri tutumie wataalamu wa ndani katika kutoa ushauri; na

3. Wametuagiza kwamba tuwezeshe sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza uwekezaji Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kujibu hoja hizo tatu. Ninasema kwamba Serikali tayari imepitisha sera na Sheria ya *PPP*. Mwekezaji yeyote anakaribishwa kuekeza katika njia ya *PPP* kwa kufuata sera na Sheria ya *PPP*. Hilo ndiyo suala la msingi kwamba tufuate sheria iliopo. Wengi wa wawekezaji wetu kwa bahati mbaya Mhe. Spika, huwa wanajaribu kuchukua *short cut*, kumbe wanajikwamisha. Kwa hivyo, ninawaomba sana taratibu zipo, wakifika *ZIPA* wataelekezwa vipi vya kufanya, wakifuata hivyo ninafikiri hakuna matatizo na wanakaribishwa.

Mhe. Spika, tuna imani kuwa hakutokuwa na mwekezaji ambaye atazungushwa iwapo taratibu zitafuatwa, wala sio nia ya serikali kumzungusha mwekezaji yeyote Mhe. Makame Mshimba, hatuna utaratibu huo. Pindipo akitokea mtu ana sifa hiyo basi tusikae kimya tuambizane ili mara moja huo ukiritimba uliopo tuweze kuuvuka na kuusimamisha. Kwa hivyo, nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe sote tujitahidini kufuata utaratibu.

Pili, serikali kwa sasa inatoa nafasi za upendeleo kwa wataalamu wa ndani katika zabuni, ili kupunguza kutumia washauri elekezi wa kigeni. Tumeshauriwa kwamba hawa *consultancy* wasiwe wa kigeni, tujaribu sana kupata wetu na tunao *Alhamdulillah*, wataalamu sasa tunao wazuri tu na wanafanya vizuri, yaani *papers* zao na kazi zao wanazofanya kwa kweli zinaridhisha kabisa, ni lazima tujenge *confidence* kwa wataalamu wetu wenyewe ambao tunawasomesha kwa pesa zetu.

Mhe. Spika, jawabu jengine ni kwamba upande wa MKUZA II imetambua kuhusu uendelezaji wa sekta binafsi kwa kuweka lengo mahususi la kuanzisha sekta binafsi iliyoimara kwa kukuza uchumi, ni kuwa na mikakati wa kurahisisha upatikanaji wa mikopo na kujenga ujuzi katika usimamizi wa biashara, kukuza

ufikiaji wa teknolojia na kuanzisha fursa za kibiashara na urahisi wa kulifikia soko. Aidha, serikali imo katika matayarisho ya mkakati wa kuendeleza sekta binafsi, yaani *Private Sector Development Strategy.*

Mhe. Spika, sehemu nyengine au mchango mwengine ambao ulichangiwa kwa aina moja na Waheshimiwa watatu; Kwanza ni Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa wa Kikwajuni, Mhe. Asaa Othman Hamad na Mhe. Omar Ali Shehe. Mipango yao au maswali yao kwa jumla tumeyaweka kwa pamoja ambapo ni kama *points* nne kama ifuatavyo.

Walitaka kujua kwamba kukua kwa uchumi bado hakujawasaidia wananchi kimaisha kumudu milo mitatu kwa siku. Pili, walitushauri kwamba serikali itengeneze mipango imara ya kuwawezesha vijana, ili waweze kujiajiri wenyewe au kuajiriwa katika sekta rasmi wanapomaliza masomo yao. Tatu, walituagiza kwamba tuimarishe sekta ya uvuvi. Mwisho, walitaka tutumie uvuvi wa bahari kuu ili kuwawezesha vijana kupata ajira.

Mhe. Spika, naomba nijibu kama ifuatavyo. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar inaonesha kuwa hali ya wananchi wa Zanzibar ni ya kuridhisha, kuongezeka kwa pato la Taifa ina maana kuwa tumeongeza uzalishaji. Vile vile, serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa jamii ili kuimarisha ustawi wao kwa kuendeleza uzalishaji na kutoa huduma ambazo tunaamini kwamba ndizo itakuwa chachu ya kuongezeka kipato kwa jamii. Hata kama kuna hali ya usawa kimapato, lakini wananchi walio wengi wanaendelea kupata huduma zote muhimu, ikiwemo chakula. Kwa mujibu wa takwimu za mapato na matumizi ya Kaya, umaskini wa chakula ni asilimia 13.

Mhe. Spika, nafikiri ni lazima tuseme ukweli, sote tunatembea miji mbali mbali ulimwenguni, tunaona hali ya umaskini ilivyo. Watu pale pakulala hawana, wanalala chini ya maghorofa kwa nyumba za vipolo, zinakuja mvua za masika hizi wote wanachukuliwa korela moja kwa moja, hiyo picha haifichiki. Leo Zanzibar kwa Unguja na Pemba nani analala nje. *Alhamdulillah* ni hali ya kuridhisha kabisa hii, ukizungumza mlo ndio usiseme. Watu wanakwenda kwenye *dustbin,* tunashuhudia, wanapekura mule chakula huko ninakosema Marekani. Marekani watu wanalala kwenye *train* mule *underground train* chini mule wenzetu wanalala, hayo hayafichiki. Leo Zanzibar yako wapi hayo, hakuna wanaolala nje, angalau tushukuru serikali yetu wazee wasiojiweza wameambiwa; Sebleni ipo, nyumba za Welezo zipo, watu wasiojiweza tunakwenda kuwasitiri kule.

Zaidi sasa mbali ya kuwasaidia tumewapa na chakula hao ndio watu wa chini. Kwa hivyo, kwa kweli tukilinganisha na kwengine ni lazima tujisifu tusingoje kusifiwa,

Zanzibar tumepiga hatua kubwa kabisa katika kupunguza umaskini na kuwalea wazee wetu.

Mhe. Spika, ushauri mwengine kuimarisha sekta ya uvuvi. Mhe. Spika, ushauri huo tumeupokea. Serikali hivi sasa inaendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana yenye lengo la kuzalisha, kuongeza na kutoa ajira za staha na heshima kwa vijana wanaomaliza masomo yao. Serikali inaendelea na juhudi ya kuimarisha sekta ya uvuvi kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi, kuongeza ajira kwa wananchi na kuwa ni lishe muhimu kwa wananchi. Katika juhudi hizo serikali inaendelea kutekeleza programu mbali mbali za uvuvi, kama zilivyooneshwa katika kitabu cha mpango wa maendeleo kwa mwaka 2015/2016, kwenye ukurasa wa 137 hadi 139. Programu ya kuimarisha uvuvi ambayo inatarajia kutekeleza miradi ifuatayo Mhe. Spika, ni kama ifuatavyo.

Mradi wa kuendeleza uvuvi wa Bahari Kuu ambapo serikali inashirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika la *JICA*. Mambo muhimu yatakayofanyika ni pamoja na kujenga soko na diko la samaki hapo Malindi. Pia, mradi wa ufugaji wa mazao baharini, mambo yanayotarajiwa ni kusaidia uwekezaji wa miundombinu katika kujenga kituo cha utafiti na kujenga kituo cha kuzalishia samaki. Vile vile, mradi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi katika ukanda wa Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi *SWIOFISH*. Mradi huu una madhumuni ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda, nchi za Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi, kuimarisha usimamizi wa uvuvi maalum utakaopelekea kuongezeka kwa jamii inayojishughulisha na uvuvi. Katika kuimarisha ajira kwa vijana, serikali imeweka moja ya kipaumbele katika mwaka 2015/2016 kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 42 hadi 43 ya hotuba yangu.

Aidha, serikali inaendelea kutekeleza programu ya ajira kwa vijana, ambayo imejumuisha uwezeshaji vijana kiuchumi katika miradi ya kilimo cha mauwa, mboga mboga, uvuvi wa bahari kuu, wafugaji wadogo wadogo na usafi wa mazingira. Aidha, mradi wa kituo cha biashara cha kutotolea wajasiriamali Zanzibar, yaani *Zanzibar Business Incubator,* unatekelezwa kwa ajili ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kwa kupitia mafunzo ya ujasiriamali, ili waweze kujiajiri wenyewe na wazalishe kwa tija.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuimarisha na kuongeza idadi ya vyuo vya amali nchini, pamoja na kuanza kwa programu ya mafuta na gesi zenye lengo la kuzalisha ajira zaidi kwa vijana. Mhe. Spika, serikali pia imeunda kamati maalum kwa ajili ya kushauri njia mahususi ya kuendeleza uvuvi wa bahari kuu, ambapo kamati hiyo ipo katika hatua nzuri za kufikia malengo yaliyowekwa.

Mhe. Spika, kwa kweli mipango yote hii kwa namna moja au nyengine imeshaanza na niseme kwamba ile *terminology* ambayo Waheshimiwa Wawakilishi nikisema wanacheka, lakini ndio ukweli wenyewe kwamba mipango yake inaendelea vizuri na *Inshaallah* utayari sasa vijana wetu tunawataka wasichaguwe. Kwa hivyo, wawe tayari kuchagua namna za kujiajiri wenyewe na tutapunguza idadi yao kungoja kazi serikalini.

Mhe. Spika, sasa naomba nimzungumze Mhe. Omar Ali Shehe, Mwenyekiti wa *PAC*, na yeye alikuwa na michango minne kama ifuatavyo. Yeye alishauri kwamba ni vyema kupatiwa tathmini ya MKUZA II, utekelezaji wake, changamoto na mafanikio kwa ujumla. Pili, alisema uchumi wetu unakuwa vizuri, lakini uhalisia hauko hivyo, uhalisia hauonekani. Tatu, mipango yetu haizungumzii namna ya kuweka thamani bidhaa, yaani *value addition* na Nne, mipango iwe na vipaumbele maalum vitakavyopewa uzito kwenye utekelezaji wa bajeti, kuliko mipango inayolenga kila kitu.

Mhe. Spika, serikali imekuwa ikifanya tathmini kila kipindi cha utekelezaji wa mipango wa mkakati wa kupunguza umaskini, kwa kila kipindi tukimaliza tunafanya tathmini. Awamu ya kwanza ya mpango wa kwanza wa kupunguza umaskini, umetekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu, kati ya mwaka 2002 hadi 2005. Mpango huu ulihusika na maeneo saba ya vipaumbele, ambavyo ni elimu, afya, kilimo, maji, miundombinu, utalii na masuala mtambuka. Tathmini imebainisha kwamba mapungufu katika mpango wa muda mrefu yamebainisha kuwa kuna mapungufu katika mpango wa muda mrefu na ufanisi wa kiuchumi haukuwa wa kuridhisha. Lazima tu-*admit*. Hata hivyo, sekta nyengine zilizopewa kipaumbele zilifanya vizuri.

Mhe. Spika, awamu ya pili ya MKUZA I ulianza mwaka 2007 hadi 2010 kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji. Mkazo uliwekwa katika kukuza uchumi, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuwa na *klasta* tatu ambazo ni;

1. Kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini wa kipato;
2. Huduma za jamii; na
3. Utawala bora na umoja wa kitaifa.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana yalikuwa ni kuimarika kwa uchumi na ustawi wa wananchi kwa kuwapatia huduma za kijamii, pamoja na kupata mafanikio katika huduma za afya na elimu, miundombinu na hasa umeme uliopelekwa Pemba kutoka Tanga. Katika kipindi hiki serikali ilitumia muda mwingi kuondoa mivutano ya kisiasa na kufikia maridhiano na kuletwa kwa kura ya maoni iliyopelekea kupatikana kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo ipo

madarakani hivi sasa, sambamba na kuanzishwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, awamu ya tatu ya MKUZA II ilianza mwaka 2010 hadi 2015. Maandalizi ya kuanza mchakato wa mapitio umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2016, ambapo kutakuwa na sura nzima ya tathmini ambayo imeanza kufanyiwa kazi na unataraji kuwashirikisha wadau mbali mbali, wote wa serikali na wa sekta binafsi ambao unajumuisha hata zile *NGOs* na wengineo.

Mhe. Spika, nadharia ya ukuaji wa uchumi ni pana. Kukua kwa uchumi wetu unakwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi ambayo yanamfikia kila mwananchi. Kuendelea kupatikana huduma muhimu za vyakula kutoka ndani na nje ya nchi, kuongezeka kwa miundombinu ya barabara mwaka hadi mwaka, kupatikana kwa huduma za kijamii kama vile afya na elimu na kadhalika, ni dalili kuwa uchumi wetu unakuwa sana.

Mhe. Spika, naomba hapa kumshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mgeni Hassan Juma. Kwa kweli mchango wake alioutoa leo ulikuwa *first class* kabisa, maana yake ile *lecture* alioitoa ni nzuri sana Mhe. Spika, na ninaomba tutaichapisha maalum ule mchango wake, kila mmoja wetu auone maana yake yeye amechukua maendeleo yote, kila sekta kaigusa na tumefanikiwa vipi serikali yetu kutekeleza. Kwa kweli nakupongeza sana Mhe. Mgeni Hassan.

Serikali Mhe. Spika, imekuwa ikifanya juhudi mbali mbali kuwasaidia wananchi kuweza kuweka thamani bidhaa zetu. Kwa sasa wajasiriamali wadogo wadogo wameweza kutumia rasilimali zetu kutengeneza sabuni, mafuta yanayotokana na viungo na kadhalika. Vile vile, serikali inashajihisha wawekezaji kuweza kuweka thamani bidhaa zetu.

Mhe. Spika, serikali imeanza mchakato wa kupunguza miradi kutoka miradi 57 mwaka 2014/15, mpaka kufikia miradi 37 mwaka 2015/16. Hatua ya kupunguza idadi ya miradi ni endelevu na ni matarajio yetu kuwa ni miradi michache inaweza kutekelezeka. Mhe. Spika, kwa ujumla kama nilivyosema Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunamshukuru kwa michango yake aliyoitoa na hasa alipoonesha mafanikio tuliyoyapata na tuna changamoto tunazozikabili kwa palipobakia.

Mhe. Hija Hassan Hija wa Kiwani na wewe tunakushukuru, ulizungumzia masuala ya sarafu, hayo mwenyewe Waziri wa Fedha atakuja kueleza. Lakini kwa ujumla mengi hasa uliyoyazungumza niseme kwamba nimeyagusa kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Mohammed Mbwana na wewe nakushukuru suala la Uwanja wa Ndege wa Pemba, Mhe. Waziri atakuja kusema, lakini hivi ninavyokuambia kwamba kazi tayari imeshaanza na huyo mjenzi yuko *onside*. *Inshaallah* tuwe na subra, nafikiri ndani ya mwezi mmoja mambo yote utayaona. Michango ya skuli, nikuambie sisi kama watu wa mipango tumeshiriki kikamilifu, kupanga kutizama mahitaji gani yanahitajika, halafu tukaishauri serikali sasa kwamba tukisamehe michango ile, tutaweza kuwasaidia sana wazee na watoto wasilipe michango ile na hatutoathirika na tutaweza, maana yake tumejipinda kifua kwamba tutaweza. Mwenyewe Mhe. Waziri wa Fedha, atakuja kusema, hatukwenda kivarange varange tu kwamba hatuna pesa tuzuie ile, hapana. Tumejipinda tukasema hapa kinachohitajika ni hiki, kuna mapungufu haya na haya, watoto wetu wanadhalilishwa.

Mhe. Spika, nasema kwa bahati mbaya baadhi ya walimu hawafuati yale wanayoelekezwa wanawafukuza watoto wasiingie skuli wasipochangia, kwa kweli haipendezi. Kwa hivyo, tumeona serikali moja kwa moja baada ya kutathmini, kuitizama hali na mwelekeo wetu wa uchumi, ndio pale tunaposema tujitahidi sana kuweka amani na utulivu ili *projection* zetu za mapato ziweze kupata fedha kukimu hayo mambo ambayo tunayasema. Kwa hivyo, tusiwe na wasi wasi Mhe. Mohammed Mbwana, kwamba haya mambo yamepangwa vizuri na hatukwenda kivarange varange tu, hapana.

Vile vile, ulizungumzia suala la kilimo, lakini watu wa sekta wenyewe watakuja kusema. Lakini sio nia yetu kuona kwamba pembejeo hazipo, nafikiri tumejitahidi sana hata kupunguza gharama za pembejeo, mbolea pamoja na dawa za magugu uliosema. Tumepunguza nafikiri *almost* mpaka kwa theluthi mbili ili wananchi wetu waweze kuona kwamba wanamudu. Sasa kama kuna watu wanauza dawa hizo za pembeni, basi inafaa tujiulize kama ulivyosema wewe wanazipata wapi na sisi tutazifuatilia ili tuone wanazipata wapi na tuone kwamba ile dhamira iliyokusudiwa kweli kweli ya kuwapunguzia mzigo wa pembejeo za kilimo na wao ziwafike ili kilimo kiende vizuri.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, tunakushukuru sana, uliuliza suala la kupunguka uzalishaji. Kwa jumla siku hizi *trend* ya watu wanaangalia kipato cha haraka haraka kiko wapi, tofauti na zamani wakati tulikuwa na kampeni zetu zile za kilimo, ambapo kama tunawalazimisha tunawapa malengo. Siku hizi ukiwapa malengo wanaangalia aah! nilime mpunga au nikalime tikiti, nilime tikiti au nikalime machungwa. Kwa hivyo, anaangalia *opportunity cost* iko wapi, ambapo kuna mwelekeo mzuri, kuna tija, basi huko ndiko anaangalia wapi ajielekeze mwenyewe kufanya. Sasa hayo mambo yako wazi wala hayataki nadharia ya kiuchumi, yako wazi tu, wakulima wengi wanakuambia nikalime mpunga gugu, hali ya hewa. Lakini nalima tikiti ana hakika, anakwenda kuvua ana hakika, analima machungwa ana hakika, soko la watalii liko bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk, tunakushukuru kwa salamu zako za undani kabisa kwa Mhe. Rais, kama nilivyosema tutazifikisha na wewe mwenyewe pia utusaidie katika kuimarisha suala zima la uchumi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid na wewe tunakushukuru sana na ulizungumza sana suala la ada za skuli. Kama nilivyozungumza kwa kweli serikali imeshajitayarisha na hatutorudi nyuma, nimesema linawezekana kabisa. Pia, ulizungumza suala la utafiti wa mazao na tiba ya matatizo ya mimea. Nayo tumesikia watu wa sekta watakapokuja nafikiri watali-*address* hili tatizo ulilozungumzia.

Mhe. Spika, kwa jumla niseme kwa upande wangu Waheshimiwa Wajumbe wengi kabisa wameiunga mkono hotuba hii na niseme kwa wale waliobahatika kuwepo kwenye semina ile uliyotuandalia kule *Zee Hoteli*, kwa kweli imetusaidia sana maana yake Waheshimiwa Wajumbe wengi waliokuwepo wamefaidika sana, na hata ile michango waliochangia leo umeona zaidi ya kuboresha.

Mhe. Spika, nimalizie na mimi kuwapongeza sana wale wenzetu waliokamilisha ungwe moja, nasema ile ni ungwe moja ya uteuzi wa chama chao na kupita salama, sasa tusubiri ungwe nyengine. Kwa hivyo, tutakiane heri na sisi ambao tunakuja mtusaidie kwa madua ili turudi salama kwa pamoja.

Mhe. Spika, niseme kwa wale walioshindwa wasione wameshindwa, mapambano siku zote tunasema Mapinduzi Daima. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Waziri, umefanya majumuisho hayo kwa muda mfupi lakini kwa uwazi, lakini kama ulivyosema inatokana na kwamba wenyewe Waheshimiwa Wajumbe mapema waliunga mkono hotuba yako. Wacha tuthibitishe sasa.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaowafiki mpango huu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2015/2016 wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, huu muda uliopo sasa sina hakika, waziri ana mambo mengi hautamtosha. Kwa hivyo, aje jioni huyu, kwa maana hiyo tusitishe shughuli zetu kutoka sasa ili tuje jioni wakati huo Mhe. Waziri wa Fedha atafanya majumuisho na nategemea pia atawasilisha ile miswada ya sheria ya fedha.

Ninachohimiza Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba tunaelewa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wangu walikuwa kwenye harakati kubwa na mpaka sasa hivi bado wengine hawajarudi na katika kazi kubwa unaweza ukachoka mno. Lakini hata hivyo kwa kuwa hivi sasa tumejaa vizuri nategemea na jioni tutajaa

zaidi ya hivi, ili tuwe na *quorum* ya kutosha kwa ajili ya kupitisha bajeti ya serikali ambapo majumuisho yake yatafanyika jioni, lakini pia kuweza kuzingatia miswada ya sheria ya fedha.

Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuwahi mapema mnamo saa 11:00 kama ilivyo Kanuni bila ya kuchelewa. Waheshimiwa Wajumbe, baada ya haya sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 6:18 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Spika**, Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kuna marekebisho ya *order paper* nafikiri mmepata na ndio maana Katibu akaita hati za kuwasilisha mezani, hii inatokana na ile kauli niliyoitoa pale mchana kwamba baada ya shughuli hii tunategemea Miswada ile ya Serikali kwa sababu ya sheria ile ya fedha itawasilishwa ndio iliyoleta hizo hati za kuwasilishwa Mezani, naomba basi kwa maana hiyo nimkaribishe Waziri wa Fedha.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha hotuba ya kuwasilisha mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Ushuru na kurekebisha sheria nyengine za fedha na sheria za kodi zinazohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani kwa niaba ya Mwenyekiti wa Wenyeviti kama ilivyo, naomba kuwasilisha.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2015/2016**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana mjadala tulifunga kuanzia pale mchana na kazi iliyobakia kwa sasa ni kumkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha ili kufanya majumuisho, naomba nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kwanza kabisa nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote wazima na kukutana tena jioni ya leo, aidha nataka nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara ya Fedha kwa kipindi cha miaka mitano. Ninaamini nimetekeleza majukumu yangu kwa uadilifu na uaminifu na kama kuna pahala nimeteleza basi Mhe. Spika, namuomba sana radhi Mhe. Rais.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo wa shukurani sasa nianze kwa kuwashukuru sana waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao ambayo wameitoa tokea jana wakati walipokuwa wanachangia bajeti ya Serikali, Mhe. Spika, michango ilikuwa ni mingi sana michango iliyoelekezwa kwenye Wizara yangu ilikuwa ni mia moja na kumi na tatu (113) na mimi nimejitahidi kuiweka katika makundi ishirini na tano (25) na nitaomba sana nitakapokuwa nafanya majumuisho Mhe. Spika, nijumuishe kwa hoja za makundi ili tuweze kufahamiana vizuri na tupunguze muda kama inavyotarajiwa baadae kuweza kusoma *finance bill.*

Mhe. Spika, nikianza basi, kwanza nataka nianze na ule usemi ambao ulitolewa jana kwamba "vijana enzini wazee ili na nyinyi mpate kuja kuenziwa", usemi huu ulitolewa jana na profesa Ali Mzee, nataka niseme kwamba hii itakuwa ni nukuu ya bajeti ya mwaka huu, vijana enzini wazee ili na nyinyi mpate kuja kuenziwa. Mhe. Spika, hili ndilo ambalo sisi vijana tumeamua kulifanya kupitia bajeti ya mwaka 2015/16. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa umoja wake na kwa upendo wake chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tumefanya maamuzi ya makusudi kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha wazee watakaoanzia miaka 70 na kuendelea tuanze kuwasaidia kwa chochote. Hii Mhe. Spika, haiondoshi dhima ya familia kumsaidia mzee, nimesikiliza sana hoja za waheshimiwa wawakilishi kwamba umri wa miaka 70 tushushe uanzie miaka 65, nataka niwaambie tu takwimu zinatuonyesha kwamba wazee tulionao Zanzibar wenye umri wa miaka 70 na kuendelea ni (27,366) jana profesa Ali Mzee alitwambia humu ndani wamo wawili tu waliofikia miaka 70 na kuendelea.

Sasa hao wawili na wenzao wengine walioko huko (27,366) nataka niseme tu Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu waikubalie Serikali tuanze na miaka 70 lengo letu hali kila mwaka inapokuwa nzuri tumekusudia kuishusha hii miaka hadi itakapofikia miaka 65 au chini ya 65, lakini kwa sasa hivi nakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe tuanzeni basi na miaka hii ya 70 na kuendelea. Ili hawa

wazee tuweze kuwasaidia kwa kupitia Serikali vile vile kuwaandalia maandilizi mazuri zaidi. Tumekusudia wazee hawa kuwapatia vitambulisho ambao popote pale watakapokwenda watapata huduma za awali, yaani *first track*, tumekusudia watakapokwenda hospitali wazee hawa waweze kuonyesha kadi yao, watakapoingia katika daladala tumesema wazee hawa waweze kuhudumiwa bure *(Makofi.*

Maandalizi tunayaandaa tutachukua kama miezi sita au saba kuweza kuwatambua wazee wote wako wapi na kuweza kuwapatia vitambulisho vyao, wazee wetu wa kizanzibari tunataka tuende huko, sisi tumezaliwa na tumelelewa hatuwezi tukawaachia wazee wetu hawa na wao wakayumba yumba tu, lazima tuwakusanye pamoja ili na sisi huko tunakokwenda tutakuwa wazee tupate na sisi kuenziwa kama nukuu ya jana ilivyotolewa na profesa Ali Mzee.

Mhe. Spika, jengine ambalo lililozungumzwa na Waheshimiwa wengi ni suala la kusimamia uimarishaji na ukusanyaji wa mapato ya Serikali, nataka niseme tu kwamba hili nimelipokea na hili litakuwepo kila bajeti itakapokwenda, kwa nini kwa sababu hamu ya kupata mapato zaidi inajionyesha, tulipoingia mwaka 2010/11 tulipokuja kwenye bajeti ya mwaka 2011/12 hili lilikuwemo na nikalipokea tuangalieni *Hansard* na nikasema nitalifanyia kazi, lakini nataka niwakumbushe tu Mhe. Spika, wajumbe wa Baraza lako tukufu tulipoingia mwaka 2010, mwezi wa Novemba, taasisi zetu mbili hizi kwa pamoja *ZRB* na *TRA* zilikuwa zinakusanya bilioni 13 kwa mwezi.

Lakini juhudi zenu waheshimiwa Wawakilishi za kunitaka mimi Waziri kusimamia na watendaji wangu vile vile kufanya kazi kwa uadilifu tumeweza sana sana tunakusanya bilioni 30 kwa mwezi, hizo sio juhudi ndogo na tulichokifanya kikubwa ni usimamizi kuliko hata ile haja ya kubadilisha kodi, kodi nadhani tumebadilisha nadhani mara mbili tu katika miaka mitano, zaidi tumesimamia. Tumesimamia na tumedhibiti, lakini nataka nikuahidini kwamba tutajitahidi kwa umoja wetu kuendelea kusimamia na kudhibiti mapato ya Serikali yasivuje.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala la kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama vile safari na semina na matumizi mabaya mengineyo, hili tumelipokea na kwa kweli tumeshaanza safari ambazo sio za lazima tumeshasema hili sasa hivi tutalikataa safari tutakayokwenda Mawaziri na Watendaji wetu ni zile ambazo zitakuwa za lazima na zile ambazo zitakuwa zina tija. Semina vile vile tutakazoziandaa ni zile ambazo zitakuwa za lazima na zile ambazo zitakazoleta tija, hili tumelipokea na tutalifanyia kazi kwa juhudi zetu zote.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wawakilishi ni suala zima la kupuguza misamaha na kwa ile miradi inayopata misamaha basi ni

ile ambayo itakayoongeza ajira na kuimarisha uchumi, hili tumelipokea na ndio kawaida tunavyofanya, miradi ambayo inaimarisha uchumi na miradi ambayo inatoa ajira ndio miradi ambayo kwa juhudi zetu zote ndio ambayo tunayoipa misamaha na huwa tunaiangalia katika *profiles* zao mwanzo wanavyotuletea tunaangalia jitihada za miradi hiyo itaongeza ajira kiasi gani na itakuza uchumi kaasi gani.

Mhe. Spika, jengine ambalo limechangiwa na Waheshimiwa hao ni kusiwe na urasimu kwa wawekezaji wanapokuja kuwekeza hapa kwetu, nataka nimpongeze sana Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini, amelieleza na amelitolea ufafanuzi wa kina na mimi sina zaidi ya kuongeza zaidi ya yale ambayo Mhe. Dk. Mwinyihaji, tutalisimamia na tutawaambia watendaji wetu kila itakapokuwa inabidi urasimu tuwache ili wawekezaji waweze kuja kuwekeza na kupata tija zaidi kwa nchi yetu.

Suala jengine lililozungumzwa na Weheshimiwa ni suala la Elimu kwa Walipa kodi, tumelipokea na tutaongeza jitihada zaidi, ukweli ni kwamba *ZRB* na *TRA* wanatoa elimu sana kwa walipa kodi, watoa kwa vyombo vya habari na vile vile wanatoa kwa mlipa kodi mmoja mmoja au kwa makundi, tutaongeza zaidi hizo jitihada na hasa kwa suala zima la utumiaji wa mashine za kulipia, kwa hivyo, tutaongeza jitihada hizo.

Mhe.Spika, jengine ambalo limezungumzwa sana ni suala la udogo wa *OC* na kutokutolewa kwa wakati, udogo wa *OC* Mhe. Spika, unategemea na hali yetu ya mapato, hali ya mapato itakapoimarika basi na *OC* zetu vile vile tutajitahidi ziimarike, tunachokifanya kwa sasa kila baada ya kulipa mishahara baada ya kulipa na ile dhima kwenye miradi ya maendeleo huwa tunagawa kilichobakia ili kiweze kwenda kama ni *OC*, tutajitahidi sana tutoe kwa wakati na hali itakapoimarika tuweze kutoa kingi zaidi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumziwa na Wawakilishi wengi tu suala la kodi za shilingi elfu mbili kwa abiria wanaokwenda Pemba na kurudi kutoka Pemba, wengine wameeleza kwamba kodi hiyo ni kubwa na wangine wameeleza kodi hiyo ni hivi, kila sababu zimetolewa. Nataka niwafahamishe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika *finance bill* kodi hiyo sasa itakuwa ni shilingi elfu moja, sio shilingi elfu mbili ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Hii katika zile zile jitihada zetu za kuweza kuwasaidia wananchi wetu, tulichokiona ni kwamba kodi hii inasaidia zaidi katika utengenezaji wa madawati, lakini vile vile tulichokiona kwamba maamuzi tuliyoyafanya mwaka jana tuliyatazama juu juu, tuliyatazama kwa msingi kwamba kila anayesafiri anayekwenda Pemba au anayetoka Pemba kuja Unguja ni yule mtu tunayemuita

hana kitu, lakini kuna wageni wanakwenda Pemba, kuna wafanya biashara wanakwenda Pemba, kwa hivyo, tunakosa hii kodi. Kwa hivyo, tukasema kwamba baadala ya kusema shilingi elfu mbili sasa na wao vile vile tuiweke shilingi elfu moja na ninaamini sana Mhe. Spika, kwamba kodi hii itatusaidia sana katika kuimarisha utengenezaji wa madawati.

Asilimia mbili ya mauzo ya umeme nayo vile vile ilizungumzwa jana, nataka niseme tu nitoe mfano, mtu ambae ananunua umeme shilingi elfu kumi kwa mwezi, atachangia shilingi mia mbili tu, mtu ambae atakuwa ananunua umeme shilingi elfu kumi kwa mwezi Mhe. Spika, atachangia shilingi mia mbili tu na hizo shilingi mia mbili zitakwenda katika mfuko wetu wa miundombinu. Mfuko huu tunalenga sasa Zanzibar ndugu zanguni kujitegemea, wahisani hawa wanaotusaidia wanatusaidia kupitia kodi za watu wao, wanaanza sasa kuwaondoka kidogo kidogo, hizi nyengine ni sababu tu utasikia kuna *EPA* ni sababu, kuna *ESCROW ACCOUNT* ni sababu. Lakini na wao wanafika pahala wananchi wao wanachoka, sisi tunasema sasa tuanze kujitegemea na mfuko huu Mhe. Spika, kwa hivi tulivyoweka kuchangia kidogo kidogo itafika wakati tutakuwa na mfuko ambao mzuri zaidi.

Mhe. Spika, nataka niwaeleze tu ndugu zangu Serikali imetengea biliano 4.5 katika mwaka huu kulipia umeme unaotumiwa katika visima vya maji, kwa sababu wenzetu ZAWA makusanyo yao hayawezi yakakidhi malipo ya umeme, kwa hivyo, haya tunachangishana sote Wazanzibari ili tuweze kusaidia kulipa umeme pamoja na kusaidia kupeleka huduma za maji pale ambapo inapohitajika.

Kwa hivyo, hii asilimia mbili tuliyoiweka hapa, ukifanya mahesabu kwa mfano kama Mhe. Spika, unatumia 50 kwa mwezi wewe utachangia shilingi elfu moja tu, yule ambaye atatumia zaidi ndio atakayechangia zaidi na anayetumia zaidi ni yule anayejiweza. Kwa hivyo, wale waliokuwa hawatumii zaidi, mtu anayetumia shilingi elfu tano umeme kwa mwezi atachangia shilingi mia tu, lakini tunajenga uwezo wa Wazanzibari wa kujitegemea, ndio kwa maan tumeiweka hii asilimia mbili ili weze kuja kutusaidia.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna wazo ambalo limetolewa na baadhi ya Waheshimiwa tuangalie uwezekano wa kuleta madaktari bingwa ili waje wafanye kazi na madaktari waliopo na hii itapunguza gharama za kupeleka wagonjwa kule India, nasema wazo sio baya, lakini madaktari wanaendana na vifaa, lengo letu kwanza kuipeleka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa *referral* kwa kuipatia vifaa hasa vifaa vya uchunguzi, wenyewe wataalam wa afya wanatwambia kwamba uchunguzi ndio muhimu sana ile *oppression* ni ya mara moja tu, ule uchunguzi ule ndio unaotakiwa.

Kwa hivyo, sisi tunataka twende huko, tukishakufanikisha kuipeleka Hospitali ya Mnazi Mmoja *referral,* ikawa na vifaa vya kutosha basi hivi sasa madaktari bingwa wanakuja, wanakuja madaktari bingwa kutoa Spain wanafanya kazi na madaktari wetu na tuna madaktari 90 sasa hivi na zaidi madaktari wa Kizanzibari lengo letu ni hilo na hili nataka niseme tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba ni wazo zuri na tukenda huko mbele litaweza kutusaidia sana ili kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nchini India au kwengineko.

Serikali tumetakiwa kuwa na vipaumbele vya Bajeti. Mimi nataka niseme kwamba hili ndio wazo miaka yote, miaka nenda serikali inakuwa na vipaumbele vyake, mwaka huu Mhe. Spika, nimevitaja, vipaumbele vyenyewe ni kama hivi vifuatavyo:

1) Ujenzi wa miundombinu, nikaeleza katika hotuba yangu.
2) Elimu, nacho pia nikaeleza katika hotuba yangu na
3) Afya.

Hivyo ndivyo vipaumbele ambavyo tumeviweka katika bajeti hii. Wazo la kuwa na vipaumbele mimi nadhani ni muhimu sana na sisi tutakuwa tunavitaja kila tunaposoma bajeti.

Mhe. Spika, jengine limezungumziwa kwamba serikali itengeneze mazingira ya kuongeza ajira katika sekta ya uvuvi, kilimo, ufugaji na viwanda vidogo vidogo. Nataka niseme kwamba sisi serikali kwa upande wetu tumetengeneza mazingira nataka niyataje baadhi ya mazingira tuliyotengeneza. Kwanza katika Sekta ya Kilimo tumetoa ruzuku kwenye pembejeo, sio ndogo, kwenye mbolea, kwenye mbegu, kwenye madawa, sio ndogo.

Lakini la pili Mhe. Spika, jambo ambalo tunaloliona sisi sasa hivi hapa Zanzibar ni kwamba *private sector* ya Zanzibar bado ni ndogo. Haya yote yangeweza kufanywa na sekta binafsi ili wananchi wetu wakaweza kupata ajira. Sisi tumetangaza tokea bajeti ya mwaka juzi, kama mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe tumeeleza kwamba mwekezaji yeyote atakayewekeza kwenye viwanda tumevi-*classify* viwanda ni *strategic investment,* atapata misamaha ya hali ya juu kabisa.

Tumeona kuna viwanda tayari ambavyo vimeshaanza kuwekezwa hapa Zanzibar, tatizo ni kwamba wengi hatutembei. Kuna viwanda hapa vimewekezwa viwanda vya *tissue paper* vipo hapa, viwanda vya *toilet paper* vipo hapa. Jana tuliulizwa hata kiwanda cha kutengeneza njukuti za kuchokolea masikio, vipo viwanda vimeshaanza kuwekezwa na *private sector* tena ni ndugu zetu wa kizanzibari

wamewekeza, kuna kiwanda cha maziwa na vyengine vitakuja. Lengo ni tushirikiane, lengo ni tuwaite sote na tuwakaribishe kwa moyo mmoja.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilozungumzwa sana ni suala la kubuni. Serikali imetakiwa ibuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitakuwa endelevu. Hapa nataka niseme kidogo, mimi nitafurahi sana kama waheshimiwa Wawakilishi watanisaidia kunambia kwamba chanzo hichi kipya chukua, nitafurahi sana.

Sisi tulikaa na wataalamu wangu, tukabuni vyanzo hivi tukaita mfuko wa miundombinu, kodi ya miundombinu. Sasa mimi nitafurahi sana kama Waheshimiwa Wawakilishi wataniambia chanzo hiki, hiki na hiki, nitafurahi sana. Nitakapovipata vyanzo hivyo tutavifanyia kazi kabla ya uchaguzi tutakuwa tumeshavifanyia kazi ili Waziri yeyote wa Fedha atakayekuja atavikuta vipo pale vimeshawekwa ataanza kuviangalia na watendaji ili kuvileta kwenye bajeti.

Mhe. Spika, nawaomba sana tutakuwepo hapa mpaka tarehe 30 Juni, 2015, kila Mwakilishi aliye na chanzo kipya aniletee tutajadiliana na watendaji wangu. Hiyo itatusaidia sana na sisi tunalo lengo hilo, kwa sababu vyanzo hivi vilivyopo sasa hivi tumevibana sana, ni bora kuwa kuna vyanzo vyengine vipya vya kuweza kutupatia mapato zaidi.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa na limesisitizwa sana na nashukuru sana profesa alilisisitiza sana hili, tuondokane na muhali katika kudhibiti fedha za umma, katika ukusanyaji na utumiaji. Nasema wazo ni zuri sana. Muhali ndio unaotuletea matatizo. Nataka niseme mifano miwili tu, na kesho nitajibu suali moja, kuna watendaji wawili, wafanyakazi wawili wa *ZRB* wamefanya udanganyifu na wakaiba shilingi milioni 19, tumewafukuza kazi. Kuna watendaji wawili wa *TRA* wamefanya udanganyifu tumewasimamisha kazi. Hawa wa *ZRB* tumethibitisha, tumewatimua hawa wa *TRA* bado uchunguzi unaendelea lakini tumewasimamisha kazi. Ukiwa na muhali hutafanya jambo lolote, watu watakuwa mapato hayakusanywi na matumizi yatakuwa yana ubadhirifu.

Kwa hivyo wazo hili la kwamba tuondokane na muhali, mimi nawaomba sana Mawaziri wenzangu, Makatibu Wakuu, tulisimamie tuondokane na muhali, tutumie sheria na tutumie haki, tusimdhulumu mtu tusimuonee mtu. Lakini tufuate taratibu za kisheria ili haki iweze kupatikana. Kwa hivyo hili tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa ni suala zima na uimarishaji wa kilimo hasa cha matunda na mboga mboga. Nataka niseme tu kwamba nia ya serikali ni hiyo na ndio kwa maana serikali yetu imetoa ruzuku katika maeneo ya

kilimo. Tutafanya hivyo na tutaendelea kuwasaidia wakulima wetu ili waweze kuzalisha vizuri kwa familia zao pamoja na kwa Taifa.

Jengine ambalo nilitakiwa kidogo nitoe maelezo na hili Mhe. Waziri Dokta Mwinyihaji Makame (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu) alipaswa kulitolea maelezo, lakini kwa sababu alilisahau au alighafilika naomba kidogo nilitolee maelezo. Tuliuliza kwamba suala la Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Kwanza nataka nikwambieni kwamba zoezi la taa Pemba limeshaanza na kama tutakwenda vizuri na programu ya uwekaji taa Pemba hatutofika mwisho wa mwezi wa Agosti taa zitakuwa zimeshawekwa. Wale waliotwambia basi tukaweke japo mishumaa, hatuweki mishumaa tunaweka taa hasa.

Lakini jengine ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, mimi mwenzenu juzi nilipata kuiona *design*. Kuna timu yangu ya Wizara ya Fedha inaondoka tarehe 23 kwenda *ADB*, moja tunaloliendea ni kuzungumza na *ADB* ili kuweza kupata mkopo kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Pemba. *Feasibility Study* inaangaliwa na wataalamu wa Tume ya Mipango pamoja na wataalamu wa Miundombinu na watalamu wa Wizara ya Fedha. Hatujauacha nyuma Uwanja wa Ndege wa Pemba. Uwanja wa Ndege wa Pemba *in case of emergency* ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar basi waweze kutua Pemba.

Lengo letu uwanja wa Ndege wa Pemba ni kuuongeza urefu, kuongeza kama mita 500, vile vile kuupanua upana hilo ndilo lengo letu. Lakini nakuomba Mheshimiwa Mwakilishi pamoja na Wawakilishi wengine tuvute subira tu kidogo, hali itabadilika chini ya Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, jengine ambalo nililoulizwa na Waheshimiwa ni suala la *GBS* tumefanya nini kama serikali. Nataka niseme tu kwamba makubaliano yaliyotiwa saini baina ya wafadhili na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kuisaidia Tanzania. Sisi tunapitia mgongo wa wenzetu na tuna asilimia 4.5. Sasa wale wanaposema kwamba wana *stop GBS* kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tabaan na Zanzibar haitokuja.

Tulichokifanya sisi tumezungumza na hawa wanaotusaidia, tumewaelezea kwamba matokeo yote mawili tokeo la *EPA* na tokeo la *Tegeta Escrow Account*, halituhusu Zanzibar, tukaomba kwamba kile ambacho walichokisia kwamba kije Zanzibar basi tuweze kukipata ili kiendeleze bajeti yetu. Lakini ndiyo haya niliyokwambieni, "*Mtegemea cha ndugu hufa masikini*", tujitegemeeni wenyewe. Kwa hivyo sisi wao wenzetu hawakufanikiwa na sisi hatukufanikiwa.

Lakini vile vile tuliulizwa hapa tumefanya nini juu ya kushuka kwa shilingi ya Tanzania. Nataka niseme tu kwamba kushuka kwa shilingi ya Tanzania na miujiza yoyote itakayofanywa wafanyaji ni Benki Kuu ya Tanzania. Kuna mambo ya msingi yaliyosababisha shilingi ya Tanzania ishuke, naomba niyaeleze machache.

Kwanza uchumi wa Marekani umeimarika, kwa hivyo fedha yoyote ile ndani ya dunia hii *against* dola imeterereka, thamani ya *euro* imeshuka, thamani ya *pound* imeshuka *against* dola na thamani ya shilingi yetu nayo imeshuka, hilo la kwanza.

Lakini la pili humu ndani *demand and supply* mahitaji ya dola yalikuwa ni makubwa zaidi kuliko mahitaji ya fedha nyengine yoyote. Kwa hivyo watu walikuwa na shilingi nyingi, wanataka kununua dola, kwa hivyo mahitaji yamekuwa makubwa kwa hivyo imelazimika shilingi ile kuanza kushuka thamani yake.

La tatu lilosababisha shilingi yetu kushuka ni kwa sababu hakukuwa na fedha, dola nyingi za ndani, misaada hatukuipata, bidhaa zetu tunazouza nje bei zimeshuka na *production* nayo imeshuka, kwa hivyo *export* zetu nazo hazikuweza kuingiza kwa wingi zaidi. Kwa hivyo shilingi yetu imeshuka. Lakini wataalamu wa BOT wamechukua jitihada.

Kwanza walilolifanya ni kuwaambia Mabenki ya Biashara kuongeza akiba katika Benki Kuu. Kwa hivyo sasa hivi akiba imepandishwa kutoka asilimia 8 mpaka asilimia 10 ili kupunguza *circulation* ya shilingi ya Tanzania katika soko, hiyo itaweza kuondosha shilingi 350 milioni kutoka katika soko itaziondosha. Kwa hivyo ikiziondosha shilingi zitakuwa na upungufu ndani zitaanza ku- *appreciate*. Lakini tunategemea vile vile kupata fedha kutoka Benki ya Dunia na *ADB* dola milioni 277 zitaingia kwenye soko. Tunategemea vile vile kupata mkopo wa dola milioni 800 zitaingia kwenye soko. Hizi juhudi tunategemea itaizuia shilingi sasa isianze kuporomoka au kuweza ku- *strengthen* thamani yake. Kwa hivyo juhudi zinafanywa na tuombe dua mazao yetu yaongezeke ili tuweze ku - *export* zaidi na kupata fedha nyingi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba niwatambue wale wote ambao waliochangia kwa kuongea nao ni kama hawa wafuatao:-

1) Mhe. Hamza Hassan Juma
2) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3) Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
4) Mhe. Raya Suleiman Hamad
5) Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
6) Mhe. Fatma Mbarouk Said

7) Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9) Mhe. Muhammed Mahmoud Mussa
10) Mhe. Omar Ali Shehe
11) Mhe. Ali Salum Haji
12) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
13) Mhe. Ali Mzee Ali
14) Mhe. Mussa Ali Hassan
15) Mhe. Asaa Othman Hamad
16) Mhe. Mgeni Hassan Juma
17) Mhe. Hija Hassan Hija
18) Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
19) Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
20) Mhe. Amina Iddi Mabrouk, na
21) Mhe. Mohammed Haji Khalid

Hao ndio waliochangia kwa kuongea. Naomba vile vile Mhe. Spika, niwataje wale wote waliochangia kwa maandishi kama kawaida yetu, nao ni:

1) Mhe. Salma Mussa Bilali
2) Mhe. Marina Joel Thomas
3) Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
4) Mhe. Asha Abdu Haji
5) Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, na
6) Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima sasa naomba nimalizie kwa kumshukuru sana Mhe. Dokta Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kutuamini na kwa kutupa dhamana.

Lakini vile vile naomba niwashukuru wasaidizi wake wawili Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad na Balozi Seif Ali Iddi Makamo wa Pili wa Rais, kwa michango yao na maelekezo yao waliyokuwa wakinipa mimi pamoja na Mawaziri wenzangu katika kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, naomba pia nikushukuru wewe, Naibu Spika, na wenyeviti wote kwa kutuongoza vikao vyetu hivi katika kipindi hiki cha miaka mitano ya awali. Naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati mbali mbali kwa kuisaidia sana Wizara yangu. Naomba vile niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa michango yao na misaada yao wakati tukiwa katika majadiliano na taasisi zetu mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba nimalizie mwisho lakini sio mwisho wa umuhimu kumshukuru sana mke wangu na watoto wangu, wamenivumilia kipindi chote cha miaka mitano nilipokuwa nawaambia nakwenda kwenye shughuli za Kitaifa, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Vile vile, namalizia kwa kuwashukuru sana watendaji Wakuu wa Wizara yangu na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu yangu mpenzi Khamis Mussa Omar. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kufanya majumuisho kwa dakika kama 37 tu. Nakushukuru sana, makofi mengi inaonekana wengi umejibu hoja zao.

Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba niwahoji wale wanaoafiki Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kazi za kawaida na Maendeleo kwa mwaka 2015/16 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2015**

*(Kusomwa mara ya Kwanza)*

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, Sheria ya Fedha inayohusu kutoza kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za kodi na zinazohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali ya mwaka 2015 inakusudia kufanya mabadiliko katika sheria mbali mbali kwa lengo la kudhibiti na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, mswada huu unaopendekezwa umefanyiwa marekebisho sheria zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar na Sheria nyengine zinazohusiana na mapato, na kuanzisha utaratibu na utozwaji wa Kodi ya Miundombinu. Sheria za Bodi ya Mapato Zanzibar zinazofanyiwa marekebisho ni kama zifuatazo:

1) Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi.

2) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

3) Sheria ya Ushuru wa Stempu.
4) Sheria ya ada ya Bandari.
5) Sheria nyenginezo inakusudiwa kurekebishwa ni Sheria ya Biashara.

Mhe. Spika, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa miundombinu, na kwa sababu ya dhima ya kuharakisha kujitegemea na kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nchi za nje, Serikali imependekeza kuanzishwa kodi maalum ya miundombinu, mapendekezo hayo yamo katika sehemu ya saba ya mswada huu. Kodi hii itakusanywa na kutumika kwa ajili ya kujenga na kuendeleza miundombinu iliyopo Zanzibar, kuanzia bajeti ya Serikali ya mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, Serikali pia imependekeza kufanya mabadiliko ya sheria mbali mbali zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato ili kuimarisha mapato ya Serikali na kuondoa kasoro zilizopo sasa katika sheria hizo, na kutokana na mabadiliko ya hali ya uchumi na mfumo wa biashara ulivyo Zanzibar.

Mhe. Spika, madhumuni ya waraka huu ni kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2015 unaotoa mapendekezo ya kubadilisha baadhi ya sheria za kodi na zinazohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato na kuanzisha kodi mpya ya miundombinu. Mswada wa Sheria hiyo umesambazwa kwa kila Mjumbe wa Kamati.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria umegawika katika sehemu 7 ambapo sehemu ya kwanza ya mswada inahusiana na vifungu vya utangulizi ambapo vinaeleza jina la sheria na utumikaji wake.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ya mswada inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi namba 7 ya mwaka 2009 ambayo inafanyiwa marekebisho yafuatayo:

a) Kifungu cha 3 kwa kuongeza maana ya maneno makisio ya kodi na cheti cha usajili ili kutoa maana halisi ya maneno hayo ambayo yametumika katika sheria.
b) Kifungu cha 5 kimeweka masharti ya mtu yeyote anayefanya biashara kuomba usajili kwa Kamishna.
c) Kifungu cha 9 kimeweka adhabu kwa mtu ambaye hajaweka cheti cha usajili katika eneo la wazi kama sheria inavyoelekeza.
d) Kifungu cha 15 kimeweka adhabu kwa mtu ambaye hajatoa taarifa ya kufunga biashara yake au kuwepo kwa mabadiliko ya biashara yake.
e) Kifungu cha 23 kimeweka adhabu kwa makosa yote yanayohusiana na utoaji wa risiti na kumtaka mlipa kodi kuziweka risiti katika utaratibu maalum wakati wa sasa kifungu hiki kinatoa adhabu kwa risiti tu.

f) Kifungu cha 32 kinazungumzia masuala ya kulipa kabla ya tarehe iliyoelezwa, hata hivyo kifungu kimefanya marejeo ya kifungu cha 31 badala ya 31(1) inayohusiana na malipo.
g) Kifungu cha 34(1) kimeondoa neno "nyengine" ili kutambua fedha zinazotumika kufanya malipo ya kodi kama shilingi, dola za Kimarekani na kadhalika.
h) Kifungu cha 52 kimefanyia marekebisho ili kutaka msaada wa Jeshi la Polisi kukamata mtu yeyote ambaye amefanya kosa chini ya sheria hii, ambacho kwa sasa kifungu hicho kimetaka msaada huo utolewe iwapo mtu kakwepa kodi au kumdhalilisha Afisa.
i) Kifungu kipya cha 53(a) kimeingizwa ili kuweka utaratibu wa kukubaliwa taarifa na nyaraka za mlipa kodi zitakazowasilishwa katika makosa ya kodi.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Stempu namba 6 ya mwaka 1996 kwa kufanyia marekebisho kifungu cha 3, ili mlipa kodi akitozwa kodi katika kiwango kilicho katika Sheria ya Kodi za Mafuta au Sheria ya Ada ya Bandari asitozwe katika sheria hii.

Mhe. Spika, sehemu ya nne ya mswada inafanyia marekebisho Sheria ya Ada ya Bandari namba 2 ya mwaka 1999 kwa kuruhusu kodi ya stempu isitozwe kwa huduma ya vyombo vya baharini, huduma ambayo tayari inatozwa chini ya sheria hii.

Mhe. Spika, sehemu ya tano ya mswada inafanyia marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani namba 4 ya mwaka 1998 kwa kuweka marejeo sahihi ya tarehe ya malipo ya kodi iliyoelezwa katika sheria ya usimamizi wa kodi *TAPA*.

Mhe. Spika, sehemu ya sita ya mswada inafanyia marekebisho sheria ya biashara ya Zanzibar namba 14 ya mwaka 2013 kwa kuweka kifungu kidogo cha 2 ili kumpa uwezo waziri kuweka aina nyengine za kodi na ada mbali mbali pamoja na kuweka majadueli ya ada na kodi hizo.

Mhe. Spika, sehemu ya saba ya mswada inaanzisha kodi mpya ya miundombinu ambayo imejumuisha maeneo yafuatayo:

1) Kutoza dola moja kwa mgeni yeyote anayelala katika hoteli zilizopo Zanzibar.
2) Kutoza shilingi elfu moja kwa abiria wanaosafiri ndani ya Zanzibar kwa kuondokea bandari za Zanzibar.
3) Kutoza shilingi 2000 kwa abiria wanaosafiri kutoka Zanzibar kuelekea bandari za Tanzania Bara.

4) Shilingi mia kwa lita katika bidhaa ya petroli na dizeli inayoingizwa nchini.
5) Asilimia mbili ya ununuzi wa umeme.
6) Asilimia 60 ya ada ya biashara ya bidhaa zinazoingizwa nchini.

b) Sehemu hii imempa mamlaka Waziri wa Fedha kuongeza vianzio, kupunguza au kubadilisha viwango kwa ridhaa ya Baraza la Wawakilishi.

c) Aidha Waziri amepewa uwezo wa kuweka utaratibu wa usimamizi wa kodi hii pamoja na kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2015.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupokee mswada huu kuupitia na hatimaye kuruhusu Baraza lako Tukufu kuupitisha.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha, sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nawakumbusha jambo moja tu, kwamba mswada wa aina hii pamoja na mswada ule wa *Appropriation Bill* ambao utakuja baadae ni ile miswada inayosomwa kwa mara ya kwanza, mara ya pili, na ya tatu kwa pamoja katika mkutano huo huo. Sasa msije mkaniuliza vipi mbona mambo yamekwenda kwa mpigo, ipo kwenye kanuni ya 100(4). Kwa hivyo aliposoma ile *long title* ilikuwa ndio anasoma kwa mara ya kwanza, kutoa maelezo ilikuwa anasoma kwa mara ya pili kwa ajili ya mjadala na baadae akaishia kutoa hoja, hoja ambayo mumeiunga mkono kwamba muko tayari kuweza kuijadili.

Niombe basi kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti ili aweze kutoa maoni ya kamati yake. *(Makofi)*

Nimemruhusu atumie teknolojia ya kompyuta, kwa sababu shughuli hii imekuja haraka haraka alikuwa haja-*print* kitu hii ndio hasa itakuja kwenye hata ile *hard copy* itaonekana hivyo hivyo.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti):** Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Wenyeviti, na mimi naomba nikushukuru kunipa nafasi hii ya mwanzo kuweza kuwasilisha hoja au kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Wenyeviti, ambapo kama nilivyokuomba kwamba kwa kuwa mswada huu umekuja kwa haraka sana, kwa hivyo sikuwahi kumaliza kuchapa na kuweza ku-*print,* kwa hivyo naomba uniruhusu basi niendelee kutumia hii teknolojia lakini ikisha-*charge* itabidi nimalizie kwa maneno.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu, kwa kuweza kukushukuru kwa mara nyengine tena kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwasilisha ripoti hii ya Kamati,

kama tulivyokubaliana na wenyeviti wenzangu katika mswada ambao ulikuja kwa haraka sana na tukaweza kuujadili.

Mhe. Spika, mswada huu wa fedha umekuja kwa nia ya kurekebisha sheria mbali mbali za tozo za kodi, kuanzisha tozo nyengine kwa madhumuni ya kuimarisha mapato ya Serikali na udhibiti wake ili kuleta ufanisi mzuri katika utekelezaji wa sheria hiyo pamoja na kusaidia maendeleo ya wananchi kupitia kodi hizo.

Mhe. Spika, ingawa mswada huu umeletwa kwa haraka kidogo, lakini kamati yangu imekaa na Wizara na Wataalamu wa Sheria wa Serikali pamoja na wa Baraza la Wawakilishi ambao wamesaidiana na Kamati yangu katika kuupitia mswada huu na kupendekeza marekebisho mbali mbali ya msingi kwa ajili ya kufanya mswada huu uwe unatekelezeka kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kamati yangu inaiomba Ofisi yako kwamba ingawa imekaa na Wizara kupitia Mswada wa Fedha, lakini tunaishauri katika kipindi kijacho basi mswada huu tuupate mapema ili tupate muda wa kukaa na wadau ili kuweza kupata mawazo yao, kwani kuna kodi nyingi hurekebishwa na walipa kodi wengi hasa wafanyabiashara huwa hawana taarifa na uelewa mzuri wa kutosha katika marekebisho hayo na kuleta usumbufu kwao, lakini pia kuweza kupata mawazo ya wadau hao ili kuweza kuwapa Wajumbe wako ili kuweza kuishauri Serikali namna bora ya ukusanyaji wa kodi Serikalini na vile vile kuibua vianzio vipya vya mapato.

Mhe. Spika, kazi ya kamati ya kuupitia Mswada huu wa Fedha isingekamilika bila ya mashirikiano makubwa iliyoyapata kutoka kwa Wajumbe wa Kamati ambao kwa heshima niweze kuwatambua kama hivi ifuatavyo:-

Kamati iliongozwa na Mwenyekiti ambaye ndio mimi mwenyewe hapa, Hamza Hassan Juma na Mhe. Omar Ali Shehe alikuwa ni Mjumbe, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa vile vile alikuwa ni Mjumbe, Mhe. Mgeni Hassan Juma vile vile alikuwa ni Mjumbe na Mhe. Hija Hassan Hija na yeye pia ni Mjumbe, Mhe. Mlinde Mabrouk Juma naye vile vile ni Mjumbe, Mhe. Ussi Jecha Simai vile vile ni Mjumbe. Lakini vile vile Ndugu Nassra Awadh Salmin Katibu wa Kamati pamoja na Khamis Hamad Haji vile vile ni Katibu wa Kamati.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mhe.Waziri wa Fedha kwa kuleta mswada huu lakini pia kwa kushirikiana na Kamati katika kuupitia na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali za Wajumbe, akishirikiana vizuri na watendaji wake na Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wao mbali mbali.

Mhe. Spika, kamati imeupitia mswada huu na kupendekeza marekebisho katika vifungu mbali mbali vya mswada ambavyo havikuwekwa vizuri katika maudhui yake.

Katika kifungu cha 4(1)(a) cha mswada kamati ilipendekeza kifungu hicho kiondolewe na sehemu ya adhabu iliyopendekezwa kifungu hicho kiondolewe na kubakisha adhabu ya faini isiyopungua shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 250,000/=.

Mhe. Spika, kamati yangu imeamua kuishauri Serikali kuondoa adhabu ya kifungo kwa kubakisha adhabu ya faini tu kwa sababu kwa kawaida masuala ya biashara ni masuala ya mapatano baina ya mtoza kodi na mtozwa kodi. Kwa hivyo ni vyema tukaweka adhabu ya faini tu ili kuweka mazingira mazuri ya biashara hapa Zanzibar hasa kwa kuzingatia kuwa nchi yetu inategemea uchumi wa huduma, na ndio maana kukaweko hata Mahkama Maalum ya Biashara yaani *Trade Tribunal*. Kwa hivyo ninaomba wajumbe kutuunga mkono kamati katika kuondoa adhabu hii na ninaamini tutakubaliana katika hili.

Mhe. Spika, kamati imependekeza marekebisho hayo kwa sababu kifungu hicho cha 4(1)(a) kinahusu adhabu ya hatia kwa kosa la mlipa kodi ambaye atashindwa kubandika hati yake ya usajili ya mlipa kodi katika sehemu inayoonekana ya biashara. Kamati imeona kuwa si busara kuweka adhabu ya kifungo kwa kosa hilo kwa mlipa kodi, kosa ambalo athari zake sio kubwa sana.Vile vile kamati imefikiria pia si busara kuweka adhabu ya vifungo kwa walipa kodi pale ambapo hakuna ulazima wa kufanya hivyo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 11 cha mswada huu kinachohusu kuwekwa kwa kifungu kipya cha 53(a) kwenye maeneo ya *proviso*, Kamati imefanya marekebisho madogo na kuongeza neno kama ushahidi baada ya neno itakubaliwa. Sababu za kuongezwa maneno hayo ni kuwezesha maudhui ya *proviso* hiyo yaende sambamba na maelezo yaliyotangulia yanayohusu taarifa za nyaraka yoyote ya mlipa kodi itakayopatikana na Afisa yeyote anayehusika na kodi kutumika kama ushahidi katika uendeshaji.

Mhe. Spika, kamati ilipokuwa ikipitia mswada huu imependekeza mpangilio mpya wa nambari ya kifungu cha 12 cha mswada kinachorekebisha kifungu cha 54(a) cha sheria mama kimefutwa na kamati imependekeza kuwa kifungu cha 13 cha mswada sasa kitakuwa cha 12 na vifungu vyengine vitafuata kwa mpangilio.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati kuhusu mlingano wa vifungu katika nakala ya mswada wa Kiingereza na Kiswahili katika kifungu cha 21(3) chenye orodha ya vyanzo vya kodi vya miundombinu. Kamati

inapendekeza kuweka kodi ya uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya Zanzibar ambapo itatozwa kwa asilimia 60 ya makusanyo. Maneno hayo yanaonekana katika nakala ya Kiingereza peke yake.

Mhe. Spika, kamati inapendekeza pia kuongezwa kwa kifungu cha 22 ambacho kitasomeka kama kinavyoonekana katika ukurasa wa 3 wa nakala ya marekebisho ya kamati kama ilivyosambazwa kwa wajumbe wote asubuhi hii.

Mhe. Spika, wakati kamati inapitia mswada huu kulikuwa na mjadala katika kifungu cha 21 kuhusu kuanzishwa kwa kodi ya miundombinu ambayo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 3 cha kifungu hicho kodi hiyo itahusisha vianzio katika malazi ya wageni, katika hoteli zilizopo Zanzibar, wasafiri kutoka bandari zote za Zanzibar kwenda katika bandari nyengine ndani na nje ya Zanzibar, kodi ya abiria anayeondoka kupitia na kuelekea sehemu nyengine yoyote ya Tanzania, kodi ya bidhaa za petroli, dizeli na mauzo ya umeme.

Mhe. Spika, hoja mbali mbali za Wajumbe zilizoibuka kutokana na kuanzishwa kwa kodi hiyo ya miundombinu katika vianzio vyake, zimekuja kwa nia ya kamati kutaka kuhakikishiwa kuwa kodi hizo hazitakuwa mzigo kwa mwananchi wa kawaida na badala yake zinasaidia katika maendeleo ya wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, katika kodi ya asilimia 2 ya mauzo ya umeme, kama inavyoonekana katika kifungu hicho cha 21 (3), kamati ilikuwa na wasiwasi kuwa huenda ikaongeza gharama za matumizi ya umeme kwa mwananchi wa kawaida. Naomba niwatoe wasiwasi wananchi kuwa, ongezeko hilo halitahusu kila *unit* moja ya umeme anayotumia mwananchi, badala yake itatozwa kutokana na gharama ya jumla ya mauzo ya umeme.

Mhe. Spika, mwananchi yeyote atakayenunua umeme wa shilingi elfu tano atalazimika kulipa asilimia 2 ya mauzo hayo ambayo ni shilingi mia moja. Sehemu kubwa ya kodi hiyo itaelekezwa katika maeneo mengine ya kuimarisha huduma za jamii katika miundombinu.

Kamati yangu haina tatizo na kuanzishwa kwa chanzo hicho cha kodi katika kodi ya Miundombinu, isipokuwa inasisitiza kuwa kila mtu anayetumia huduma ya umeme atalazimika kulipa kodi hiyo. Kumekuwa na utamaduni usio sahihi katika mashirika mengi ya umma ambayo yanatoa huduma ambazo wananchi huzilipia, lakini huduma hizo nyengine hutolewa bure kwa watendaji wa mashirika hayo.

Kamati yangu inatoa angalizo kwa serikali, kwa kuwa mashirika ya umma siyo sadaka, yanapotoa huduma zake lazima huduma hizo zilipiwe na faida ipatikane kwa Serikali. Kamati yangu inaitaka serikali kuhakikisha watendaji wote wa

Shirika la Umeme wote wanalipa huduma ya umeme na kodi ya mauzo ya asilimia 2 kama iliyowekwa kwa wananchi wengine na ihakikishiwe inalipwa kutoka katika mauzo.

Mhe. Spika, baada ya ufafanuzi wa kina wa hoja mbali mbali zilizoibuka wakati wa kupitia mswada huu, kamati yangu imeridhika na Mswada huu na tunatamka Mhe. Waziri kukubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya mswada huu kama yanavyoonekana katika waraka wa marekebisho ambao kamati umesambaziwa pamoja na Wajumbe wote.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza mambo ya msingi sasa naomba niingie katika yale mambo ya kiujumla.

**Mambo ya kiujumla katika mswada wa Sheria hii**

Mhe. Spika, kimsingi kamati yangu inaunga mkono marekebisho na mapendekezo yote ya sheria mbali mbali za kodi ili kuweza kumpa mamlaka waziri husika kuweza kuwa na maamuzi sahihi kwa mujibu wa sheria, lakini bado kamati yangu inaishauri serikali kuwa wakati umefika wa kutafuta vianzio vipya vya uhakika vya mapato.

Aidha, kuharakisha Programu ya *PPP* ili kupata makampuni ambayo yataingia nchini, yataingia ubia na serikali na kuweza kuanzisha na kuweza kuzalisha mali au kutoa huduma zitakazokuwa na tija zaidi kwa wananchi kwa gharama nafuu. Lakini pia serikali kuharakisha mpango wa kuanzisha mradi wa uvuvi wa Bahari Kuu ili kuweza kutoa ajira kwa vijana wetu, pia kuweza kupata mapato yatakayotokana na mazao ya samaki hao.

Jengine ni kwamba tukianzisha uvuvi wa Bahari Kuu basi pia tuanzishe na viwanda vya kusindika samaki hapa nchini ili kuweza kuwa na kitoweo cha kutosha pamoja na kuuza nje jambo ambalo linaweza kutuletea pesa za kigeni na kupunguza nakisi ya uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

Kwa hiyo, tunaiomba serikali kutafuta kampuni zenye uwezo ili kuja kuwekeza katika sekta hizo, na tunaamini zipo nyingi hapa Duniani.

Mhe Spika, kamati yangu bado tunaendelea kuishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuanza kuzisarifu karafuu zetu ili kuondokana na kuziuza kama zilivyo kwenye magunia jambo ambalo linaikosesha sana serikali mapato na ajira kwa wananchi kwa kiasi kikubwa. Tunaamini karafuu na mwani kama utasarifiwa hapa hapa Zanzibar basi zitaweza kuongeza mapato kwa kiasi kikubwa pamoja na kutoa ajira nyingi.

Mhe. Spika, kwa kuwa katika marekebisho haya ya kodi kuna tozo ya asilimia mbili kwa watumiaji wa umeme, basi wananchi wangelipenda hasa kujua hiyo asilimia ya kodi itakuwa kwa kila *unit* au kwa kila mauzo?

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi nafikiri hili aliweza kulitolea ufafanuzi kwamba ile kodi ya asilimia mbili haitakuwa kwa *unit* isipokuwa kwa mauzo ya jumla. Lakini pia je, tozo hiyo wananchi wangelipenda kujua itamsaidia nini mwananchi katika kuboresha huduma zake za maisha za kila siku.

Mhe. Spika, kwa kuwa kamati yangu iliweza kupata ufafanuzi wa kutosha katika hii tozo ya asilimia mbili (2) ya umeme, nadhani Mhe. Waziri ingelikuwa ni vyema yeye mwenyewe akaja kutoa ufafanuzi akaelezea hasa ile kodi ya asilimia mbili (2%) ya umeme inakwenda kumlipia mwananchi yule yule katika maeneo gani.

Mhe. Spika, kamati yangu inaitaka serikali kila inapotaka kuongeza au kutoza kodi mpya basi wawe na utamaduni wa kuwaelezea wananchi kupitia vyombo vya habari namna ya kodi hiyo itakavyoenda kutumika na faida gani wataweza kuipata kupitia kodi hiyo, kwani naamini kuwa wananchi wakijua tu basi hawatakuwa wagumu katika kuchangia kodi hiyo, kwani tumejifunza katika nchi mbali mbali ikiwemo Ulaya na Uingereza; hata wanapotaka kuongeza ada kwenye usafiri basi ndani ya vyombo hivyo vya usafiri utasikia matangazo ya kuwa kuanzia mwezi fulani bei ya *ticket* ya *train* au ya basi itaongezeka kwa kiasi fulani. Kwa sababu aidha wanataka kuboresha baadhi ya huduma au kuimarisha miundombinu ya usafiri. Kwa hiyo, wananchi hupata kujua taarifa hiyo mapema na kujua ikifika muda huo basi bei ya *ticket* hiyo itaongezeka kwa kiasi gani, na mara nyingi hujipanga hata katika bajeti zao binafsi za matumizi yao.

Mhe. Spika, kama nilivyoelezea katika hotuba yangu ya Ripoti ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali kwenye ada ya Bandari ambayo pesa zake zinakwenda moja kwa moja kwenye ununuzi wa madeski, basi kuwe na uangalizi maalum wa matumizi ya pesa hizo vyenginevyo tatizo la madeski linaweza kuwa ni mradi wa baadhi ya watu katika kujinufaisha wao wenyewe. Pia kamati yangu inaishauri serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuweza pia kuzitumia pesa hizo kwa kuyakarabati baadhi ya madeski yaliyoharibika ili kuokoa pesa nyingi za kuchonga madeski mapya. Kamati yangu tunaamini kuwa ikiwa yatakusanywa madeski hayo yaliyoharibika basi yataweza kuokoa kiasi kikubwa cha fedha hizo kwani yapo mengi sana ambayo yanaweza kutengenezeka.

Mhe. Spika, kuhusu kodi ya Miundombinu, tunamtaka waziri anayeshughulikia masuala ya fedha kuandaa kanuni kwa haraka sana itakayoweza kuweka utaratibu maalum wa ukusanyaji, mgawanyo pamoja na matumizi ya pesa hizo ili ziweze aidha kusaidia mifuko mingine au kutoa ufanisi mzuri kama ilivyokusudiwa, vyenginevyo inaweza pia kodi hii ikawa ni mradi kwa baadhi ya watu wachache kwa kujinufaisha wao wenywe.

Mhe. Spika, kwani tunaamini Mfuko huu utawezesha kusaidia na kuisukuma miradi na Mifuko mingine kama ilivyokusudiwa. Ninaamini kwa kweli ada hii ya miundombinu kama tulivyoelezwa basi itaweza kuondoa changamoto nyingi lakini vile vile katika mambo madogo madogo ya dharura yanapotokezea.

Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kuweza kunipa nafasi kwa kuwasilisha maoni haya ya kamati, kwa niaba ya wana kamati na vile vile Mswada huu kwa kuwa siyo mkubwa Mhe. Waziri ametoa maelezo ya kina na ya ufafanuzi. Kwa hiyo, kamati yangu inaukubali na tunawaomba Waheshimiwa waweze kuujadili, kutoa maoni kwa nia ya kurekebisha na kuimarisha na hatimaye kuupitisha na kumuwezesha Mhe.Waziri aweze kukusanya fedha ili kuweza kukamilisha au kuweza kutekeleza vizuri bajeti yake aliyotusomea kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, baada ya hayo maoni binafsi. Nawashauri Waheshimiwa Wajumbe waweze kuchangia mswada huu, pamoja na udogo wake mswada huu kwa kuwa tumeshapitisha Bajeti ya Serikali lakini bado tulikuwa hatujampa Mhe. Waziri ruhusa ya kuweza kukusanya hizo kodi ambazo tulizokwishakuzipitisha katika bajeti hii.

Kwa hiyo, naamini mswada huu sio mkubwa na ninaamini Waheshimiwa Wajumbe wataweza kuuchangia na kuunga mkono ili sasa kuipa nafasi serikali yetu kufanya kazi iliyokusudia ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kamati tunaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kamati. Mjadala unaendelea kwa ujumla na nimkaribishe basi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana jioni ya leo kwa kuweza kusaidia kuchangia mswada huu ulioletwa hapa mezani kwetu, ili kuweza kutoa mambo ya kumsaidia Mhe. Waziri katika utekelezaji wake.

Kwanza mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri, na mara nyingi kama angekuwa ananifuatilia *hansard* zangu nilikuwa ninaelezea jinsi gani ambavyo tunaweza kutafuta kodi zilizokuwa haziumizi raia wetu kwa *style* ya aina yake. Aminia! Kama angekuwa ananifuatilia kweli basi nafikiri kumbe anani-*copy* vizuri, naamini hivyo anani-*copy* vizuri kwa kutengeneza sheria. Kwa sababu mimi nakuwa nasema tu yeye kumbe ananitengenezea sheria na ndivyo ilivyo lazima watu kupeana vijiti, namshukuru kwa hilo kwa kutimiza wajibu wake.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na huu mswada wala sina tatizo nao hata kidogo, lakini kuna mambo naomba Mhe. Spika, unisaidie, bado kuna vitu vyengine amesahau kuviongezea vionjo ili kupata kodi zaidi na eneo moja hasa katika zao letu la kitaifa la karafuu. Mimi nafikiri hapa nitazungumza yeye atengeneze sheria, angetafuta mbinu na humo tukapata angalau kiji-*percentage* fulani kama katika sehemu nyengine. Kwa sababu hili zao ni kubwa la kitaifa linatia tija kubwa sana. Sasa naomba nayo itafutwe *style* yake aidha kwa kila kilo au kwa kila *gram* ya gunia ili kuweza kupata michangio na yeye kwa mujibu wa sheria hii ili aweze kutusaidia.

Mhe. Spika, naomba sana hilo kwa kuwa sheria hizi nyengine zinanipita pita na wakati, kwa hivyo siwezi nikazidi kutanua zaidi. Lakini ningeomba sana hili suala tuliangalie, kwa sababu ni zao, na hasa sasa hivi Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alivyolipa nguvu zaidi sana. Kwa sababu amelitolea motisha, na kwa kweli hata kwenye vitalu sasa hivi hamna miche ya mikarafuu, kwa sababu watu wameshaona umuhimu wake na tija zake zinavyoingia. Niishukuru sana serikali kwa kulitolea nguvu zaidi, motisha kwa walimaji wa mikarafuu sasa nalo hili tuone *style* ya kuweza kulichangia.

Mhe. Spika, binadamu yeyote hivi sasa na hasa huko tunakokwenda lazima tujenge, mtu kujenga ni lazima tupate pahala pazuri pa kukaa. Mimi naamini ndio utawala bora huo; maisha bora na utawala bora sisi tuwe nao, lakini kidogo nilishtuka hapa nikajiuliza Mhe. Waziri katika kutoa hukumu alifikiria utawala bora? Ametwambia kuna watu hapa wamechukua shilingi milioni 16, mimi nikajiuliza shilingi milioni 16 hizo si chipsi za Forodhani tu, akasema amemfukuza mara moja nikashtuka, mimi ni mmoja katika mtaalamu wa kuwaelimisha watu nini maana ya dhana ya utawala bora.

Mhe. Waziri hapa alimsifu mzee wetu Profesa wangu Mhe. Ali Mzee Ali kuwa sasa tubadilike tusioneane haya. Nakubaliana nalo hilo naunga mkono na *hansard* yake imo mule. Lakini mimi ningeomba twende kwa mujibu wa sheria ya utawala bora, huyu mtu ningeomba Mhe. Waziri wakabidhi vyombo vinavyohusika, laa alisema tuwape masikini ya Mungu unajua mtu unapokaa kwenye kiriri hutoka maneno tu, hilo mimi namsamehe Mheshimiwa wangu najua hakufanya hivyo,

kuwa mara moja amemstopisha yule mtu, naamini hajafanya hivyo, amkabidhi kwa vyombo vya sheria vitaamua huyu mtu azilipe zile fedha au alifanya jambo bila kujijua, lakini kwa shilingi milioni 16 ni pesa za chipsi.

Mhe. Waziri kuna watu wanachukua mamilioni labda kwenye shilingi milioni mia sita lakini huko sio pahala pake leo nimeona kidogo nisaidie hilo.

Mhe. Spika, hivi sasa kila leo tunachimba mchanga, Mhe. Waziri msaada wake huu leo anataka tumsaidie vile vianzio ili kuzidi kupata pato la ndani, twende kwenye mchanga kila leo watu wanachimba mchanga. Sasa nalo hilo ataona atafute *style* yake kwa sababu namjua mtaalamu wangu *master* Uingereza. Mhe. Waziri aangalie kidogo nalo angalau na huko achote kwa sababu ni vitu ambavyo vitasaidia kutomnyonya huyu mwananchi wetu kwa sababu hali ngumu ya maisha. Sasa na hii kama kuna *style* anaweza kuifanya akapata kijiasilimia vile vile basi mimi naamini bajeti yetu ya keshokutwa itakuwa ni nzuri zaidi.

Kwa sababu katika jadweli lake hapa ameonesha jinsi gani alivyodokoa dokoa shilingi elfu moja, shilingi elfu mbili, mpaka *percentage* ya kila mauzo ya umeme. Sasa na hicho naomba sana nacho kianzio chengine hicho. Mchanga sasa hivi ni mali, nao angetafuta *style* yake hapo hamnyonyi mwananchi wake aa, hapo kuna tajiri. Kwa sababu eneo moja linavyochimbwa gari si chini ya mia ngapi kwa siku zinachukua. Sasa na hapo naomba sana Mhe. Waziri na hilo alitizame ili kuweza kusaidia zaidi mapato haya.

Mhe. Spika, lakini nimem-*quote* Mhe. Waziri katika uzungumzaji wake, alisema kuwa yuko tayari mlango wake uko wazi kuwa asaidiwe vianzio vyengine vipya. Mheshimiwa mimi niko tayari sana, niko tayari kumsaidia Mheshimiwa, na kama alivyosema *immediate* ataweza kutekeleza. *Concern* yangu ya mwanzo hii hapa nimempa vitu nataka nione jinsi gani atavyotekeleza hili la kwanza tu.

Jengine alikubaliana hapa na Dokta Mwinyihaji na amemuhimiza kuwa sheria ya *PPP* ifanye kazi haraka sana, sijui kama Mhe. Rais ameitia saini au bado. Sasa nayo hii Mhe. Rais kama ananisikia basi ningeomba aitie saini kwa sababu tayari wawekezaji tunao. Mimi ninao ndani ya mfuko si chini ya wawekezaji watatu tena hao ni matajiri sio vijitajiri, ni matajiri. Halafu basi, hawataki fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hata kidogo, wao wanataka kuweka fedha ndani ya Zanzibar lakini sheria imetukwaza.

Mhe. Spika, kuna sheria mbili zinanikwaza; ya kwanza sheria ya umeme bado hatujaletewa rasmi haiko *open*. Hii moja kidogo naomba Dokta Mwinyi aangalie, ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati, tuone vipi au jinsi

gani ya kuruhusu hilo jambo kwa sababu hapo ndipo tunapoanzia. Kwa sababu tukiwa na umeme wa kutosha viwanda vipo.

Siku moja nilisema hapa Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili akacheka. Mheshimiwa kuna mbegu ambazo zinatoa maziwa hazina *cholesterol* hivi vitu watu wawekezaji wapo. Juzi kuna mtu kanijia ananambia kokwa za boga zinatoa maziwa tena mazuri sana, na wako tayari kuwekeza, mimi nikiwaambia watu wanacheka lakini ni maziwa *first quality* hayana *cholesterol* ni mazuri kabisa. Lakini ukiangalia umeme wetu tuangalie unaweza ukaendesha viwanda vikubwa kama hivyo?

Sasa mimi naomba tulete sheria tuiweke wazi ikubalike ili tuweze kuleta viwanda tukainua uchumi. Kwa sababu mara nyingi sana mimi nasema Zanzibar sio kuwa ni masikini Mhe. Spika, kwa sababu tunao uwezo hapa wa nusu dakika tu, tukazitia fedha kuliko leo mtu unaambiwa ah, lakini Mheshimiwa hili suala tuliangalie vizuri sana.

Mhe. Spika, sheria hii tunampa uwezo Mhe. Waziri wa kuona wapi panastahiki ili aweze kuongeza kile cha kuongeza. Mhe. Spika, hili suala kama nilivyokwambia ni suala zuri sana, lakini nieleze tena na nifurahike sana leo umetwambia kuwa kuna yale majiko kuhusu ile habari inayoitwa *spirit* nayo ni moja kati ya kaumu ya mafuta ya taa. Mhe. Waziri ile watu walikupongeza sana na hii ndio ujabari unavyotakiwa, wamefurahi sana kwa sababu kama tunavyojua mazingira sasa hivi yanatoweka kwa nguvu sana na hususan katika masuala yetu haya misitu.

Mhe. Spika, misitu yetu inakwenda na maji, na kwa hiyo naomba ushujaa wako uendelee hivyo hivyo. Kuna kijifungu hapa cha sheria kinanipa tabu kidogo. Kifungu hiki kinasema hivi:-

Hili suala la kiwango cha faini kisichopungua shilingi laki moja (100,000) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000). Mhe. Spika, mara nyingi sana Mwanasheria Mkuu nasema tafsiri hii itakuja kukwazeni mbele, kwa sababu kila Mahakama itapokea vyake, Mahakama nyengine itakuja kumtoza mtu shilingi hamsini elfu au itamtoza mtu shilingi laki moja ndio faini. Lakini kuna Mahakama nyengine itamuweka mtu si chini ya hiyo laki tano, hebu tuweke lugha moja ya fasaha iwe moja tu, tukiamua kama laki moja iwe laki moja tusiongeze kitu chengine hapa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, unajua kila hakimu anahukumu vile anavyoona yeye. Sasa mimi naomba sana kifungu hichi ni kizuri napenda kukutumia sana lakini kina hatari yake huko mbele kwa sababu inawezekana kuwa wewe kama ufungwe miaka miwili, miaka mitatu kumbe yule sheria imempa na wewe ukaja kushangaa na

ukaja kusema kwamba itakuwaje na sisi tumesema kwamba isizidi miaka miwili, kumbe ana uwezo si chini ya hapo kumfunga yule mtu miezi miwili au mitatu.

Mhe. Spika, hichi kifungu kinalegalega kwa kweli, Mwanasheria hebu kiangalie vizuri hakijakaa vizuri kwa mujibu wa sheria ya sasa hivi. Kwa sababu sasa hivi tunakuwa na sheria ambazo tayari wenzetu ulimwenguni wanazidi kuzibadilisha ili ziendane na wakati.

Mhe. Spika, nizungumzie suala jengine la masikitiko kidogo tu, ulisema kwamba sasa hivi wawekezaji wetu tusiwasumbue hasa wa ndani. Lakini Mhe. Spika, naomba huyu mwekezaji wetu wa Chelezo. Mhe. Spika, Chelezo ni kimoja ambacho katika nchi hasa nchi yetu ya Zanzibar sasa hivi baskeli zetu ni boti kwa asilimia kubwa sana, na boti ambazo zinatia fedha na ndio maana tukafika pahala Mhe. Spika, ukawa una uwezo katika hiyo tiketi ikatwe shilingi elfu moja.

Mhe. Spika, hili naomba sana ni moja katika vianzio vizuri kwa sababu tunakimbilia kupeleka *dry-dock* Mombasa, *Dry-dock* yetu ya serikali ya Bandari bado haina vifaa vya kisasa, sasa nalo hilo pungufu Mhe. Spika, nalo hilo naomba sana tumeshalisema sana na mtu ameshafanyiwa utafiti wa mazingira, ameshapewa *certificate,* amekubalika kila kitu, binadamu makosa madogo madogo tuchukuliane, yamo kibinadamu, hakuna binadamu anayekamika na katika mazito watu hupunguziana.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Spika, sasa hivi kuna fununu watu wanahamia Bagamoyo kutaka kujenga Chelezo. Mhe. Spika, kikihamia Chelezo Bagamoyo tumeumia, kwa sababu Mhe. Spika, sisi mara nyingi sana tunakuwa hodari asilimia mia tunakuwa wabunifu tuko juu, na umaliziaji wake Mhe. Spika, inakuwa *poor* na hasa wenzetu wanatu-*copy* wanakuwa haraka sana kutu-*copy* kwa ile tume-*plan* sisi. Mhe. Spika, tumefanya mambo mengi sana, tizama *television* hapa katika *East Africa,* nani walioanza? Zanzibar, lakini leo tuko nyuma sana, ni kitu ambacho kinashangaza sana, ukweli tuuseme.

Sasa mambo kama haya Mhe. Spika, naomba sana na mutuelewe nini tulichokizungumza, Chelezo hichi kitahamia ameshafanya huyu mtu mfano kajenga huko si Chelezo lakini *especial* gati kimependeza tu na tayari huko karibu na eneo hilo atapewa. Sasa mimi namuomba sana Mhe. Spika, kuwa hili suala tulitafutieni ufumbuzi sana Mhe. Waziri, na kupitia kwa Dkt. Mwinyihaji Makame, mimi naamini hivyo. Dkt. Sasa hivi wewe ndio mpishi ndiye sasa wewe hapa ...

**Mhe. Spika:** Zingatia muda.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** wewe hapa ndiye mwenye uchumi wa Zanzibar kwa kumpelekea Mhe. Waziri, kwa sababu wewe utakuwa una uwezo wa

kuwa makampuni ya kuweza kuja kwako wewe na kutengeneza sheria na wakaanza kuwekeza hapa na kuweza kupata yale mapato ambayo tumekusudia.

Mhe. Spika, naona umewasha taa yako, kwa hivyo, kusema la ukweli nitoe pongezi kubwa sana. Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri tena namuombea dua, namuomba sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Mhe. Waziri, huyu hana doa, sijamsikia hata siku moja kudokoa wala sijamsikia watu kumsema kuwa Mhe. Waziri amechukua vijipesa.

Mhe. Waziri ni haki yake akiwa chini ya usimamizi wake wa Katibu wake na Naibu Katibu na Wakurugenzi wake, kwa kweli mpaka sasa sifa mbaya hatujazisikia, na kama zipo basi nasema ni *study* kweli na ni fundi kweli lakini siamini.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba nimuombe Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, mimi sina wasi wasi, ushindi tunao Chama cha Mapinduzi amchague yule amrejeshe ili tuwe naye katika ulingo huu atupe vitu kama hivi vya ubunifu.

Mhe. Spika, niseme nakubaliana naye Mhe. Waziri na Mswada huu naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru sana lakini awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia uhai na uzima tukaweza kufika hapa katika chombo hichi cha maamuzi.

Mhe. Spika, pia, nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa kutuletea mswada huu kwa ajili ya urekebishaji wa sheria hii ya fedha kwa kutaka aidhinishiwe fedha ili aweze kutekeleza Bajeti yake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, mimi sina tatizo na mswada huu, na hapa nilinyanyuka kwa jambo moja tu ambalo nataka nipate ufumbuzi wake katika suala hili. Mhe. Waziri aje anieleze uzuri.

Mhe. Spika, naomba serikali wananchi wanaotozwa kodi kwanza na wao tuwafikirie kuwa wao watoa kodi lakini wanahitaji kupata huduma iliyo nzuri, tupate huduma iliyo nzuri, kodi hizi zote zinazunguka kwa mtu pengine kwa kila siku kwa sababu hasa katika vianzio hivi vya kodi vya miundombinu, kila siku mtu anachangia katika utoaji wa kodi hii.

Kwa hiyo, tunaiomba serikali iwafikirie wananchi barabara zote hazipitiki kwa mashimo haziendeki, wale wana vyombo vyao na wanaichangia serikali lakini wao hawajaliwi na vile vifaa vyao walivyonavyo ili kuweza kupatiwa huduma nzuri

kwa jamii. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kupitia vianzio vyake hivi wanavyovitaka basi na wao waangaliwe kwa jicho la huruma.

Suala jengine Mhe. Spika, hasa lililonisimamisha ni kuhusu kianzio hichi ambacho abiria wanaoondoka katika Bandari ya Zanzibar na kuelekea Bandari yoyote ya Tanzania. Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri atakapokuja kwa sababu katika madhumuni amesema kuwa mswada huu unakusudia kuanzisha na kurekebisha tozo na kurekebisha baadhi ya sheria za fedha na kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali ili kuleta ufanisi mzuri katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Spika, wasafiri ni sisi kwa sisi tunaosafiri, na nimegundua katika Bandari ya Mkoani kuna tatizo ambalo kuwa unapofika pale Bandarini Mkoani kama umeondoka na mzigo huku tuseme wa bidhaa kama vitanda, kabati na nini ukifika pale mlangoni huondoki kama hujatoa pesa. Lakini sasa kinachonishangaza mimi ni kuwa pesa unaitoa wale wanaokwambia lete kiasi fulani hawakupi risiti. Kwanza tunataka tujue pale pana idara ngapi ambazo wanatoza hizi kodi, hawatoi risiti, sasa pengine mtu kachukua kitu kile kaagizwa akifika kule anakopeleka anatakikana ushahidi, na ukiwaambia kuwa wakupe risiti ni wakali kama kitu gani.

Kwa hiyo, hili Mhe. Waziri nakuomba kwanza utwambie pale Bandarini pana watu wangapi wanaokusanya kodi, kwa sababu tunasikia wanaofanya masuala hayo ni watu wa kilimo. Sasa kwa nini kama pesa inaingia kwenye mfuko wa serikali wasitoe risiti na hapa unapoegesha gari pahali popote risiti unapewa. Lakini je, leo pale unamtolesha mtu shilingi thalathini, arubaini bila ya kumpa risiti hii ni dhuluma. Kwa hiyo, hili Mhe. Waziri ndilo nililosimamia hasa kutaka kuambiwa ni nani pale wanaotoza pesa, na kwa nini hawataki kutoa risiti kwa ajili ya kumpa yule anayetoa pesa yake. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii adhimu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu angalau mpaka leo hii ninayozungumza na sote tuliokuwemo ndani ndio pumzi zake Mwenyezi Mungu tuliokuwa nazo na tunazoringia.

Mhe. Spika, muda mchache uliopita tumeunga mkono sisi sote Wawakilishi kwa kuitakia mema Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye anaongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa, Bajeti hii ambayo punde tuliipitisha. Kwa hivyo, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini matumaini yetu ambayo tunayowakilisha wananchi fedha hizi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu *inshaallah* itakapokuwa zinakusanya na kupitisha sheria hii, matumaini kwamba wananchi tunaomba waje wafaidike kuondosha kero hizi ndogo ndogo ili isaidie maendeleo yetu na isaidie bajeti yetu.

Kwa niaba ya wananchi wa Uzini na mimi mwenyewe binafsi hichi kipindi Mhe. Spika, ni lala salama kama ulivyosema, wenzetu wameshakuja na sisi tunateremka kilima jua limeshatua. Kwa hivyo, mimi naunga mkono baada ya Bajeti na hii sheria na wizara inayohusika naitakia kila la kheri, na naunga mkono asilimia mia zaidi ya mia kupitisha sheria hii ya kodi. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika hapa, na wewe nakushukuru vile vile Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ili na mimi kuchangia mswada huu wa kutoza kodi.

Mhe. Spika, nchi zote duniani zinaendeshwa kwa kodi na zinasimamia kodi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naiomba Wizara ya Fedha isimamie kodi, tena iwahakikishe watu wabadhirifu wa kodi kwa sababu tunaweza tukasimamia kodi, lakini wale wasimamizi nao wakiwa si waamifu, wananchi watatoa kodi lakini fedha ikawa zinakwenda katika tumbo nene, kwa hivyo maendeleo itakuwa hapana.

Mhe. Spika, vile vile, ningeliomba serikali kupitia wizara, tatizo kubwa jengine linalowakwaza wananchi wanaweza kutozwa kodi lakini kile kinachotozwa kodi hakipo, hawakipati, kwa mfano maji wananchi wanaweza wakaambiwa kwamba lipia maji lakini maji hamna, kwa hivyo, hii itakuwa ni mkakasi.

Mhe. Spika, mimi naiunga mkono sana sheria hii lakini naiomba serikali kupitia wizara yake ihakikishe kwamba inasimamiwa kodi na vinasimamiwa vitu vya kulipia kodi, tuna sekta chungu nzima sisi; kuna sekta za mchanga kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba, kuna sekta za mawe, sekta za umeme, sekta za maji, yaani kila kitu, kuna  sekta za ushuru. Lakini tatizo kubwa kwamba kuna baadhi ya mambo yatalipiwa kodi hayapo.

Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba nyanja zote zinazolipiwa kodi zipo na zinahakikisha zinatumiwa na wananchi na wananchi wanazipata ili pasiwe na tatizo la kukosa vile vinavyotozwa kodi. Mhe. Spika, nakushukuru mimi naunga mkono mswada huu mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nianze kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe...

**Mhe. Spika:** Niwaombe Wajumbe walioko nje nafikiri wamemaliza kusali sasa warudi ili tumalize hoja ilioko mbele yetu. Endelea Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Fedha:**Naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa michango yao na nataka niwahakikishie kwamba michango yao nimeipokea na tutaifanyia kazi.

Labda nianze tu kuwataja wale ambao wamechangia kwa kuongea, tukianza na:-

Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

Mhe. Bikame Yussuf Hamad

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali

Mhe. Abdi Mosi Kombo

Naelewa wengi walitaka kuchangia lakini kwa sababu mswada wenyewe ulikuwa umefahamika vizuri ndio wamekubaliana na michango ambayo imetolewa awali.

Mhe. Spika, nianze basi na kutoa ufafanuzi kwa baadhi tu ya maeneo ambayo nimetakiwa niyatolee ufafanuzi.

La kwanza ambalo Mhe. Mwenyekiti amelieleza ni suala zima wakati umefika wa kutafuta vianzo vipya vya mapato. Nataka nikubaliane naye kabisa Mhe. Mwenyekiti na kama nilivyosema awali wakati nafanya majumuisho tutakuwepo hapa kwa muda mpaka tarehe 30, nipo tayari kukaa na Mhe. Mwakilishi mmoja mmoja na kunielezea vile vianzio ambavyo alivyonavyo yeye kwa fikra zake nitavichukua, ili baadae nije nikae nifanye majadiliano na wenzangu pale ofisini ili tuweze kuona kwamba vianzio hivyo vinaweza vikatumika katika kutafutia mapato ya Serikali.

Lakini vianzio ambavyo tunavyovitafuta ni vianzio ambavyo endelevu *(sustainable sources of income, sustainable sources of revenue),* vianzio endelevu siyo vianzio ambavyo mvua ikinyesha mapato yanapatikana, mvua hakuna mapato hakuna. Sasa vianzio kama hivyo tutakuja kujadiliana, lakini ninasema kwamba wazo la Mhe. Hamza Hassan Juma ni wazo zuri sana na tutalifanyia kazi.

Jengine ambalo Mhe. Spika, ambalo Mhe. Hamza ametaka kidogo nitoe ufafanuzi wa asilimia 2. Nadhani nilipokuwa nafanya majumuisho nimetoa ufafanuzi, lakini nataka niseme tu kwamba asilimia 2 ya umeme ya manunuzi ya umeme, hii itasaidia sana kulipia vyanzo vyetu vya maji. (*Makofi*).

Sasa hivi Serikali tumebanwa kuisaidia *ZAWA* shilingi karibu milioni mia tano kwa kila mwezi. Kwa sababu makusanyo ya *ZAWA* hayakidhi mahitaji ya umeme unaotumika kwenye visima vyetu. Kwa hivyo tumeanzisha hii. Kule wenzetu Tanzania Bara wana kitu wanakiita *REA*, wanayo asilimia tano. Wao wanapeleka

umeme vijijini, wote Tanzania Bara kule wanachangia asilimia 5 kwenye umeme lakini wao wanapeleka umeme vijijini.

Sisi umeme wetu umeshafikia asilimia 85 Wazanzibari; asilimia 85 tayari tuna umeme. Kwa hivyo tumesema kwamba tuendeleze na hivi vitu vyengine ili navyo viweze kufikia asilimia 85. Lakini vile vile baadae tutakuwa na utaratibu wa kuanza kufikiria kuwawekea *solar pump* wenzetu wa *ZAWA* ili waondokane na kutegemea huu umeme ambao una gharama kubwa. Hilo ninafikiri Mhe. Hamza nimsaidie na tutaendelea vile vile kutoa elimu.

Lakini umesema kwamba tutoe elimu kwenye hizi kodi ambazo tunazozianzisha. Mimi nakubaliana na wewe, tukishakuziidhinisha hapa Mhe. Spika, kwa sababu kodi Serikali inazianzisha kwa idhini ya Baraza la Wawakilishi. Kabla ya mimi sijapata idhini siwezi kuzitolea matangazo. Lakini tukimaliza hapa tukipitisha *finance bill* mheshimiwa akisaini *finance bill* tayari mimi ninaanza kuzitangaza hizi kodi mpya ili wananchi waweze kutufahamu. Kwa hivyo hilo Mhe. Hamza nakubaliana na wewe na Waheshimiwa wengine tutafanya hivyo ili wananchi wetu waweze kutufahamu zaidi.

Umesesma vile vile fedha tunazopeleka kwa ajili ya madeski kuwe na uangalizi mzuri ili isije ikawa ni mradi wa mtu au mradi wa watu. Mimi ninadhani tuna ile sekta ya Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Sekta chini ya Mhe. Mgeni Hassan Juma. Ninadhani wao vile vile wachukue hiyo *role*, sisi kwa upande wetu Hazina tutachukua *role* hiyo tuwe tunaziangalia kwamba fedha zile tulizozipeleka zimekwenda kutekeleza yale tuliyokubaliana. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ataangalia *value for money*, ataangalia vile vile je, deski kweli thamani yake hii, kwa pamoja tutafika pahala tutajua aah! wenzetu wa Wizara ya Elimu kweli wanatumia fedha kama tulivyokubaliana na wanazitumia kwa ufanisi au laa. Sasa kama ni laa, basi tutamtafuta nani anafanya vitendo hivi, tutaangalia wapi ambapo anaweza akachukuliwa hatua achukuliwe hatua. Kwa hivyo mimi ninakubaliana na wewe kabisa Mhe. Hamza katika hili.

Kodi ya miundombinu, umenitaka niandae Kanuni haraka sana. Ninakubaliana na wewe. Kuna mambo mawili. La kwanza nitaandaa Kanuni haraka sana lakini la pili tutatengeneza *notice* ya haraka sana ili kuanzisha mfumo wa miundombinu. Haya tutayafanya katika kipindi cha miezi miwili mitatu, tutahakikisha kwamba tumeweza kuyakamilisha ili hizi kodi ziweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ninakushukuru sana umeeleza kitu nilikuwa ninanong'ona na wenzangu hapa Mawaziri kwamba ume-*raise point* muhimu sana. Tuliangalie zao la karafuu kuna kodi gani mule ndani ya zao la karafuu.

Zao la karafuu ni endelevu, kila mwaka tunazalisha karafuu lakini tunapishana kwa viwango. Tutaliangalia kwa undani na kama kuna uwezekano wa kuangalia *atleast* na wale ambao wanaouza karafuu zao, nilikuwa ninanong'ona na wenzangu ninawaambia hivi tutaliangalia kwa upana zaidi sitaki niyatolee maelezo zaidi sasa hivi.

Nilikuwa ninaangalia kama mfanyakazi wa Serikali anapata mshahara wa shilingi laki mbili, kila kilichozidi laki na nusu kinatozwa kodi. Sasa na huku nako tuangalie, sio wauzaji wa karafuu tu, tuangalie na mazao mengine ambayo ni endelevu. Tutajaribu kuangalia kitu kama hicho lakini tutaangalia kwa misingi kwamba hatutaki tuje tumuumize mkulima, hatutaki tuje tumuumize mwananchi wetu wa kawaida, tutaiangalia.

Umezungumzia kodi ya uchimbaji mchanga. Hizi ni zile kama munakumbuka asubuhi niliulizwa hapa kuhusu kodi za Halmashauri na Mheshimiwa Mwakilishi mmoja hapa. Hizi zipo kwa Halmashauri, vile vibali vya Halmashauri na vyengine. Tutaangalia zaidi tutakaa na mwenzangu Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa tuweze kuoainisha na kuweza kuona vyanzo vipya ambavyo ni endelevu, ndivyo tutakavyovifanyia kazi.

Suala la uwekezaji ambao wapo tayari kuwekeza katika sekta ya viwanda. Hebu tukae Mhe. Mshimba utueleze hao wawekezaji ni wawekezaji gani, sekta gani ya viwanda, halafu utaona jinsi gani tutakavyoweza kuwapeleka *ZIPA* wapate hizo *facilitation* waweze ku-*process* na uweze kuwakaribisha. Tunavihitajia viwanda, hatuwezi tukakaa tu tukasikia maneno wapo wapo na sisi tunasikiliza tu. Lazima tusikie kwa vitendo, tufanye kazi kwa vitendo. Ninasema kwamba acha tukae tuwafanyie kazi.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad ulizungumzia kwamba walipaji kodi wafaidi kodi zao. Ukataja mfano mmoja tu wa barabara. Mimi nataka nikwambie kwamba kodi yoyote inayokusanywa lazima irudi kwa walipa kodi, irudi katika sekta zote unazozijua wewe. Sekta ya barabara. Sasa hivi kilomita moja ya barabara kuijenga inatugharimu dola milioni moja, *one kilometer, one million dollar.*

Sasa lazima irudi imsaidie mwananchi. Sekta ya maji, sekta ya elimu, sekta ya afya na sekta nyengine. Hii ndiyo kodi itakuwa na tija kwa wananchi wake, lakini kama kodi inakusanywa inawasaidia watawala tu, watawaliwa haiwasaidii, hiyo siyo kodi.

Mimi ninataka nikubaliane na wewe Mhe. Bikame kwamba kodi lazima zirudi na tutahakikisha kwamba sisi Wizara ya Fedha tunakusanya hizi kodi, tunapeleka kwenye sekta na sekta nayo wahakikishe kwamba wanawapatia wananchi katika zile huduma ambazo wanazozihitajia. Vyenginevyo itabidi tukiingia humu ndani

kwenye Baraza tuulizane maswali, tumekupa wewe bilioni thalathini umefanya nini kwenye sekta ya maji, tumekupa wewe bilioni kumi na nane, umefanya nini kwenye sekta ya elimu, utwambie ulichokifanya kwenye sekta ya elimu ili kuona kwamba ile kodi imerudi kwa wananchi.

Mimi ninataka kwamba hilo tutalifanyia kazi. Suala ambalo umeniuliza nilitegemea labda baadae ningepata kunong'ona na wenzangu, pale bandari Mkoani kuna wakusanyaji kodi wangapi. Nilitegemea ninong'one na wenzangu niweze kuwajua, kwa sababu kuna watu wa kilimo pale, kuna watu wa mazao, kuna watu sijui wa wanyama pale, sijui kuna watu gani.

Lakini ninataka nikwambie Mhe. Bikame, hata kama kuna mtu mmoja, hata kama kuna watu wawili, hata kama kuna watu kumi au ishirini wanaokusanya kodi lazima wakupe risiti, lazima watoe risiti. Anayechukua pesa yako asikupe risiti, tafuta utaratibu wa kupeleka mashitaka yako katika taasisi zinazokuwepo hapo Bandarini. Kuna Polisi, lazima wakupe risiti, kufanya hivyo maana yake ni kuiibia Serikali. Kwa hivyo hakikisha wanakupa risiti, akikataa kukupa risiti kamchukulie Polisi mwambie huyu kanilipisha kitu fulani hataki kunipa risiti yangu.

Mhe. Mohammedraza Hassanali umeunga mkono Mswada huu na mimi ninakushukuru sana, kama kawaida yako mambo ya Serikali unayaunga mkono na mimi ninakushukuru sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo alisema kuwa Wizara ya Fedha isimamie kodi ili ipatikane kwa ukamilifu.

Mhe. Spika, nilivyomueleza Mhe. Hamza tutasimamia. Hilo ndilo jukumu letu la msingi la kwanza. Wizara ya Fedha jukumu lake la msingi la kwanza ni hilo, hawana jukumu jengine la msingi ni hilo. Kwa hivyo tutalisimamia kwa juhudi zetu zote, tusimamie pia maeneo yanayolipiwa kodi, lazima yaendane sambamba, unaisimamia ile kodi na kodi hiyo inatolewa kwenye eneo gani. Haya yote lazima tuweze kuyasimamia. Ndiyo nilijibu asubuhi, nikasema kwamba kuna maeneo kodi yake yanakusanywa na Serikali Kuu na kuna maeneo kodi yake inakusanywa na Halmashauri. Kwa hivyo lazima kuwe na *line of demarcation,* lakini sisi Serikali Kuu tuzisaidie Halmashauri ziweze kukusanya kodi zao kwa ukamilifu.

Ninataka nishukuru Mhe. Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi wote.

**UTARATIBU**

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake lakini kuna jambo moja nililisahau sana naomba radhi, nilikuwa nataka kabla hajahitimisha atusaidie ufafanuzi.

Mhe. Spika, katika bajeti kuu ya Serikali imetangaza kwamba itafuta ada za mitihani pamoja na ada zile za kiingilio kwa skuli za msingi, ninafikiri kama sikosei mpaka mitihani ya *form IV*. Sasa kwa bahati unajua sisi ni wadau wa elimu. Jana tu niliporudi nyumbani majira ya usiku kuna wananchi wangu walinifuata wanataka ada ya kuwalipia vijana wao mitihani ya *form IV.* Sikuwakatalia kwa sababu tunataka wapate elimu, lakini niliwaambia hebu nipeni muda nipate ufafanuzi wa Serikali. Je, hii ada inayofutwa kuanzia mwezi gani, kwa sababu bajeti hii tunayoipitisha, tunaipitisha ikishafika Julai ina maana tunaanza bajeti mpya. Sasa je, hii mitihani ya *form IV* tunategemea itakuwa *around* kwenye mwezi wa nane, wa tisa ambayo bajeti hii tumeshaipitisha.

Je, katika hili hebu watusaidie ufafanuzi Serikali ili na wananchi waweze kujua nini hasa imekusudiwa na Serikali.

Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Kabla sijamkaribisha tena Mhe. Waziri, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe walioko nje waje ili tutimize akidi ya kuweza kupitisha huu Mswada. Vyenginevyo itabidi tunakaa humu tutizame, tupige kelele, lakini kwa kweli ninadhani tujitahidi.

Watendaji pale tuwahimize Waheshimiwa Wajumbe warudi ili tuweze kuupitisha Mswada huu kwa mujibu wa taratibu za Kanuni zetu. Mhe. Waziri toa ufafanuzi wa kina kidogo juu ya hilo na mengine na Wajumbe watakuwa wanakuja kuupitisha huu Mswada. Karibu.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, Mswada wa Fedha tutakapoupitisha leo tarehe 19/05/2015, utekelezaji wake unaanza rasmi tarehe 1/07/2015. Ndiyo Mswada wa Sheria ya *Finance Bill* utekelezaji wake unapoanza. Kwa hivyo kama upo mtihani, kuanzia tarehe moja ile ada imefutwa. *(Makofi).*

Kwa hivyo, Serikali inabeba na italipia ada zote za mitihani kuanzia tarehe 1/7/2015. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe wakiingia ndani ili tupitishe Mswada huu. Hebu Katibu wahesabu Wajumbe waliopo.

Waheshimiwa Wajumbe ndiyo hali yetu na kama ingelikuwa Kanuni zinaruhusu vyenginevyo kuna msemo mmoja wa Kiswahili ningeutumia, "Ng'ombe anavyoanguka .....", lakini naona Kanuni inazuia nisifanye hivyo.

Lakini nitumie nafasi hii kuhimiza sana kwamba mahudhurio ni kitu muhimu sana, ni jambo kubwa kwa mujibu wa taratibu zetu. Hata ile bajeti tuliyoipitisha hivi punde basi isingekuwa na *quorum* ni sawa sawa kwamba bajeti ile haikupitishwa. Labda tungeweza kuahirisha tukatafuta utaratibu mwengine. Lakini na hii kama isingekuwa na *quorum* maana yake Mswada huu usipitishwe.

Tungepitisha bila ya *quorum* ikija hoja basi tumeanguka. Ni muhimu sana mahudhurio. Niwaombe Wanadhimu wanisaidie sana jambo hili, kwa sababu ni muhimu kutimiza wajibu wetu.

Waheshimiwa Wajumbe sasa ninayo taarifa kwamba Wajumbe wameshatimia, naomba sasa niwahoji, nimeambiwa arobaini na moja imetimia, akitoka yule mmoja haijatimia.

*(Hapa baadhi ya Wajumbe wanaingia ukumbini na makofi yanapigwa)*

Ninaelewa vile vile kwamba wengine wapo kwenye mfungo walikuwa wanapata maji na chai kidogo, lakini sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

Mhe.  Spika, naomba kutoa hoja.

**KAMATI YA KUTUNGA SHERIA**

**Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2015**

**Sehemu ya Kwanza**

**Utangulizi**

| | |
|---|---|
| Kifungu 1 | Jina fupi na kuanza kutumika |

**Sehemu ya Pili**

**Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya 2009**

| | |
|---|---|
| Kifungu 2 | Kusomwa |
| Kifungu 3 | Marekebisho ya Kifungu cha 3 |
| Kifungu 4 | Marekebisho ya Kifungu cha 5 |
| Kifungu 5 | Marekebisho ya Kifungu cha 9 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 6 | Marekebisho ya Kifungu cha 15 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 7 | Marekebisho ya Kifungu cha 23 pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 8 | Marekebisho ya Kifungu cha 32 |
| Kifungu 9 | Marekebisho ya Kifungu cha 34 |
| Kifungu 10 | Marekebisho ya Kifungu cha 52 |
| Kifungu 11 | Kuweka Kifungu kipya cha 53A pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 12 | Marekebisho ya Kifungu cha 54A pamoja na marekebisho yake |

**Sehemu ya Tatu**

**Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996**

| | |
|---|---|
| Kifungu 13 | Kusomwa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 14 | Marekebisho ya Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake |

**Sehemu ya Nne**

**Marekebisho ya Sheria ya Ada za Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999**

| | |
|---|---|
| Kifungu 15 | Kusomwa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 16 | Marekebisho ya Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake |

**Sehemu ya Tano**

**Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998**

| | |
|---|---|
| Kifungu 17 | Kusomwa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 18 | Marekebisho ya Kifungu cha 17 pamoja na marekebisho yake |

**Sehemu ya Sita**

**Biashara ya Zanzibar Nam. 14 ya 2013 pamoja na marekebisho yake**

**Mhe. Mwenyekiti:** Yaani hata hiyo *heading* ina marekebisho

| | |
|---|---|
| Kifungu 19 | Kusomwa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 20 | Marekebisho ya Kifungu cha 54 pamoja na marekebisho yake |

**Sehemu ya Saba**

**Kodi ya Miundombinu**

| | |
|---|---|
| Kifungu 21 | Kuanzishwa Kodi ya Miundombinu pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 22 | Usimamizi wa Kodi ya Miundombinu pamoja na marekebisho yake |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa imuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2015**

*(Kusomwa kwa mara ya Tatu)*

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2015 usomwe kwa mara ya tatu.

*(Hoja ilitolewa imuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2015 ulisomwa kwa mara ya tatu na umepitishwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii tena kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa ya kufanya shughuli zetu. Kumbe tukishirikiana vizuri namna hii mambo yanakuwa mepesi. Naomba sana kama mulivyoombwa na Mawaziri waliotangulia kutoa hoja zao na hata michango ya Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali katika kipindi hichi cha lala salama ndiyo munavyoita, basi tuwe na mashirikiano makubwa ili tuweze kutimiza shughuli zetu na tuweze kufanya mambo mengine ambayo yanakuja mara baada ya hapa.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya machache haya basi, sasa naahirisha kikao hichi kesho tarehe 20/05/2015, saa tatu barabara za asubuhi

*(Saa 1:04 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 20/05/2015 saa 3:00 asubuhi)*